**BUNGE LA TANZANIA**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Pili – Tarehe 31 Januari, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika(Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu kwa mwaka 2004/2005 *(The Annual Report and Accounts of the Marine Parks and Resources Unit for the Year 2004/2005).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 15

**Ukumbi wa Chimwaga**

**MHE. SAID AMOUR ARFI (k.n.y. MHE. PHILEMON NDESAMBURO)** aliuliza:-

Kwa kuwa Ukumbi wa Chimwaga ni wa Serikali:-

(a) Je, Serikali imekwishapata fedha kiasi gani kutokana na kuukodisha ukumbi huo?

(b) Je, Serikali inatumia kiasi gani cha fedha kuukarabati?

(c) Je, ni Taasisi ngapi zimekwishatumia Ukumbi huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kwa kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni kweli Ukumbi wa Chimwaga uliopo hapa Dodoma ni wa Serikali na umekuwa ukitumika

kwa shughuli za Mikutano ya Taasisi mbalimbali za hapa nchini. Ukumbi huo upo pahali pazuri na muafaka kwa ajili hiyo. Ukodishaji wa Ukumbi huo ni Tshs.300,000/= kwa siku. Huduma zilizopo Chimwaga ni pamoja na Ukumbi wenye uwezo wa kutosha watu takriban 3,000, maji na umeme na uko umbali wa kilomita 8 nje kidogo ya Mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, kwa heshima na taadhima, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ndesamburo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kutokana na kukodishwa ukumbi huo, Serikali imekwishapata kiasi cha Tshs.5,250,000/=. Fedha hizi ni makusanyo ya ukodishaji kati ya mwaka 1992 hadi mwaka 2006.

(b) Mpaka sasa zimeshatumika kiasi cha Tshs.5.25 bilioni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa jengo hilo.

(c) Taasisi ambazo zimetumia ukumbi wa Chimwaga ni:-
Chama cha Mapinduzi (CCM) Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

Mheshimiwa Spika, napenda kuitumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekwishaamua kwamba Ukumbi wa Chimwaga utakuwa sehemu ya Chuo Kikuu kipya cha Dodoma ambacho kinatarajiwa kuanza mwezi Septemba mwaka huu 2007. *(Makofi)*

Na. 16

**Miundombinu mibovu ya Barabara Wilayani Kishapu**

**MHE. FRED M. TUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Kishapu ni moja kati ya Wilaya zilizo nyuma kimaendeleo kutokana na miundombinu mibovu mfano barabara zake muhimu za Vijijini, ikiwemo barabara ya kutoka Butuyu kupitia Wishiteleja, Kabila, Idukilo, Ngundangali hadi Mhunze na kwa kuwa, barabara ya kutoka Butuyu hadi Mhunze yenye urefu wa km. 52 inaunganisha Wilaya ya Shinyanga na Wilaya ya Kishapu yenye watu karibu 240,000 na kwamba kama barabara hiyo ikijengwa wananchi wapatao 240,000 watakuwa wamefaidika kwani itakuwa kiungo muhimu cha kiuchumi na kijamii kwa kuwaondolea kero.

Kwa kuwa, kama barabara hiyo haikujengwa wananchi wa Kata za Bunambiyu, Bubiki na Seke/Bugoro watalazimika kusafiri kwanza kwenda Makao Makuu ya Mkoa wa Shinyanga ndipo waweze kupata huduma katika Makao Makuu ya Wilaya yao mpya umbali wa km.52 kinyume na lengo zuri na uamuzi wa busara wa Serikali kuwapatia Wilaya hiyo kwa lengo la kusogeza huduma karibu nao:-

Kwa kuwa, Serikali iliandaa mapendekezo ya gharama za mradi wa kujenga barabara hiyo mwaka 2004. Je, Serikali itaanza lini ujenzi wa barabara hiyo ili kuwaondolea wananchi wa maeneo hayo usumbufu mkubwa wanaoupata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpendazoe, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoeleza Mheshimiwa Mbunge imegawanyika katika sehemu mbili kuu. Barabara kutoka Binambiyu –Butuyu hadi Bubiki km12 na barabara kutoka Washiteleja – Ngundangali km 40. Jumla ya kilomita zote ni km 52. Barabara hiyo ni muhimu kiuchumi na kijamii kwa wakazi wa Wilaya ya Kishapu na Shinyanga na ipo kwenye Mpango wa Miradi ya barabara za Vijijini iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka 2006/2007. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu imeshandaa andiko na kuwasilisha katika Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga.

Kwa taarifa tuliyoipata kutoka kwa Katibu Tawala wa Mkoa imeeleza kwamba Halmashauri inaomba kuzifanyia matengenezo barabara hizo kama ifuatavyo:-

| Na | Barabara | Gharama za Matengenezo | Urefu (km) |
|---|---|---|---|
| 1. | Bunambiyu-Butuyu–Bubiki km12 - | 178,145,100.00 | 12 |
| 2. | Washiteleja-Ngundangali km 40 - | 664,167,000.00 | 40 |
| | **Jumla** | **842,312,100.00** | |

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kiasi cha fedha kinachoweza kupatikana kutokana na Mpango wa kuboresha barabara za vijijini ni shilingi milioni 339. Hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu inashauriwa kukaa na kuangalia eneo la kipaumbele katika barabara hiyo ili fedha zilizopo ziweze kutolewa. Aidha, fedha zitaendelea kutolewa kadri Serikali itakavyopata pesa.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kwa kuwa mwaka huu Wilaya ya Kishapu imepata mvua nyingi sana ambazo zimesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu hasa barabara za vijijini na kwa kuwa sasa Wilaya ya Kishapu inakabiliwa na tatizo kubwa zaidi kuliko awali la ubovu wa barabara utakaoathiri mipango ya maendeleo itakayopangwa na itakayotekelezwa.

Je, Serikali itakubaliana na ushauri wangu na pia ombi langu kwamba katika mwaka wa fedha ujao yaani mwaka 2007/2008 Serikali itatoa kipaumbele kwa ajili ya ukarabati wa barabara zilizoharibiwa na mafuriko Wilaya ya Kishapu na maeneo mengine nchini?

La pili, kwa kuwa moja ya kichocheo kikubwa cha maendeleo mahali popote duniani ni ubora na uimara wa miundombinu hasa barabara; na kwa kuwa, Chama cha Mapinduzi katika Ilani yake ya uchaguzi 2005 kwa kutambua umuhimu wa kuchochea maendeleo katika Wilaya ya Kishapu iliahidi kujenga barabara ya kutoka Mwigumbi mpaka Maswa kwa kiwango cha lami; na kwa kuwa kwa dhamira hiyo hiyo wakati wa sherehe za wafanyakazi za mwaka 2006.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kwanza swali lako la nyongeza ni refu mno na nina mashaka inaelekea unasoma kinyume cha kanuni. Kwa hiyo, uliza huku ukiangalia ukumbi siyo uangalie meza. *(Kicheko)*

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, nauliza swali la pili la nyongeza kwa kifupi. Kwa kuwa kichocheo cha maendeleo mahali popote duniani ni uimara na ubora wa barabara; na kwa kuwa katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005 Chama cha Mapinduzi kiliahidi kujenga barabara kutoka Mwigumbi mpaka Maswa kwa kiwango cha lami na kwa dhamira hiyo hiyo mwaka 2006 Rais wa Jamhuri ya Muungano aliahidi kujengwa kwa barabara kutoka Kulwandoto mpaka Maswa kwa kiwango cha lami kupitia Bunzo Makao Makuu ya Wilaya ya Kishapu. Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Swali la pili ni swali jipya linaulizia barabara ya lami kutoka Kulwandoto kwenda Maswa ambazo zilizopo hapa ni barabara tofauti. Ningeomba Mheshimiwa Naibu Waziri ujibu swali la nyongeza la kwanza.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba barabara nyingi nchini zimeharibika msimu huu wa mvua na wote tunatambua hilo na mvua bado zinaendelea kunyesha. Serikali baada ya msimu wa mvua itaangalia na itafanya upembuzi yakinifu kwa barabara zote zilizoharibika wakati wa msimu wa mvua na kuangalia upya vipaumbele vya barabara mbalimbali.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge awe na subira kwa sababu mvua bado zinaendelea kunyesha. Kwa sasa hatuwezi tukampa jibu kamili kwamba *priority* itakuwa kwa Kishapu peke yake na siyo Wilaya nyinginezo. *(Makofi)*

Na. 17

**Ukosefu wa Miundombinu ya Uhakika Mbezi Luis, Goba-Madale**

**MHE. CHARLES N. KEENJA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wengi Jijini Dar es Salaam hivi sasa wanahamia maeneo ya Mbezi Luis, Goba hadi Madale na kwa kuwa maeneo hayo hayajapimwa na yana miundombinu mibovu sana:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba huu ni wakati muafaka wa kuandaa mpango kabambe wa kuendeleza maeneo hayo ili kuepusha hatari ya kuendelezwa kiholela kama ilivyo kwa silimia 80 ya Jiji?

(b) Kwa kuwa, maeneo hayo yanakabiliwa pia na tatizo la miundombinu mibovu. Je, Serikali ina mipango gani ya kuweka huduma za maji, umeme, barabara na kujenga madaraja kwenye barabara zinazovuka mito na vijito kwenye maeneo hayo hususan barabara za Goba – Makongo, Goba – Mbezi Luis na Goba – Madale?

(c) Kwa kuwa, ni muhimu sana kulipanga eneo hilo hivi sasa bila kuchelewa zaidi. Je, Serikali inakubali kuzingatia mpango wa kuendeleza eneo hilo kwenye makisio ya mwaka wa fedha 2006/2007.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuandaa mpango wa kuendeleza maeneo hayo ili kuepusha hatari ya kuendelezwa kiholela kama ilivyo katika maeneo mengine ya Jiji. Kwa kutambua hilo michoro kwa ajili ya mipango miji imekwishatayarishwa kwa maeneo ya Mbezi Luis, Goba Mtambani, Goba II na Madale.

Mheshimiwa Spika, pamoja na michoro hii kuandaliwa kazi ya upimaji ili kuweza kuweka miundombinu imeshindikana kutekelezwa kutokana na ufinyu wa Bajeti na ukosefu wa fedha. Kwa sababu hiyo, upimaji wa maeneo hayo utafanyika Serikali itakapopata fedha za kulipa fidia kwa wananchi wanaokaa katika maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu, hasa ya barabara, Wizara yangu, kupitia Manispaa ya Kinondoni na Wizara ya Miundombinu, kupitia *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam zimekuwa zinashughulikia barabara za maeneo hayo ya Goba, Madale, Makongo hadi Mbezi Luis. Wizara ya Miundombinu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa Dar es Salaam inahudumia barabara za Goba – Mbezi Luis (kilometa 15.5) na Goba – Madale (Kilometa 11.3). Barabara ya Goba – Makongo inahudumiwa na Manispaa ya Kinondoni.

Barabara ya Goba – Mbezi Luis na Goba – Madale ziko katika kiwango cha changarawe na udongo, barabara hizi zina hali nzuri na zinapitika bila matatizo.

Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Wizara ya Miundombinu imepanga kufanya matengenezo ya kawaida na maalum kwenye barabara inayoanzia Samaki

Wabichi – Goba hadi Mbezi Luis kwa gharama ya shilingi 72.655 milioni. Barabara ya Goba – Madale nayo inafanyiwa matengenezo kwa gharama ya shilingi 66.03 milioni.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kuzingatia ongezeko kubwa la magari yanayotumia barabara ya Goba – Mbezi Luis na Goba – Madale, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 imetenga jumla ya shilingi milioni 168 ili kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hizo kwa kiwango cha lami itakayounganisha barabara kuu za Bagamoyo, Morogoro na Nyerere kupitia maeneo ya Madale, Goba, Mbezi Luis, Kifurumsingwa, Kinyerezi na Ukonga (Banana). Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hizo zinatarajiwa kuanza mwezi Machi 2007 baada ya uteuzi wa Mhandisi Mshauri kukamilishwa.

Kukamilishwa kwa ujenzi wa barabara hizo kwa kiwango cha lami kutaondoa kero ya miundombinu ya barabara kwa wananchi waishio maeneo ya Mbezi Luis, Goba na Madale.

(c) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa katika kipengele (a), mpango wa kupima na kupanga maeneo hayo upo lakini tatizo lililopo ni ufinyu wa bajeti na vipaumbele vilivyopo. Hivyo, kwa sasa haitawezekana kuweka mipango hiyo katika mwaka 2006/2007 au 2007/2008.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kutia moyo.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, wakati swali hili linaandaliwa mvua za vuli zilikuwa hazijanyesha. Baada ya mvua zile kunyesha sasa hivi zile barabara zimebadilika kuwa makorongo au mabwawa na hali hii inaelekea kuwa ni kubwa zaidi kwa nchi nzima na siyo kwa Jimbo la Ubungo peke yake. Je, Serikali sasa ina mpango gani mahsusi kushughulikia dharura hii ambayo inatokana na neema ya kupata mvua nzuri.

Mheshimiwa Spika, la pili, linahusu hii Mipango Miji iliyoandaliwa na kukosa fedha. Sasa Serikali inafikiria itapata lini fedha kutekeleza mipango hiyo iliyoandaliwa. Kwa sababu uharibifu huu ambao umefanyika ni mkubwa na mbaya sana na unaweza ukaathiri maisha ya wananchi kama tunavyoona kila wakati yanapotokea magonjwa ya milipuko?

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha sasa hivi karibu nchi nzima miundombinu yetu hasa ya barabara na madaraja zimeathirika sana. Sasa hivi Serikali imefanya tathmini kwa nchi nzima na tunajua matatizo yaliyopo kwa kila Mkoa na ili tuweze kurudisha hali hiyo ya kidharura tunahitaji kama shilingi bilioni 10 kwa nchi nzima. Ni lazima tatizo hili tulielewe kwamba ni tatizo kubwa kweli kweli. Ni neema kwa upande fulani kwa sababu

tatizo la umeme sasa hivi siyo kali kama lilivyokuwa huko nyuma. Lakini katika neema hiyo limeibuka balaa nyingine.

Mheshimiwa Spika, lakini yote ni kheri tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha maeneo mengi katika nchi yetu yanapitika kidharura. Lakini kazi kubwa itabidi tuifanye pindi mvua zitakapotulia. Sasa hivi hizi mvua ni za vuli tu hatujui mvua za masika zitakuwaje. Tunamwomba Mwenyezi Mungu atusaidie mvua hizi zisivuruge sana miundombinu iliyopo hivi sasa *otherwise* itakuwa ni tatizo kubwa kweli. Tunaliangalia hili kuweza kupitika barabara hizi ni bilioni 10, lakini kuzirejesha katika hali yake ya kawaida tutahitaji takriban bilioni 45 na ni kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Charles Keenja na Waheshimiwa Wabunge tunaomba mtuelewe kwamba tuko pamoja na nanyi kwa sababu bila ya barabara uchumi wetu utaathirika na wananachi wetu katika shughuli zao za kila siku na wenyewe wataathirika lakini tunawapa matumaini Serikali iko pamoja na nyie. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Mipango Miji. Ningependa kumhakikishia Mbunge kwamba Serikali ina mpango madhubuti wa kutazama upimaji hasa katika Mipango Miji ya Jiji la Dar es Salaam na Miji mingine ya nchi nzima.

Ningependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es salaam kwamba sasa umefika wakati tutumie mkakati ambao Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeuweka wa kukopa fedha za mzunguko tulizozikopa kutoka Hazina kupima viwanja katika maeneo yaliyobaki ya Mkoa wa Dar es Salaam. Fedha hizo zipo za mzunguko tunaomba tuwasiliane nao ili tupime maeneo yaliyobaki kwa haraka iwezekanavyo, lakini tutawakopesha waweze kuzirudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuongeza kuwa Serikali ina mpango unaotegemewa kutafutiwa fedha za haraka wa *Peri Urbarn Development* ambao tunategemea kutazama maeneo ya pembezoni ya Jiji la Dar es Salaam ili kuyapima ili kupunguza ujenzi holela.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda pia kuwakumbusha Manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam kwamba niliwaeleza na kuwaomba watoe fedha kidogo katika bajeti ya mwaka huu ili tuweze kupata msaada na mchango kutoka *Habitat* ambao walionyesha kutusaidia katika upimaji wa Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza ujenzi holela katika Jiji letu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Charles Keenja ni mmoja wa Madiwani katika Manispaa ya Kinondoni na mimi vilevile ninamwomba tushirikiane ili kuhakikisha tumeandaa mpango wa kuweza kupata fedha kutoka *Habitat* ya kupima maeneo yaliyobaki ya Goba, Mbezi Luis na mengine katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Na. 18

**Zoezi la Kukusanya Maoni ya Wananchi Juu ya Shirikisho la Afrika Mashariki**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (k.n.y. MHE. JOB Y. NDUGAI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki alipokuwa akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo tarehe 9/8/2006 aliahidi kwamba Wizara hiyo imeandaa zoezi la kukusanya maoni kuanzia tarehe 15/9/2006 Mkoa hadi Mkoa kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki:-

Je, ni nini gharama za zoezi hilo ni madhumuni yake ni nini hasa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndugai, Mbunge wa Kongwa, na kabla ya kufanya hivyo, ninaomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Shirikisho la Kisiasa ni hatua ya mwisho katika mchakato wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeainisha hatua nne za mtangamano ambazo ni umoja wa forodha, soko la pamoja, sarafu moja na hatua ya mwisho ni shirikisho la kisiasa. Suala la kuangalia uwezekano wa kuharakisha uanzishwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki lilijadiliwa na Wakuu wa Nchi za Afrika Mashariki katika kikao chao kilichofanyika Mjini Nairobi Kenya tarehe 27 - 29 Agosti, 2004. Wakuu hao walikubaliana kuunda Kamati Maalum kufanya utafiti wa kina kuhusu suala hili. Kamati hiyo inajulikana kama Kamati ya Wako. Kamati hiyo ilitoa mapendekezo na maangalizo katikati ya mwaka 2005. Baada ya kupitia Taarifa ya Kamati, Wakuu wa Nchi wanachama, waliagiza wananchi washirikishwe kutoa maoni na mapendekezo juu ya kuharakisha shirikisho.

Jumuiya mpya ya Afrika Mashariki inalenga maendeleo ya wananchi walio wengi. Kwa sababu hiyo ushiriki wa wananchi katika mtangamano wa Afrika Mashariki hususan kutoa maoni na mapendekezo kuhusu mwelekeo wa baadaye wa ushirikiano ni muhimu sana katika kujenga Shirikisho Endelevu.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kupata maoni ya wananchi ulizinduliwa rasmi na viongozi wa Jumuiya, sawia, katika Miji Mikuu ya nchi Wanachama (Nairobi, Kampala na Dar es Salaam) tarehe 13 Oktoba, 2006. Uzinduzi ulikwenda sambamba na uteuzi wa Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Mchakato mzima.

Zoezi la kukusanya Maoni kwa Wananchi ni la kuhusisha wananchi wote kwa ujumla Wilaya hadi Wilaya likihusisha viongozi mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wanataaluma, Wafanyabiashara, Wakulima, Wafanyakazi pamoja na makundi maalum katika jamii kama vile viongozi wa dini, wazee, wanawake, vijana na

wengineo. Lengo la zoezi ni kupata maoni ya wananchi walio wengi ili hatimaye maamuzi yatakayotolewa kuhusu shirikisho yawiane na maslahi ya wananchi kwa ujumla.

Zoezi la kukusanya maoni kwa wananchi limeanza rasmi tarehe 8/1/2007 katika Mkoa wa Dar es Salaam na litaendelea nchi nzima hadi mwezi Mei, 2007 litakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, kama ifuatavyo:-

Makadirio ya gharama za zoezi la Mchakato kwa Nchi nzima linatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi 2.6 bilioni kwa vile zoezi litahusisha Wilaya zote za Tanzania (Bara na Visiwani). Kama nilivyoeleza kwenye maelezo yangu ya awali, madhumuni ya zoezi hili ni kutoa fursa kwa wananchi kutoa maoni yao kuhusu mustakabali wa mtangamano wa Afrika Mashariki, kama mkataba unavyofafanua.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri, lakini ningependa niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa matokeo ya zoezi hili linaloendelea ni agizo kutoka kwenye Jumuiya na kwa kuwa sasa majibu yale yatakuwa yanasaidia uwepo na maisha ya Jumuiya yenyewe kutoka kwenye nchi husika. Pengine maoni yale yanaweza yakawa yanatofautiana kutoka nchi moja hadi nchi nyingine.

Swali langu la kwanza ni kwamba. Je, kama maoni hayo yatatofautiana Shirikisho hili litakuwa katika hali gani?

Lakini swali la pili, ni kwamba kwa gharama hizi kubwa ambazo sasa nchi inaingia je, haikuwa busara Shirikisho lenyewe likaingia gharama hizo badala ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**: Mheshimiwa Spika, Mkataba unaoanzisha Jumuiya ya Afrika Mashiriki umeeleza bayana kwamba hakuna uamuzi wowote utakaofanywa na kikao chochote cha Jumuiya kama nchi wanachama wote hawakuridhia.

Kwa maana hiyo nchi mojawapo mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki akisema hapana au akisema tusiende kama inavyoulizwa, twende kama ilivyo kwenye Mkataba kwamba twende hatua kwa hatua baada ya kwenda haraka basi hapana shaka itabidi kuheshimu uamuzi wa nchi hiyo hata ikiwa moja. Kwa sababu Mkataba unasema maamuzi yote yatafanyika *by conscious* na vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni kwamba hizi gharama kubebwa na shirikisho.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwanza Shirikisho lenyewe halipo. Kilichopo hivi sasa ni Jumuiya na katika ushirikiano huo ukiangalia kifungu cha tano cha Mkataba wa Jumuiya sehemu ya pili, ndicho kinachoeleza ushirikiano huu utaenda hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza, ikiwa ushuru wa forodha wa pamoja ambao tayari umeanza tarehe 1 Januari, 2005.

Hatua ya pili ya soko la pamoja ambalo sasa ndio tupo katika mipango ya kuanza majadiliano jinsi ya kuanzisha Itifaki. Hatua ya tatu ya sarafu moja na hatua ya mwisho ndiyo ya Shirikisho la kisiasa ambalo tunakusanya maoni kuangalia kama tunaweza kwenda haraka ama kwenda hatua kwa hatua kama mkataba unavyosema. Kwa sababu hilo Shirikisho halipo na huwezi ukasema Shirikisho libebe gharama hizo ni wajibu wa kila nchi mwanachama kutoa fedha za kukusanya maoni kwa nia ya kushirikisha wananchi na kuweza kupata maoni ya walio wengi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwanza, kabla sijamwita Mbunge yeyote kuhusu swali la nyongeza nilikuwa napenda nielewe tu Naibu Waziri anaposema M-kataba nadhani una maana ya Mkataba. Kama ni hivyo basi swali la nyongeza liulizwe. (*Makofi/Kicheko)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa Serikali ya Tanzania imekubali au inaazimia kutumia fedha nyingi kiasi hicho kwa kutafuta maoni ya wananchi. Je, Serikali itakuwa tayari kuheshimu maoni ya wananchi wakati watakapokataa juu ya Shirikisho kwa wakati huu?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo viongozi wetu wakuu wameeleza na kama ambavyo Serikali imeeleza katika vikao mbalimbali na katika mikutano mbalimbali ni kwamba maoni ya wananchi watakayotoa yataheshimiwa na yatapewa kipaumbele. Kwa sababu hiyo naomba niseme kwamba wale wote wanaotoa maoni yao kwamba twende haraka kwa hivi sasa wako sawa sawa na wale wanaosema kwamba twende taratibu na wao wako sawa sawa. Tutakachoangalia mwisho wa siku walio wengi watasema nini. (*Makofi)*

**MHE. MANJU S. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, maoni kwa sasa hivi yanakusanywa kutoka kwenye nchi tatu Tanzania, Kenya na Uganda. Lakini hivi karibuni tumewaruhusu Rwanda na Burundi kujiunga na Afrika Mashariki.

Je, tutakwenda tena kukusanya maoni kwa watu wa Rwanda na Burundi baadaye au maoni yatakayopatikana kwa hizi nchi tatu za Afrika Mashariki ndiyo yatakayotumika kuwaamulia watu wa Rwanda na Burundi?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Rwanda na Burundi ziliomba kuwa wanachama wa Jumuiya

ya Afrika Mashariki na walipewa masharti ambayo yote wameyakubali na wamepewa miezi sita hivi sasa kuweza kukamilisha taratibu nyingine za kisheria ili waweze kuwa wanachama rasmi na unapokuwa unakaribishwa Mkataba uko wazi kwamba yale unayoyakuta yapo hakuna la kuchagua inatakiwa uyafuate mia kwa mia bila kupunguza chochote.

Kwa hiyo, watakapojiunga na sisi wakikuta tayari tumeshakuwa Shirikisho maana yake watakuwa wamekubaliana na hayo na hivi sasa wameshakubaliwa kimsingi lakini wanakamilisha taratibu nyingine za kisheria baada ya miezi sita wataleta *instruments* zao zitakuwa *deposited* na taratibu nyingine zitafuata.

Na. 19

**Watanzania Wameandaliwa Vipi Kuitumia Rasilimali yetu Kujiletea Maendeleo**

**MHE. ZAYNAB M. VULU** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi za Kenya na Uganda zimewaandaa wananchi wake katika kuzitumia rasilimali na mali za asili za Afrika ya Mashariki ili kujiletea maendeleo:-

(a) Je, Watanzania wameandaliwa kwa kiasi gani katika kutumia rasilimali hizo na maliasili zetu ili kujiletea maendeleo na hatimaye kujikwamua na umaskini uliokithiri miongoni mwa Watanzania walio wengi?

(b) Je, kama hawakuandaliwa vizuri, si watabakia kuwa vibarua na wakimbizi katika nchi yao?

(c) Kama wameandaliwa kama ambavyo nchi nyingine walivyofanya. Je, Wanawake wa Ki-Tanzania wameandaliwa kwa kiasi gani au kama hawajaandaliwa kuna mkakati gani wa kuwaandaa sasa kabla hatujachelewa zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuwandaa Watanzania kutumia rasilimali na maliasili za nchi, ni pamoja na kuwafahamisha fursa za masoko katika Jumuiya, kuwapa elimu ya biashara na ujasiliamali. Aidha, Serikali imekuwa makini katika kujenga mazingira bora ya uwekezaji, uzalishaji na biashara. Hatua nyingine ni pamoja na kubuni na kutekeleza mikakati ya kupunguza umaskini na kuongeza vyanzo vya mitaji kwa wananchi.

Mipango husika ni pamoja na MKUKUTA (Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania), Sera ya Uwezeshaji ya Mwaka 2004, Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji ya Mwaka 2004, Mpango wa Kurasimilisha Mali Tanzania (MKURABITA) na Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA).

(b) Serikali imezingatia umuhimu wa kufanya maandalizi ya kutosha katika ushiriki wake katika Jumuiya za Kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, mwelekeo wa ushirikiano wa sasa ni kujenga Jumuiya ambayo inazingatia usawa na haki. Kwa hiyo, hatutarajii Watanzania kuwa vibarua au wakimbizi katika nchi yao.

(c) Kwa kupiga vita umaskini Serikali inazingatia makundi maalum katika jamii wakiwemo vijana, wanawake na walemavu. Misingi hii inazingatiwa pia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na wanachama wake. Tayari wanawake wanapewa upendeleo wa makusudi katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa kama njia mojawapo ya kuwaandaa. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa mikataba hii ya uundwaji wa Shirikisho mingi imeandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Na kwa kuwa baadhi ya wananchi wengi wanaoishi vijijini na hata mijini lugha hiyo hawaifahamu vizuri. Je, Serikali imeweka mkakati gani wa kuiweka katika lugha nyepesi ili wananchi waweze kuielewa na kuepuka migongano itakayokuwepo?

Pili, kwa kuwa hadi sasa kuna migogoro mingi katika baadhi ya vijiji vyetu hapa nchini hiyo inatokana na kwamba kuna maeneo hawajapata sheria au kutokuielewa sheria ya ardhi vizuri.

Je, Serikali imeweka mkakati gani ili kuweza kupeleka maoni haya na kuyapokea vizuri na kuweza kuwaelimisha wananchi waweze kuzielewa ili kusiwe na migongano au wananchi kupokonywa ardhi yao? (*Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mikataba na itifaki mbalimbali hivi sasa iko kwenye lugha ya Kiingereza.

Lakini kweli vile vile hivi sasa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki tuko katika mpango wa kutafsiri mikataba pamoja na itifaki mbalimbali kuziweka katika lugha ya Kiswahili na ni matarajio yetu kwamba wakati muda si mrefu mikataba hii na hizi itifaki zitawekwa kwenye lugha ya Kiswahili na wananchi waweze kuelewa kwa ufasaha.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, linahusu migogoro mbalimbali inayojitokeza kwa sababu ya wananchi kutoelewa hizo sheria. Niseme Wizara inayohusika imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kutafsiri Sheria ya Ardhi na ni matarajio yangu kwamba kadri siku zinavyokwenda wananchi wengi zaidi wataweza kupata zile sheria zilizotafsiriwa kwa lugha nyepesi.

Lakini niseme migogoro hii saa nyingine haisababishwi na watu kutojua Sheria ya Ardhi. Wengine wanajua sheria lakini kwa sababu mbalimbali wanakiuka sheria hizo kwa makusudi.

Na. 20

**Utoaji wa Tuzo Kwa Wafanyakazi Wakubwa**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa wafanyabiashara mbalimbali hasa wenye mapato makubwa ndiyo walipaji wa kodi kubwa na ushuru na hivyo kuliingizia Taifa mapato makubwa kila mwaka:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na sera ya kuwalipa kiinua mgongo ama tuzo wafanyabiashara waaminifu na wa muda mrefu kama hatua ya kutambua mchango wao mkubwa kwa Taifa na pia kama motisha kwao ili wawe waaminifu zaidi?

(b) Je, ni nchi ngapi zenye utaratibu huo wa kuwalipa wafanyabiashara kiinua mgongo baada ya kulipa kodi zao kwa uadilifu?

(c) Je, Serikali itaanza lini kuiga utaratibu wa nchi hizo ili kuchochea uadilifu katika ulipaji kodi na kupunguza ukwepaji wa kulipa kodi kunakofanywa mara kwa mara na wafanyabiashara wasio waaminifu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango mkubwa wa wafanyabiashara kwa Taifa, hivyo kuanzia mwaka uliopita 2006 wakati wa kuadhimisha miaka 10 ya kuanzishwa kwa *TRA,* Serikali imeanzisha utaratibu wa kutoa tuzo kwa walipa kodi ambao wameonyesha uadilifu katika kulipa kodi. Jumla ya walipa kodi 224 kwa nchi nzima walipewa tuzo katika maadhimisho hayo yaliyofanyika tarehe 12 /10/2006 Kitaifa jijini Dar es Salaam. Aidha, Serikali imeanzisha utaratibu wa kuwa na siku maalum ya mlipakodi itakayofanyika kila mwaka. Hivyo basi, kwa sasa Serikali tayari imeshaona umuhimu wa kuwa na sera ya kuwatambua wafanyabiashara waaminifu na wa muda mrefu na kutoa vyeti/vikombe kama motisha kwao ili wawe waaminifu zaidi.

(b) Mheshimiwa Spika, kuna nchi nyingi duniani zenye utaratibu wa kutoa tuzo maalum kama ishara ya kutambua mchango wa walipa kodi wao

katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Nchi hizo ni pamoja na jirani zetu Kenya, Uganda, Rwanda na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo hatuna taarifa kama kuna nchi yoyote duniani ambayo ina sera ya kulipa kiinua mgongo kwa walipa kodi wake mbali na kufurahia huduma nzuri zinazotolewa na Serikali kwa wananchi wake kutokana na kodi zao kama vile, elimu bora, afya, barabara, ulinzi na usalama wa raia na kadhalika.

( c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoelezea kwenye jibu la sehemu (a), utaratibu wa kutoa tuzo kwa walipa kodi umekwishaanza na utaendelea kila mwaka wakati wa kuadhimisha Siku ya Mlipa kodi kama kichocheo cha uadilifu katika kulipa kodi na kupunguza ukwepaji wa kodi unaofanywa na wafanyabiashara wachache wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwa kushirikiana na *TRA* katika mikakati yake mbalimbali ya kupambana na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu ili kwa pamoja tujenge Taifa letu.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika utaratibu mzima wa mfumo wetu wa kutathmini hasa kwa bidhaa zinazotoka nje limekuwepo tatizo kubwa la wafanyabiashara kukwepa kodi hii ni kutokana na urasimu unaojitokeza katika *assessment*. Je, Wizara haioni kwamba ingekuwa ni vizuri ingejaribu kuangalia tena utaratibu huu mpya ili kuweza kurahisisha ili kuwafanya hawa watu wasiweze kukwepa kodi au kuwashawishi watendaji waweze ku-*commit* pamoja katika kukwepa kodi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB):** Mheshimiwa Spika, utaratibu upo walipa kodi tumewagawa sehemu tatu. Walipa kodi wakubwa kabisa, walipa kodi wa katikati na wa walipa kodi wadogo wadogo na wote katika vikundi hivyo tunawafuatilia kwa karibu sana na namna wanavyolipa kodi na namna tunavyotathmini na hata mizigo inapoingia pale bandarini utaona kwamba kuna yule ambaye ana *green card*, yule mwenye *yellow card* na yule mwenye *red card.* Mara nyingi ni mara chache sana mwenye *green card* huwa anapekuliwa vya kutosha.

Na. 21

**Nafasi ya Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania Zanzibar**

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE** aliuliza:-

Kwa kuwa, maamuzi ya Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* aliyepo Zanzibar hayana uzito kwa bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia Zanzibar

ambapo ushuru wa bidhaa hizo hukadiriwa upya mara zinapoteremshwa Tanzania Bara na kwa kuwa, kiutendaji *TRA* bado inaichukulia Zanzibar kuwa miongoni mwa nchi za Nje:-

(a) Je, kuna ulazima gani kwa *TRA* kuwa na Afisa Mwandamizi wa cheo cha Naibu Kamishna Tanzania, Zanzibar mwenye watumishi wengi chini yake, wakati kazi wanayoifanya ya kuzikagua na kuzifanyia tathmini bidhaa zinazoingizwa nchini kupitia Tanzania, Zanzibar haitambuliwi na Mamlaka husika Tanzania Bara?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, utaratibu wa kuichukulia Tanzania Zanzibar kuwa Nchi ya Kigeni, unakiuka Katiba ya Nchi na Hati ya Muungano?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Harisson George Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni muhimu kwa *TRA* kuwa na Afisa Mwandamizi wa Cheo cha Naibu Kamishna, Zanzibar kwa kuwa ndiye Msimamizi Mkuu wa utendaji wa kazi na anayo majukumu muhimu katika kusimamia ukusanyaji wa kodi zote za Muungano Zanzibar ambazo huchangia kwa wastani wa karibu asilimia arobaini (40) ya mapato ya kodi Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa bidhaa kutoka Zanzibar kuja Dar es Salaam unalenga katika kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinazoingizwa Tanzania Bara zinafuata utaratibu ulio sawa *(uniform treatment*) kwa ajili ya kuleta ushindani wa soko ulio huru na wa haki kwa bidhaa kutoka pande zote mbili. Wafanyabiashara wote wanaofanya biashara zao Bara wanalazimika kupitia taratibu za kiforodha zinazotumika Bara ambazo ni tofauti kidogo na zile zinazotumika Zanzibar katika mfumo wa kukagua bidhaa baada ya kuwasili nchini (*Destination Inspection).*

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa *Destination Inspection* Tanzania Bara unafanywa na wataalam ambao wana mtandao wao duniani kote kwa kuweza kujua bei ya bidhaa kutoka nchi inayosafirisha yaani *Exporting Country*. Bandari za Zanzibar ni vituo pekee vya forodha katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambavyo havitumii utaratibu huu.

Kwa kuwa bidhaa zote zinazoingizwa Tanzania Bara sharti zipitie katika utaratibu huo bidhaa kutoka Zanzibar hulazimika kuthaminiwa tena zinapoingizwa Tanzania Bara ili kukidhi taratibu zote za uthamini wa (*Destination Inspection).* Pale ambapo matokeo ya uthamini yataonyesha kuwa kodi husika zimelipwa Zanzibar mfanyabiashara hadaiwi chochote. *(Makofi)*

Mheshismiwa Spika, aidha ikiwa itabainishwa na na wataalamu kuwa kulikuwa na tofauti ya thamani iliyotumika kwa ajili ya kutoza kodi kule Zanzibar na ile ambayo

wataalamu wa uthamini wanayo kwenye mtandao wao basi ile ziada ya thamani tu ndiyo hulipwa. Vile vile pale ambapo Mamlaka ya Mapato upande wa Tanzania Bara haikupata ushahidi wa kutosha kwa kodi zililipwa Zanzibar wakati wa kuingiza bidhaa hizo basi kodi zote hukusanywa na Idara ya Forodha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, *TRA* Tanzania Bara inatambua uthamini unaofanywa na Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania aliyeko Zanzibar. Tofauti ni kwamba uthamini unaofanywa na Naibu Kamishna huyo hautumii utaratibu wa *Destination Inspection.*

(b) Mheshimiwa Spika, Zanzibar haichukuliwi kuwa ni nchi ya kigeni bali ni upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utaratibu unaofuatwa hauvunji Katiba ya Nchi isipokuwa lengo ni kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wanalipa kodi kwa mujibu wa Sheria.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mafupi tu ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano iko kwenye ibara yake ya 2. Imetamka wazi kuwa eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni eneo lote la Tanzania Bara na ni eneo lote la Zanzibar.

Kwa kuwa moja ya sifa kuu ya eneo lolote linalotambuliwa kuwa nchi moja ni biashara ya ndani isiyo na vikwazo na vile vile matumizi ya sarafu moja.

Je, kwa nini *TRA* Tanzania Bara idai malipo ya dola za Kimarekani 25,000 na si vinginevyo kwa mwezi kwa mtu yoyote anayetaka kutumia gari yenye usajili wa Zanzibar kwenye barabara za Bara na *TRA Zanzibar* haifanyi hivyo?

(c) Kwa kuwa fomu za kuruhusu matumizi ya magari ambayo yana usajili wa Zanzibar zinatamka wazi na ninazo hapa mkononi Mheshimiwa Spika, kwamba ni fomu kwa ajili ya *Foreign Vehicles* yaani magari ya nchi za nje na zinatamka wazi kwamba hiyo nchi ya nje yenye *Original Registration* ni Zanzibar na vile vile inatamka wazi kwamba hilo gari litatumika Tanganyika. Je, Serikali haioni kuwa dosari hizi ndogo ndogo kuendelea kuwepo kwake zaidi ya miaka 42 baada ya Muungano zinachochea hisia za utengano badala ya umoja?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAM I. KHATIB):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo nyuma katika maswali kama haya juu ya usajili wa magari ya Zanzibar na Tanzania Bara kwamba kuna sheria tofauti za usajili wa Tanzania Bara na Usajili wa Zanzibar. Tukaeleza vile vile tofauti iliyopo kwamba Zanzibar walikuwa hawatumii *Escuda II* ambayo sasa baada ya kurekebisha wanatumia *Escudor II* kwamba matatizo hayo yasiwepo tena.

Lakini watasema vile vile wanaoteremsha mizigo katika bandari ya Tanga au bandari ya Horohoro. Inapofika Kibaha wakati mwingine inaangaliwa upya na inapobidi anatozwa faini vile vile dola 25,000, kama vile gari lililotoka Zanzibar na mizigo mingine imetoka bandari ambayo siyo ya Dar es Salaam ambayo haaitumii *Escuda II* au haitumii *system* ile. Kwa hivyo ninachosema kwamba kama tulivyojibu katika majibu ya hapo nyuma kwamba tatizo hilo sasa linaondolewa kwa sababu Zanazibar wameshapelekewa *Escuda II* ili utaratibu wa kutathmini uwe mmoja.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nami ni shahidi na nina kumbukumbu kwamba niliwahi kujibiwa humu kwenye Bunge lako Tukufu kwamba hivi sasa matumizi ya *Escudar* yameshaanza kutumika kule Zanzibar.

Lakini kutokana na ushahidi wa swali la msingi lililoulizwa ionaonekana kwamba hizi fomu ambazo kwa kweli hazikidhi hii haja anayozungumza Mheshimiwa Naibu Waziri bado zinaendelea kufanya kazi na watu wanatozwa hiyo dola 25,000 kwa mwezi.

Sasa tunataka kusikia Serikali inatupa tamko mambo haya yatasimamishwa kuanzia lini. Kwa sababu sasa hivi ni miezi mitatu tokea tulivyoambiwa kwamba hii *Escudor* imeshaanza kufanya kazi Zanzibar ni lini itasimamishwa kodi hii?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM I. KHATIB)** Mheshimiwa Spika, kama ana kesi ya hivi karibuni ebu aniletee na ni ya mwezi gani ili tuweze kuliangalia suala hili. Kwa sababu yeye ni mmojawapo waliokuwemo katika kulitatua jambo hili pale Zanzibar. Wakati *TRA* walipokwenda Zanzibar kuzungumza juu ya utaratibu wa kuondoa tatizo hili sasa kama kuna kesi ya karibuni baada ya kuleta *Escudor II* naomba tafadhali aniletee ili tuangalie vipi tunaweza kulitatua.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwa jinsi alivyojenga hoja Mheshimiwa Mwakyembe na maoni yaliyotolewa ndani ya Bunge pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Fedha napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba tumelichukua jambo hili na kwamba jambo la msingi ni kero ndani ya Muungano na tutalishughulikia kikamilifu. *(Makofi)*

Na. 22

**Hitaji la Maji**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:_

Kwa kuwa, Ziwa Victoria liko karibu sana na Makao Makuu ya Wilaya ya Magu, na kwa kuwa katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005, Rais alitoa ahadi ya kuupatia maji safi na salama Mji wa Magu:-

Je, ni lini ahadi ya Rais itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa, Esther Kabadi Nyawazwa, Mbunge Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi kuhusu mradi wa maji wa Magu Mjini kama ifuatavyo:-

Mradi wa maji kwa ajili ya Mji wa Magu Mjini ulipimwa na kusanifiwa mwaka 1972/1973 na ujenzi kwanza mwaka 19974/1975. Ujenzi wa mradi huu ulikamilika mwaka 1984. Chanzo cha maji cha mradi huu ni Ziwa Victoria. Awali, mradi huu ulilenga kuhudumia watu 6,000 katika vijiji sita (6) vya Itumbili, Nyalikungu, Sagani, Kipeja, Ilungu na Nyashimba, ambapo vijiji vya Itumbili na Nyalikungu ndivyo vimekua na kuzaa Mji wa Magu. Kwa sasa, idadi ya watu waliopo ni 30,000. Aidha, mwaka 2005 kina cha maji katika Ziwa Victoria kilishuka kutokana na ukame hivyo kusababisha mtambo wa kusukuma maji kusimama kuanzia Oktoba mpaka Desemba, 2005. Mahitaji ya maji ya Mji wa Magu kwa sasa ni mita za ujazo 3,700 kwa siku ambapo kiasi cha maji kinachozalishwa ni mita za ujazo 1,400 kwa siku kutokana na ufinyu wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo mafupi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Kabadi Nyawaza kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua tatizo la maji la Mji wa Magu linalotokana na ongezeko kubwa la watu, ufinyu wa miundombinu na kushuka kwa kina cha maji katika Ziwa Victoria kutokana na ukame.

Ili kukabiliana na tatizo la maji katika Mji wa Magu, kwa mwaka 2006/2007, Wizara yangu imenunua na kufunga pampu mbili za kuelea majini (*floating submersibile pumps*) za kusukuma maji hadi kwenye mtambo wa kusukuma maji uliopo Busulwa kwa gharama ya jumla ya shilingi 108,606,931.20. Aidha, mwezi Januari 2006, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Magu, ilinunua na kufunga pampu ya majini (*submersible pump*) ya kusukuma maji pia kutoka Ziwani hadi mtambo wa kusukuma maji Busulwa kwa gharama ya shilingi 10,700,000; na pia mwezi Mei 2006 imenunua na kufunga pampu nyingine (*surface pump*) ya kusukuma maji kutoka kituo cha Busulwa hadi Magu Mjini kwa gharama ya shilingi 6,900,000.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tatizo la maji katika Mji wa Magu unahitajika ukarabati na upanuzi wa mradi wa kusambaza maji. Kazi zitakazohusika ni pamoja na ufungaji wa bomba kuu jipya, ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji, kufunga pampu nyingine za kusukuma maji na kufunga mabomba mengine zaidi ya kusambaza maji. Kazi hizi zinakadiriwa kugharimu jumla ya shilingi 2.5 bilioni. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji Mjini Magu kulingana na uwezo wake kifedha kila katika kipindi kipya cha Bajeti.

Napenda kumsihi Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kwamba mradi huu Serikali inaufahamu na inafahamu tatizo kubwa la maji na tuko mbioni katika kuhudumia mradi huu.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize suala dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri napenda nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kuliona tatizo hili la wakazi wa Mji wa Magu kwa kuwa walifanya utafiti wao mwaka 1984 kwa kukadiria wananchi 6,000 na sasa wako 30,000. Je, sasa Serikali inatumbia nini wakazi wa Mji wa Magu hizi bilioni 2.0 zitaanza kutengwa katika Bajeti ya mwaka huu 2007.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza ya kwamba Serikali tunafahamu tatizo hili tunajua kiasi cha maji huduma yake ni ndogo sana na tumeahidi ya kwamba tutakuwa kila mara tukiweka fedha na kwa hali hiyo napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalizingatia jambo hili ili tuanze kutenga fedha kidogo kidogo kuanzia Bajeti ijayo.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza kwenye swali lililoulizwa na Mheshimiwa Nyawazwa. Kwa kuwa Waziri amekubali na kukiri kwamba Magu kuna tatizo kubwa la maji na mradi uliopo ulikuwa kwa ajili ya watu 6,000 na sasa ni 30,000 mara tano zaidi na Waziri anaposema kwamba Serikali itatenga hela kidogo kidogo kila mwaka haiwezi Serikali ikatenga bilioni 2.5 ikamaliza tatizo la Magu mara moja kwa sababu hivi sasa ndoo moja inauzwa na hasa kipindi kunapokuwa na ukame mkubwa ndoo moja huuzwa shilingi 200/- na kwa familia ya kawaida ni ndoo kumi kwa siku kwa hiyo ni shilingi 2,000/- kwa siku. Familia maskini wanahangaika na akina mama wanahangaika usiku na mchana.

Naomba Serikali itenge bilioni 2.5 itatue tatizo la Magu kwa sababu wanaliwa na mamba Mheshimiwa Waziri. Naomba uiangalie maji kwa jicho la huruma.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tatizo la maji tunakumbuka Mheshimiwa Rais alipokuja kuhutubia Bunge kwa mara ya kwanza alitufahamisha kwamba ni kero kubwa na ni kero namba moja kwa wananchi ni kweli kwamba shida ya maji ipo nchi nzima na ni kila mhala na kuna baadhi ya sehemu nikitoa mfano katika Wilaya ya Babati kuna sehemu ambazo huduma ya maji ni asilimia sifuri yaani huduma ni sifuri. *(Makofi)*

Kwa hali hiyo kero hii ni kubwa sana na tunagawana sungura yule yule mdogo ambaye kila sehemu inabidi tutoe kidogo kidogo kwa kuendelea hivyo hivyo hatimaye tutamaliza kote. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutafanya kwa kadri ya jinsi sungura tutakavyomgawa aenee kila mahali ahsante.

Na. 23

**Kupungua kwa Kina cha Maji Ziwa Victoria**

**MHE. JUMA SAID OMAR** aliuliza:-

Kwa kuwa kina cha maji katika Ziwa Victoria kinaendelea kupungua siku hadi siku na kwa kuwa mradi wa maji wa Kahama Shinyanga unategemea maji kuoka Ziwa hilo:-

(a) Je, huko kupungua kwa maji katika Ziwa hilo kutaathiri vipi wa mradi wa maji wa Kahama – Shinyanga?

(b) Je, Serikali inawakikishia vipi wananchi wa Kahama/Shinyanga kwamba mradi wao wa maji utaendelea na kukamilika katika muda uliopangwa ili waweze kupata maji yaliyo safi, salama na ya uhakika?

(c) Je, mradi huo umefikia hatua gani mpaka hivi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omar Mbunge wa Mtambwe naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria hadi Miji ya Kahama na Shinyanga utakuwa na uwezo wa kutoa maji mita za ujazo 80,000 kwa siku kwa sasa na utatoshereza mahitaji ya watu 420,000 na baadaye utapanuliwa kukidhi mahitaji ya watu milioni moja katika miji ya Kahama na Shinyanga pamoja na vijiji 54 ambavyo viko kandokando ya bomba kuu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Said Omar, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Aina ya chanzo ni mfereji wa wazi uliopo katika Kijiji cha Ihelele Wilayani Misungwi, ujenzi wa chanzo hicho umezingatia kina cha chini kabisa cha Ziwa Victoria kilichofikiwa mwezi Oktoba mwaka 1952 cha mita 1132.79 kutoka usawa wa Bahari. Mfereji huu wa sasa uliochimbwa uko mika 1.65 ambao ni usawa wa chini zaidi ya kina kilichofikiwa mwaka 1952. Kwa hali hiyo kitaanzia sehemu ambayo ya kina cha mita 1131.14. Hivyo kushuka kwa kina cha maji kwenye Ziwa Victoria hakutaathiri utiririkaji wa maji kwenye mradi huu.

(b) Mradi wa Maji wa Kahama – Shinyanga umepewa kipaumbele na Serikali kwa kutoa rasilimali ya wataalam, vifaa na fedha za kutosha hadi sasa kwa mwaka 2006/2007 asilimia 82 ya fedha zilizokasimiwa zimetolewa na hivyo utakamilika kama ulivyopangwa mwishoni mwa mwaka 2007.

(c) Mradi wa Maji wa Kahama Shinyanga unatekelezwa kwa kandarasi tano na wastani wa utekelezaji hadi Januari 2007 ni asilimia 80 imekamilika. Mradi unatazamiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2007 kwa kuhudumia Miji ya Shinyanga, Kahama na vijiji 54 vilivyoko kando kando mwa Bomba Kuu. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya maji yaliyoko Shinyanga yanafanana kabisa na matatizo ya maji yaliyoko Singida na sisi ni Mikoa ya jirani. Je awamu inayokuja itafika Mkoa wa Singida ili matatizo ya maji kwa wananchi

wa Singida nayo yatatulike kama ambavyo Serikali inakusudia kutatua kwa Mkoa wa Shinyanga na Kahama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna Wilaya nyingi ambazo zimeomba pia wafikiriwe kama kutakuwa kuna awamu nyingine ili waweze kupewa huduma hiyo ya maji.

Kwa mfano kwa sasa kuna Wilaya ya Bukombe na wenyewe wameomba lakini hata hivyo litakalofanyika namsihi Mheshimiwa Mbunge kwamba na yeye pia watoe maombi yao na kama kutakuwa na awamu ya pili tutaangalia hayo maombi na stadi zitafanywa ili kuona gharama na kujua uwezo wetu wa fedha utafikia wapi kama na wenyewe wanaweza wakawemo na pia napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mradi huu wa Maji wa Victoria – Kahama – Shinyanga ni mradi ambao Serikali imetumia pesa yake ya hapa nchini na hatukupata hata senti tano kutoka nje. Kwa hiyo, mradi huu kama utaendelea awamu ya pili tutategemea na stadi na hali kadhalika na uwezo wetu wa fedha.

Na. 24

**Madaktari wa Tanzania Wanaofanya Kazi Nje ya Nchi**

**MHE MAIDA HAMAD ABDALLAH (k.n.y. MHE. KIDAWA HAMID SALEH)** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi ina upungufu mkubwa wa Madaktari; na kwa kuwa inasemekana Madaktari wengi wa Kitanzania wanafanya kazi nje ya nchi yao:-

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge idadi ya Madaktari walio nje ya nchi pamoja na nchi wanazofanyia kazi?

(b) Je, taifa linanufaika vipi kwa Madaktari hao kufanya kazi nje ya nchi yao?

(c) Je, ni sababu zipi hasa zilizosababisha Madaktari hao kuihama nchi yao ingawa Watanzania wanawahitaji sana?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Chama cha Madaktari wa Tanganyika *(Medical Association of Tanganyika)* mwaka 2006, unaonyesha kuwa kuna jumla ya watumishi wa afya 342 ambao wanafanya kazi nje ya nchi. Kati ya hao, 111 ni Madaktari. Utafiti huo unaonyesha kuwa asilimia kubwa ya watumishi hao wanafanya kazi katika nchi za Botswana, Lesotho, Namibia, Malawi, Afrika Kusini, Swaziland, Zambia na Zimbabwe.

(b) Kwa vile Madaktari hao huondoka bila kuaga, imekuwa vigumu kuwekeana mikataba na Serikali za nchi wanazokwenda kufanya kazi au na waajiri wao. Kutokana na sababu hiyo nchi yetu haipati manufaa yoyote ya moja kwa moja toka nchi walizokimbilia.

Ninaamini kuwa Waheshimiwa Wabunge mnafahamu ni kwa kiasi gani Serikali inakabiliwa na tatizo kubwa la watumishi wa afya hususani Madaktari. Hivyo, kuondoka kwa Madaktari nchini kunachangia kwa kiasi kikubwa kudidimiza utoaji wa huduma za afya nchini.

(c) Kwa kiasi kikubwa sababu iliyokuwa inasababisha Madaktari hawa kuihama nchi yao ni kutokana na maslahi duni hususan mishahara iliyokuwa ikitolewa hapo awali kwa watumishi wa Umma wakiwemo Madaktari.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kutokana na maboresho ya mishahara ya watumishi yalioanza kufanywa na Serikali kuanzia mwaka jana (2006), Wizara yangu imeshuhudia idadi kubwa ya Madaktari kutoka sekta binafsi kuingia katika utumishi wa Umma. Aidha, Daktari mmoja Mwandamizi amerejea nchini toka Zimbabwe ambako alikuwa anafanya kazi kwa zaidi ya miaka thelathini.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kuwa juhudi zinazoendelea kufanywa na Serikali katika kuboresha maslahi ya watumishi zitasaidia kuwashawishi watumishi wa afya wakiwemo Madaktari waliokuwa na nia ya kwenda kufanya kazi nje ya nchi kubaki hapa nchini na walio nje ya nchi kurejea nchini.

**MHE. ABDULKARIM E. HASSAN SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba Tanzania kuna mapungufu makubwa ya madaktari na Serikali katika Bunge lililopita pia alisema kwamba ina mpango wa kupata madaktari kutoka Nchi za Cuba na Misri na moja ya ahadi ambayo waliitoa hapa Bungeni walisema kwamba watakapofika kati ya Wilaya zilizopo Tanzania basi Mafia itapata Mabingwa hao wa Madaktari kutoka Cuba au Misri.

Je, Serikali mbona ipo kimya mpaka leo hatujapata taarifa zozote za Madaktari hao wanaotoka hizo sehemu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilisema itatafuta Madaktari kutoka Cuba na Misri na si Misri tu ili waweze kuja kusaidia kujaza mapengo ya uhaba wa madaktari tulionao.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba bado utaratibu unaendelea lakini si hivyo tu kwamba tunasubiria Cuba na Misri lakini wapo ambao wanaonyesha kuwa na *interest* kwa mfano Urusi tunafanya mazungumzo nao lakini Serikali sasa hivi kwa kutumia pesa ya *Global Fund* tayari tumeanza kuweka matangazo ambapo tumetangaza kuajiri wafanyakazi wa Idara ya Afya 365 na kati ya hao 30 ni Madaktari kutumia mpango wa *Emergency Hiring.*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge napenda kuwahakikishia kwamba tunaendelea na tukipata wataalam na wafanyakazi basi Mafia tutaiangalia na si Mafia peke yake ni Wilaya zote ambazo zina upungufu mkubwa wa Madaktari.

Na. 25

**Maambukizi ya Ukimwi**

**MHE. RAJAB HAMAD JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa athari za maambukizi ya UKIMWI nchini kitaifa ni asilimia saba (7%); na kwa kuwa ziko Wilaya zilizofikia asilimia kumi na saba (17%) ya maambukizi ya ungonjwa huo jambo ambalo linatisha sana:

(a) Je, kuna Wilaya zenye maambukizo chini ya asilimia mbili (2%), na kama zipo ni Wilaya ngapi?

(b) Je, Serikali inayo mikakati maalaum *(specific strategies)* ya kutekelezwa katika Wilaya zenye kiwango cha juu cha maambukizo ya ugonjwa huo ili kiwango hicho kishuke?

**SPIKA:** Kabla Mheshimiwa Naibu Waziri hujaenda kujibu naomba nitangaze malalamiko kuhusu baridi ndani ya ukumbi yanashughulikiwa nimekwisha waomba wahandisi washughulikie. Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mbunge wa Tumbatu, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Hapa Tanzania Bara umefanyika uchunguzi mmoja tu wa kina wa kitaifa kuhusu hali ya maambukizi ya virusi vya UKIWMI. Uchunguzi huo unaojulikana *Tanzania HIV Indicator Survey (THIS)* ulifanyika katika kipindi cha miaka ya 2003 na 2004 na matokeo kutolewa mwaka 2005.

Kwa mujibu wa muundo (*design*) wa uchunguzi huo, inawezekana tu kufanya makadirio ya viwango vya maambukizi kimkoa. Hivyo basi kutokana na takwimu za uchunguzi huo, wastani wa maambukizi kitaifa ulikuwa asilimia saba. Maambukizi miongoni mwa wanaume yalikuwa asilimia 6.3 na miongoni mwa wanawake yalikuwa asilimia 7.7. Kwa jumla sehemu za mijini zilikuwa na wastani wa maambukizi ya asilimia 10.9 wakati sehemu za vijijini zilikuwa na wastani wa maambukizi ya asilimia 5.3. Mikoa iliyokuwa na viwango vya chini kabisa ambavyo vilikuwa asilimia 2.0 ilikuwa Kigoma na Manyara, wakati Mikoa iliyoongoza kwa maambukizi ya juu zaidi ni Mbeya asilimia 13.5, Iringa asilimia 12.4 ikifuatiwa na Dar es Salaam ambayo ilikuwa na maambukizi kiasi cha asil mia 10.9.

Kutokana na matokeo ya uchunguzi huo *(THIS – Community Based)* Mikoa kumi na mitatu ilionekana kuwa na viwango vya maambukizi chini ya wastani wa kitaifa, yaani chini ya asilimia saba Mikoa mingine yote iliyobaki ilikuwa na viwango asilimia 7.2 hadi kufikia asilimia 13.5. Takwimu zinazotokana na upimaji wa maambukizi ya virusi vya UKIMWI miongoni mwa watu waliotoa damu ya kuongezea wagonjwa hospitalini kiwilaya kwa mwaka 2004 Wilaya zilizokuwa na viwango vya chini ilikuwa kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1. Arumeru na Ulanga | 1.5%; |
| 2. Rombo | 2.1%; |
| 3. Karatu | 2.3%; |
| 4. Tandahimba | 2.5%; |
| 5. Kibondo na Handeni | 2.6%; |
| 6. Kasulu | 2.8%; na |
| 7. Mtwara Mjini | 2.9%. |

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kulingana na takwimu zilizopo Wilaya zenye viwango vya Maambukizi ya UKIMWI chini ya asili mia mbili ni mbili. Wilaya hizo ni Arumeru na Ulanga.

(b) Serikali inatoa mkakati elekezi *(Strategic Plan*) ambao unaanisha afua (*interventions*) za kutekeleza kitaifa ambazo zinalenga udhibiti wa maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na mafunzo kwa wale ambao tayari wameambukizwa yaani *care and treatment*.

Afua zote hizo zimeelekezwa zitumike nchi nzima lakini Wilaya zima uhuru wa kusisitiza afua ambazo zinalingana na viwango na uzito wa mlipuko wa ugonjwa wa UKIMWI katika Wilaya au Mikoa husika. Afua zinazochaguliwa na Wilaya zinaanzishwa katika mpango wa Wilaya wa kudhibiti UKIMWI. Kutokana na hali hiyo, Mikoa na Wilaya zina fursa ya kuweka msisitizo katika eneo moja au jingine kulingana na hali halisi ya ugonjwa wa UKIMWI katika eneo husika.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nilikuwa na swali dogo. Kwa kuwa moja ya *intervention* zinazotumika katika kuzuia maambukizi mapya ni pamoja na kuhimiza matumizi ya Kondom na kwa kuwa matangazo yanahimiza matumizi ya mipira hiyo sehemu kubwa kumekuwa na *distortions* kwa maana kwamba inahamasisha zaidi kuliko kuzuia kutokana na vichocheo vinavyowekwa katika matangazo yale. Kwa mfano kondom imeongezewa radha ya *chocolate* na kadhalika.

Je, Serikali haioni kwamba matumizi na matangazo kama hayo yanachochea hasa vijana ambao wanaweza kujenga hisia za ku-*test* badala ya kuona kwamba ni njia

mbadala ya kuokoa maisha yao na katika udhibiti huo na kwanini Serikali isiwahimize watangazaji wa biashara hizo kwamba walau waweke angalizo kwa mfano:-

Matumizi Mabaya ya Kondom yanaweza kusababisha Maambukizi katika utangazaji ili watu waelewe kwamba matumizi ya kondom ni *alternative* na si njia ya kujiburudisha kama ilivyo sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge kwa matumizi ya kondom yanawekwa vibwagizo ambavyo yeye anahisi kwamba yanaleta vishawishi kuweza kutumia vibaya kondom. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi Wizara ya Afya hatuamini kwamba kuwekwa kwa mfano radha ya *chocolate* katika ile Salama Tatu Bomba inafanya mtu aweze atumie vibaya.

Mheshimiwa Slpika, naomba niliarifu Mbunge lako Tukufu kwamba Salama Tatu Bomba ambayo ndiyo inaradha ya *chocolate banana* na *strawberry* ilipozinduliwa ilitolewa kwa makusudi kwamba zile za kondom za zamani wengine walikuwa wanalalamika kwamba zina harufu mbaya wakati wanapozitumia.

Sasa naomba tufahamu kwamba watu wanakuwa wabunifu ili kuweza kuwasaidia wananchi na wale watumiaji wa zile kondom kujikinga na hili janga la UKIMWI na jinsi gani tunaweza tukawashawishi wote tunaweza tukawafahamu kwamba *chocolate* na *strawberry* ina harufu nzuri na kunukia vizuri kwa maana hiyo kule kuweka ile harufu kwenye kondom inakufanya wewe badara ya kusikia harufu ile mbaya ambayo unaona inakukinai unapata harufu nzuri ya *chocolate* na kukushawishi wewe uweze kutumia ile salama ikiwa na harufu nzuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba nisisitize nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba kondom inatumika kwa wale ambao hawawezi kuacha na kwa wale ambao hawawezi kuwa waaminifu. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla kondom inasaidia kupunguza maambukizi ya UKIMWI pamoja na kuzuia maambukizi ya magonjwa yanayotokana na ngono.

**SPIKA:** Sina hakika kama jibu hili la Serikali lina saidia kuzuia au linahamasisha lakini tunaendelea. (*Kicheko*)

Na. 26

**Uvamizi wa Wafugaji – Lindi**

**MHE. RIZIKI SAID LULINDA** aliuliza:-

Kwa kuwa siku za karibuni kumekuwepo na wimbi la mifugo kuingia Mkoa wa Lindi kwa wingi bila utaratibu unaoeleweka na kwa kuwa wafugaji hao wameingilia vyanzo vya maji na mabonde ya kilimo.

(a) Je, Serikali haioni kuwa wafugaji hao ndio waliohamishwa kutoka katika Bonde la Hifadhi na sasa wanaendeleza uharibifu huo Mkoa wa Lindi?

(b) Kwa kuwa wananchi wa Lindi si wafugaji na hawataki kuingiliwa katika mipango yao ya kutafuta maisha bora kwa kuletewa wahalifu wa mazingira. Je, Serikali itachukua hatua za haraka za kunusuru uharibifu huo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Riziki Saidi Lulinda, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ufugaji ni shughuli mojawapo halali na muhimu katika uchumi wa taifa na huokoa fedha za kigeni ambazo vinginevyo zingetumika kuagiza nyama, mayai, maziwa na mali ghafi za viwandani. Ufugaji wetu hutegemea mfumo kwa kufuata maeneo yenye malisho na maji kwa sababu maeneo mengi hajaendelezwa. Kuwepo kwa magonjwa au upungufu wa maji na malisho ni baadhi ya sababu zinazowafanya wafugaji kuhama ili kunusuru mifugo yao.

Serikali sasa imeweka utaratibu utakaowezesha matumizi mazuri ya rasilimali zilizoko ili ziwe endelevu na kukidhi suala la hifadhi ya mazingira. Pia Serikali imeandaa sera ya mifugo ambayo pamoja na mambo na mambo mengine inaelekeza namna ya ya kufuga kwa kuzingatia uwezo wa ardhi na malisho.

Aidha, mkakati wa kuhifadhi mazingira na vyanzo vya maji ambao wafugaji wanaelekeza kuutekeleza umeshaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Wafugaji wanaotoka Wilaya ya Mbarali Mkoani Mbeya, kwenda Lindi, hawategemewi kufanya uharibifu wa mazingira kwa kuwa maeneo wanayohamia ni yale yaliyotengwa kwa ajili ya ufugaji, yanapimwa na kuwekewa mipango mizuri ya matumizi ya ardhi na miundombinu muhimu ya uzalishaji. Aidha, wafugaji wanaelimishwa na kuelekezwa namna ya kufuga ya kufuga kwa kuzingatia kanuni za ufugaji bora.

(b) Kwa kutambua umuhimu wa mifugo, mwaka wa 2002 Mkoa wa Lindi, uliandaa programu ya uingizaji mifugo Mkoani ijulikanayo kama *Lindi Stocking Programme* na kupitishwa mwaka wa 2003. Lengo la mpango huo ni kuhamasisha wenyeji wa Mkoa huo na wageni, kuwekeza katika ufugaji.

Nawapongeza sana viongozi na wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa kuona umuhimu wa mifugo katika uchumi wa Mkoa. Kutokana na programu hiyo wenyeji wamekuwa wakiwapokea wafugaji wageni kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa.

Inategemewa utaratibu wa kuhamishia mifugo Mkoa huo utasaidia kuongeza kasi ya utekelezaji wa programu hiyo.

Aidha, wananchi wa Lindi sasa wataboresha afya zao kwa kutumia mazao ya mifugo ambayo sasa yatapatikana kwa bei nafuu na kwa urahisi, wataongeza ajira, kuboresha na kupanua zaidi kilimo kwa kutumia maksai. Serikali za vijiji na Halmashauri za Wilaya zitanufaika na ushuru utokanao na biashara ya mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, sio sahihi kusema kwa ujumla wananchi wa Lindi hawataki ufugaji bali natoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge kuhamasisha ufugaji kwa kuwa utaimarisha uchumi na kuboresha maisha ya wananchi wa Mkoa huo na taifa kwa ujumla.

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Kwa kweli wananchi wa Lindi wanapenda ufugaji wa kisasa hawahitaji wa ukorofi. Kwa mfano mimi mwenyewe ni Mjumbe katika Kamati ya Mazingira na Maliasili, nimetembelea Mbarali, Ihefu, Ikoga na sehemu mbalimbali za wafugaji.

Lakini kilichotokea Lindi wafugaji kutofuata taratibu walitakiwa wapitie Kibiti angalau wakatibiwe na wahesabiwe wafugaji hawakufanya hivyo wamepitia Madibira, Tunduru na wameingia Matekwe kwa fujo sana.

Katika hali hii Serikali haikuangalia hizo taratibu. Ninachosema kuwa tunaomba Serikali iliangalie hili tatizo wasione Lindi kama ni sehemu ya kuhamishia tatizo la Mbarali na kulipeleka Lindi. Wafanye mazingira mazuri angalau ambayo yataleta maendeleo badala ya kutuletea umaskini katika Mkoa wa Lindi.

Lindi tuna uvuvi tunakula samaki, tunayo mifugo ya kutosha, watuletee kilimo cha kisasa na ufugaji wa kisasa.

**SPIKA:** Swali Mheshimiwa?

**MHE. RIZIKI SAID LULIDA:** Je, Serikali inampango gani wa kuliangalia hili tatizo badala ya kulihamisha kutoka Mbalali na kuleta tatizo hilo Lindi?

Pili, Miaka ya nyuma wezi wa mifugo walihamishiwa Mkoa wa Lindi lakini sasa hivi tena wamewapeleka wafugaji.

Je Serikali kwa hili inaliangalia vipi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali haikuhamisha tatizo la Mbarali kwenda Mkoa wa Lindi. Ilichofanya katika mkakati wa kuhifadhi mazingira na hasa chanzo cha maji kwenye Bonde la Ihefu ni kuangalia maeneo muafaka ya kuwapeleka wafugaji waliokuwa Wilaya ya Mbarali. Mkoa wa Lindi ni eneo ambalo lina uwezo wa kubeba mifugo ipatayo 945,000. Kwa kuzingatia hilo na hasa kwa kuzingatia kuwa tayari Mkoa wa Lindi ulishaona umuhimu

wa kuinua uchumi kupitia ufugaji kwa kuwa na programu ya *Lindi Stocking Programme,* Serikali ikaona ni busara kutumia fursa hiyo ambayo wananchi wa Lindi wao wenyewe walikwishaiona na kusema kweli ndiyo azma ya Serikali na Ilani ya Chama cha Mapinduzi pia kwenye Aya ya 32 inasisitiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la wizi wa mifugo siwezi kulieleza sana kwa sababu silifahamu vizuri. Lakini, kama kuna tatizo hilo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane ili tuweze kulitatua.

Mheshimiwa Spika, lakini, napenda kusema pia, mimi tangu tarehe 16 hadi 20 Januari, 2007 nilitembelea Mkoa wa Lindi na Mtwara kuangalia utekelezaji wa zoezi la kuhamisha wafugaji kutoka Mbarali kwenda Lindi. Mambo yanaenda vizuri, pamekuwepo na matatizo madogo ni ya kawaida. Lakini kusema ukweli Serikali imejitahidi sana kuhakikisha kuwa hali ya zoezi hili inaenda vizuri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Maswali ya Usalama wa Raia tutaanza nayo kesho asubuhi. Ninayo matanganzo.

Tangazo la kwanza, naomba kutambua kuwepo pale kwenye *Speaker's Gallery* Bi. Audrey Milieu, Mwakilishi wa Balaozi wa Ufaransa hapa nchini. Yeye ni mgeni wa Mheshimiwa Naibu Spika. *Madam, we welcome you to Parliament in Dodoma. It's always a pleasure to have representatives of friendly countries visiting Dodoma and seeing our Parliament. Thank you very much. (Makofi)*

Mheshimiwa Janeth Kahama, anao wageni wake ambao ni Bi. Anna Makeja na Dotto Mrisho, hii Dotto sijui ni mwanaume au mwanamke. Lakini wakisimama labda tutawaona, wale pale. Karibuni sana, karibuni sana! Pia kuna wageni wa kutoka Mkoa wa Tabora, aliyeleta hakusema jina, lakini wageni hao ni Mheshimiwa Diwani Regina Athuman kutoka Nzega, yule pale na Mheshimiwa Ramadhan Wakulichembe, yeye anafanya kazi kwenye Kiwanda cha Nyuzi pale Tabora. Karibuni sana na poleni sana na mvua kubwa huko nyumbani.

Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, anaye mgeni wake anaitwa Habib Chande Kigwalilo, ambaye ni mdogo wake na anasema pia ni msaidizi wake katika masuala ya kampeni, yule pale. Karibu sana.

Vikao vya Kamati, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira ameniomba nitangaze kwamba leo saa tano asubuhi katika Ukumbi Namba 428 Wajumbe wote wa Kamati ya Maliasili na Mazingira wanaombwa kukutana ili kujadili Azimio la Bunge lililowekwa mbele yetu. Ni kazi ambayo haitachukua muda mrefu sana.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa William Kusila, anawaomba Wajumbe wote wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wakutane leo Chumba Namba 219 mara baada ya kipindi hiki cha maswali.

Mheshinmiwa Anna Makinda, Mwenyekiti wa *Tanzania Women Parliamentary Group (TWPG),* anaomba leo Wabunge wanawake wote wakutane saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, nimeona orodha ya maswali, nikagundua kwamba swali la Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji ambalo lingetoa fursa ya kumtambua mwenzetu Mheshimiwa Gaudence Kayombo, halitafikiwa hadi wiki ijayo. Kwa hiyo, atakuwa anapita pita tu anatabasamu. Lakini kinyume na wengine atakuwa hakutambuliwa. Kwa hiyo, naomba kuchukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji asimame tumpongeze kwa sababu ni vema tufanye hivyo. Ahsante sana! *(Makofi)*

Nikiwa bado katika hali ya pongezi, nimeshindwa kujizuia kuwatambua baadhi ya Wabunge ambao kwa mwaka huu 2007 wameonekana kuchukua jitihada maalum kuboresha taswira zao. Naanza na Mheshimiwa Aloyce Kimaro ambaye ameamua kufuga ndevu. *(Kicheko/Makofi)*

Katika mlolongo huo, siwezi kumwacha Mheshimiwa Susan Lyimo, ambaye amechukua kwa kweli *style* mpya kabisa ya nywele na pia nimalizie na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, naye kidogo nilibabaika hata kumtambua, lakini, kumbe! Huo ndiyo mwisho wa matangazo. Sasa Katibu, kwa hatua inayofuata. *(Kicheko/Makofi).*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika! Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika!

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, natumia Kanuni Namba 55(3). Punde hivi ulitoa taarifa kwamba baadhi ya Wabunge wamekutangazia kwamba kuna baridi humu ndani.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani wagonjwa hao walioandika, wanaumwa! Hali ya hewa ndani iko sawa, nzuri kabisa na sioni kama mimi nimevaa hivi, sikuvaa tai na suti kamili sioni baridi, sasa kwa hivyo Mbunge gani huyo ataona baridi hali hii wakati ambao joto limo ndani!

Mheshimiwa Spika, watu wanaposali, Imam anapokwenda chini na yeye anaenda chini, anapoenda juu na yeye anaende juu. Kwa hiyo, lazima wakubaliane na wengi waliomo ndani hawaoni baridi.

**SPIKA:** Huu ni mvutano wetu wa kawaida tu ambao Wahandisi wanajaribu kuweka hali sawa. Kwa hiyo, sina hakika kama Mheshimiwa Haroub Said Masoud, anasikia joto, amepatwa na vitu gani ambavyo vimemwezesha kusikia joto na pia sielewi hao ambao wamekuwa wakiniandikia hapa zaidi wakiwa ni Wabunge wanawake, sijui kuna shida gani hadi wanasikia baridi. Wahandisi wamesikia, kwa hiyo, wataweka wastani na utatusaidia wote. Ahsante sana! *(Kicheko/Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Usajili wa Biashara wa Mwaka 2006
### *(The Business Activities Registration Bill, 2006)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na hotuba na kwa sababu sikuhudhuria Bunge lako la mwezi Oktoba kwa udhuru na kwa ruhusa yako, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais ambaye alinihamisha toka Wizara ya Miundombinu kuja Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na vile vile kunipa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, ili tuweze kufanya kazi pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba wewe na Wabunge wenzangu mnipokee katika nafasi hii mpya na labda nitumie fursa hii vile vile kusema kwamba baadae Rais alipofanya mabadiliko ya Makatibu Wakuu kwenye Wizara chache, aliteua pia Katibu Mkuju mpya na Naibu Katibu Mkuu mpya katika Wizara hiyo ambao nitawataja baadae. Ingawa nitawataja baadae, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Nazir Karamagi na Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, ambao walitangulia kwenye Wizara hiyo kama Waziri na Naibu Waziri *respectively* kwa kazi nzuri waliyofanya. Ni tumaini langu kwamba tutaendeleza yale waliyotuachia na kuanza yetu mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara *(Business Activities Registration Bill, 2006)* pamoja na marekebisho yake, sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kutoa pole sana kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na familia kwa kupatwa na msiba mkubwa wa Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, aliyekuwa Mbunge wa Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Shughuli za Bunge, aliyefariki kutokana na ajali ya ndege kama sote tulivyotambua jana. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Batilda Salha Burian, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Pia nampongeza Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, Mbunge wa Mtama, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Aidha, nampongeza pia Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mbunge wa Sengerema, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninampongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Wote hawa nawatakia kazi njema na kuwahakikishia kuwa Wizara yangu itatoa ushirikiano wote utakaohitajika katika kutekeleza majukumu yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwandishi Mkuu wa Sheria, Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara na wadau mbalimbali chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, kwa ushirikiano wao mkubwa katika maandalizi ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu, Serikali ya Awamu ya Nne imeazimia kutoa msukumo mkubwa katika kukabiliana na tatizo la ajira kwa lengo la kukuza Pato la Taifa na kuondoa umaskini. Serikali imekusudia kurasimisha sekta isiyo rasmi kama mbinu mahsusi ya kuwawezesha wananchi walio wengi kutambulika, kubuni, kujiajiri na kujiongezea mapato yao binafsi na pia mapato ya Serikali. Katika kufanikisha malengo hayo, Serikali inatekeleza programu na mipango inayolenga kuwawezesha wananchi kushiriki katika uchumi kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaleta kwenye Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara kama mbinu mojawapo ya kuboresha mazingira ya biashara kwa kufanya mabadiliko katika mfumo mzima wa shughuli za biashara nchini. Chimbuko la kutunga Sheria mpya ya Usajili wa Shughuli za Biashara linatokana na nia ya Serikali ya kuondoa kero zilizokuwa zinawakabili wafanyabiashara, zikiwemo gharama kubwa za kuanzisha biashara, muda mrefu wa kupata leseni za biashara, utitiri wa leseni kutoka mamlaka mbalimbali na urasimu kabla ya kuanza biashara. Ili kuondokana na tatizo hilo, Bunge kupitia Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2001/2002, lilipitisha hoja ya Serikali ya kuanzisha kituo kimoja cha utoaji wa leseni *(one stop centre)* ili kupunguza urasimu na kero alizopata mwekezaji au mfanyabiashara aliyehitaji kupata leseni ya biashara.

Vile vile katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2004/2005, Serikali ilitangaza kuachana na utoaji wa leseni za biashara kama chanzo cha mapato ya Serikali na kutekeleza uamuzi huo katika Sheria ya Fedha *(Finance Act)* ya mwaka 2004. Maamuzi ya Serikali yalijumuisha mabadiliko matatu makubwa, kama ifuatavyo:-

(i) Biashara zilizokuwa na mzunguko wa mauzo *(sales turnover)* usiozidi shilingi milioni 20 kwa mwaka na zote zilizokuwa zinaanzishwa kwa mara ya kwanza kupewa leseni za bure yaani bila kulipiwa.

(ii) Biashara zilizokuwa na mzunguko wa mauzo wa zaidi ya shilingi milioni 20 kwa mwaka zilitakiwa kulipa shilingi 20,000 tu kama ada ya leseni.

(iii) Kuondolewa kwa ulazima wa kulipia leseni zote zilizotolewa na zinazoendelea kutolewa hadi hapo biashara husika zitakapokufa au leseni hizo zitakapofutwa na sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, maamuzi yote hayo yameanishwa katika Muswada huu ili kurahisisha utekelezaji.Sambamba na mfumo mpya wa usajili wa shughuli za biashara, Serikali ingali ikiandaa sera ya Utoaji wa Leseni za Udhibiti *(Regulatory Licences)* kwa lengo la kuainisha na kurekebisha Sheria 63 zinazotumika kusimamia udhibiti wa biashara nchini. Lengo ni kuweka mfumo utakaofanikisha malengo ya udhibiti bila kuathiri utawala bora wa biashara kutokana na kujumuisha masuala ambayo siyo muhimu na yanayokera wawekezaji na wafanyabiashara husika.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kuanzisha utaratibu wa kusajili shughuli za biashara badala ya utaratibu wa sasa wa utoaji wa leseni za biashara isipokuwa leseni za udhibiti zitaendelea kutolewa na mamlaka husika kwa mujibu wa sheria zinazozisimamia. Sheria hii mpya itaboresha mazingira ya kuanzisha na kufanya biashara na kuwawezesha wafanyabiashara walioko katika sekta isiyo rasmi kurasimisha biashara zao.

Aidha, Sheria inalenga kuhakikisha kuwa inaanzishwa Masijala ya Biashara ya Taifa yenye wataalamu, zana na tekinolojia ya kisasa ili kuhakikisha kwamba taarifa zote zinazohusu biashara zinatunzwa vizuri na kuiwezesha Serikali kupata taarifa za uhakika kuhusiana na mwenendo wa biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, mambo muhimu yatakayozingatiwa katika sheria inayopendekezwa ni pamoja na:-

(i) Kuwa na Masjala ya Taifa ya Usajili wa Biashara na kutamkwa wazi kisheria kuwa *BRELA* ambayo ni Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni itakuwa pia msimamizi mkuu wa chombo hicho;

(ii) Kuboresha mfumo wa biashara nchini ili kuendana na mahitaji ya soko huria;

(iii) Kupunguza gharama za uandikishaji wa shughuli za biashara;

(iv) Kuondoa utaratibu wa kupata leseni kwanza kwa shughuli za biashara isiyohitaji udhibiti wowote na kuweka mfumo mbadala wa kusajili shughuli za biashara;

(v) Kwa sekta zinazohitaji leseni za udhibiti *(Regulatory Licenses),* leseni zitatolewa na mamlaka husika na taarifa za leseni hizo kuwasilishwa kwa msajili wa biashara ambaye ni *BRELA* na mamlaka hizo;na

(vi) Kufanikisha lengo la kuwa na kituo kimoja cha utoaji wa leseni *(One Stop Centre)*. Taarifa kuhusu leseni za udhibiti zitawasilishwa na mamlaka husika moja kwa moja kwa msajili wa biashara.

Aidha, lengo lingine la Muswada ni kuondoa kero na gharama za aina nyingi zikiwemo:-

(a) Gharama zinazotokana na ada za uandikishaji;

(b) Gharama na muda ambao mwombaji anatumia kutafuta leseni;

(c) Kupunguza idadi ya leseni ambazo mwombaji alikuwa anawajibika kupata;

(d) Kuondoa ulazima wa kukata leseni nje ya eneo ambalo biashara inafanyikia; na

(e) Kuondoa mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile Sheria itaongeza kasi ya utekelezaji wa lengo la Serikali la kurasimisha shughuli za biashara nchini na kurahisisha upatikanaji wa takwimu sahihi za biashara. Sheria hii itafuta Sheria ya Leseni za Biashara Namba 25 ya mwaka 1972.

Mheshimiwa Spika, Muswada uliopo mbele ya Bunge lako una sehemu kuu tisa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kwanza inatamka Jina la Sheria yenyewe na eneo itakapotumika. Aidha, sehemu hii inacho pia kipengele cha tafsiri ya maneno mbalimbali yatakayotumika katika Sheria hii.

Sehemu ya Pili inahusu Mgawanyo wa Majukumu. Inaelezea majukumu ya Waziri, kutamkwa kwa Msajili Mkuu na kuanzishwa kwa Masjala Kuu ya Shughuli za Biashara.

Sehemu ya Tatu inahusu kuanzishwa kwa Vituo vya Usajili wa Biashara. Sehemu hii inazungumzia uanzishwaji wa Vituo vya Usajili wa Biashara katika ngazi zote za Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya. Aidha, sehemu hii inaainisha majukumu ya Vituo hivyo, uteuzi wa Wasajili na uanzishaji wa Masjala maalum kwenye vituo hivyo.

Sehemu ya Nne inashughulikia Usajili wa Biashara. Sehemu hii inahusu masharti ya usajili wa biashara, maombi ya usajili, usajili wenyewe na muda wa hati ya usajili, upeo wa mamlaka ya hati za usajili na wajibu wa wafanyabiashara. Vile vile, sehemu hii inaondoa mamlaka ya Serikali za Mitaa kutoa leseni za biashara.

Sehemu ya Tano inaweka namna ya kusitisha, kubatilisha, kutengua usajili na kufuta hati za usajili. Sehemu hii inahusu utaratibu wa kufuta hati za usajili wa biashara kutokana na kukiukwa kwa masharti yanayopaswa kuzingatiwa na wafanyabiashara, haki ya kusikilizwa na taratibu za kukata rufaa kwa wale wanaofutiwa hati za usajili, pamoja na taratibu za rufaa.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita inahusu Wajibu wa Wafanyabiashara. Sehemu hii ina maeneo matatu ingawa katika Muswada uliopo mbele yako, eneo linalohusu Kamati za Rufaa (Kifungu namba 23) limewekwa kwa makosa katika sehemu hii kwenye yaliyomo. Hivyo marekebisho yamefanywa ili eneo hili lipelekwe sehemu ya Tano ya Muswada ambayo pamoja na mambo mengine, inahusu masuala ya rufaa. Maeneo yanayobakia yanahusu utoaji wa taarifa kwa Msajili pale biashara inapofilisika

au kubadili mahali ilipokuwa; aina ya biashara ikibadilika au kama cheti cha uandikishaji kikipotea au kuharibika na kulazimu kuomba kupatiwa kipya.

Sehemu ya Saba ni juu ya Uteuzi wa Wakaguzi. Sehemu hii ina maeneo mawili yanayohusu uteuzi na kazi za wakaguzi, pamoja na upeo wa mamlaka zao katika kuhakikisha utekelezaji wa Sheria hii.

Sehemu ya Nane inaelezea aina ya Makosa na Adhabu. Sehemu hii ina maeneo mawili. Mosi ni kubainisha makosa mbalimbali chini ya sheria hii na pili uchapishaji wa taarifa zinazohusu kusitishwa au kubatilishwa kwa hati.

Sehemu ya Tisa inahusu Uandaaji wa Kanuni na Taratibu mbalimbali. Sehemu hii inampa Waziri mwenye dhamana ya Biashara mamlaka ya kutunga kanuni zitakazosaidia utekelezaji wa sheria hii. Vile vile sehemu hii inahusu ufutwaji wa Sheria ya Leseni za Biashara Namba 25 ya mwaka 1972.

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho linahusu vipengele vya mpito kuhusiana na leseni zilizotolewa chini ya Sheria inayofutwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Muswada huu unalo jedwali moja ambalo linaonyesha jinsi Hati ya Kusajili Shughuli za Biashara chini ya Sheria hii itakavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni hatua muhimu sana katika kuboresha uchumi wa Tanzania kwa njia ya biashara. Umesubiriwa kwa shauku kubwa na wafanyabiashara wetu wa ndani na wa nje, wakubwa na wadogo, wakiwemo pia wawekezaji wa ndani na nje na watu wote wanaotutakia mema, maendeleo na ufanisi katika uchumi wetu.

Namalizia kwa kuwashukuru viongozi, wataalamu na watendaji walioandaa Muswada huu, hususan Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Mbunge na Waziri wa Nishati na Madini, ambaye alinitangulia katika Wizara hii na Mheshimiwa Dr. David Mathayo David, Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika aliyekuwa Naibu wake. Nawashukuru pia Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri wangu, Bwana Wilfred Nyachia aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ambaye sasa amehamishiwa Wizara ya Ushirikianao wa Afrika Mashariki, Dr. Stergomena Tax-Bamwenda, Katibu Mkuu mpya na Dr. Florens Turuka, Naibu Katibu Mkuu mpya. Wote hao wamenisaidia sana na ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Kabla sijamwita Msemaji ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara, nimepokea majina mawili tu ya wachangiaji. Kwa hiyo, natoa taarifa hiyo ili wale ambao bado wangependa kuchangia, waweze kuleta karatasi.

Sasa namwita Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, kwa ajili ya kuwasilisha maoni ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la mwaka 2004 niweze kutoa maoni kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu Muswada wa Sheria ya Utaratibu wa Usajili wa Biashara wa mwaka 2006 *(The Business Activities Registration Bill, 2006)* inayokusudia kufuta Sheria ya sasa ya Leseni za Biashara Namba 25 ya mwaka 1972 pamoja na kuweka masharti ya mpito kwa leseni zilizotolewa chini ya Sheria inayofutwa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa salaam za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwako wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika, familia, ndugu, wakazi na wapigakura wote wa Tunduru kwa kifo cha Mbunge mwenzetu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu aliyekuwa akishughulikia masuala ya Bunge, Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, kilichosababishwa na ajali ya ndege.

Mheshimiwa Spika, Marehemu atakumbukwa daima kwa uchapakazi na uadilifu wake, kwa moyo wake wa kujituma na kwa uongozi wake wa mfano. Sisi wote humu Bungeni ni mashahidi wa wasifu huo wa Marehemu. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kutoa maoni ya Kamati kuhusu Muswada ulio mbele yetu, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya wajumbe wote wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Mbunge, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Hii ni heshima kubwa kwa Taifa letu, Bunge letu Tukufu na Taasisi iliyomlea na kumjenga Kitaaluma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Bernard Membe, Mbunge wa Mtama, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Dr. Batlida Burian, Mbunge wa Viti Maalum kushika wadhifa wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Bunge, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwekezaji na Mheshimiwa William Ngeleja, Mbunge wa Sengerema kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuupitia Muswada huu kwa lengo la kuuboresha, Kamati iliwaalika wadau mbalimbali kwa majadiliano ya kina kuhusu Muswada wenyewe, majadiliano ambayo yalisaidia sana kuibua mawazo mapya, maoni na hoja nzuri za kujenga. Nakiri kuwa maoni ya Kamati kuhusu Muswada huu ni matokeo ya mchakato huo wa kubadilishana mawazo na wadau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao waliitikia mwaliko wa Kamati wa kuja kutoa maoni yao kwa lengo la kuboresha Muswada ulio mbele yetu sasa.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati, hii walioshughulikia Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 95(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2004 ni hawa wafuatao; Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Mohammed Amour Chomboh, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mohammed Habib Mnyaa, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mheshimiwa Mohammed Sinani, Mheshimiwa Abdallah Sumry na mimi mwenyewe Dr. Harrison Mwakyembe, Makamu Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilisaidiwa na makatibu wake wawili, Ndugu Abdallah Hancha na Ndugu Lina Kitosi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati nianze kwa kumshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba na Katibu Mkuu wa Wizara Dr. Stergomana Tax-Bamwenda, kwa ushirikiano wao mzuri na wa karibu na Kamati, pamoja na hatua waliyochukua ya kushirikisha wadau mbalimbali katika ngazi zote za awali za kuuboresha Muswada huu. Matokeo yake ni Muswada uliorutubishwa kwa mawazo ya wengi, hivyo ubora wake unajionyesha wenyewe bayana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Muswada huu ni kuboresha mazingira ya ufanyajibiashara nchini kwa maana ya kuwaondolea wafanyabiashara kero, usumbufu wa kutafuta au kupata leseni kabla ya kuanza biashara na adha ya gharama inayoambatana na zoezi hilo la kufukuzia leseni. Kama nilivyodokeza awali, Muswada huu unapendekeza kufutwa kwa Sheria ya Leseni za Biashara Namba 25 ya mwaka 1972 na badala yake unaweka utaratibu rahisi na usio na gharama wala vichocheo vya rushwa wa kusajili tu biashara na kuendelea nayo bila kikwazo kingine chochote.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unazika kabisa dhana ya leseni kuwa chanzo kimojawapo cha mapato ya Serikali. Kamati ingependa kutoa angalizo kuwa kwa biashara zinazohitaji udhibiti maalum kama vile biashara zinazogusa masuala ya afya, mipango miji, mazingira, usalama, taaluma kama uhasibu, udaktari, sheria na kadhalika, taratibu maalum za udhibiti wa biashara katika sekta hizo zitaendelea kufuatwa.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati imeridhika kuwa Muswada huu ukipitishwa utaleta mapinduzi makubwa katika ufanyaji biashara nchini na utasaidia sana kufanikisha Mpango wa Taifa wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara zisizo Rasmi (MKURABITA).

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati, pamoja na malengo mazuri ya Muswada huu, mafanikio yake hayataonekana ikiwa wadau hawataelimishwa vizuri kuhusu faida za utaratibu huu mpya kwa maslahi yao na ya Taifa zima. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara, Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa ngazi mbalimbali kuwaelimisha

wananchi waelewe vema utaratibu huu mpya, waupokee kwa ari ili waweze kufaidika nao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua umuhimu wa kuendelea kudhibiti baadhi ya biashara katika maeneo maalum niliyokwisha yataja kama vile afya na mipango miji, Kamati inapendekeza kuwa Wizara sasa ielekeze nguvu zake huko ili kuwaondolea wanaofanya biashara hizo maalum kero, gharama zisizo za lazima na mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza zoezi hili la usajili wa biashara, Wizara iweke maandalizi mazuri ili wananchi wasisumbuliwe mithili ya watu wanaoomba kazi na kuwafanya waanze kulikwepa zoezi ambalo ni la manufaa kwao na kwa nchi. Aidha, Hati ya Usajili wa Biashara iwe na namba yake maalum *(Serial number)* na Wizara ihakikishe kuwa zoezi hili haligeuzwi na Halmashauri kuwa la kujipatia kipato cha ziada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unahitaji atakayejisajili katika masuala haya ya Biashara awe na *TIN number*. Kwa mfanyabiashara ndogo ndogo ambaye hata *TIN number* haielewi na amekuwa nje ya mfumo rasmi kwa umri wake wote, inaweza kuwa kikwazo kikubwa tusipochukua hatua za makusudi za kuwaelimisha wananchi kwanza. Ikiwezekana Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na Wizara ya Fedha zikae pamoja kukubaliana utaratibu bora zaidi unaozingatia hisia halisi za wafanyabiashara wadogowadogo ambao kwa muda wote wamekuwa nje ya mfumo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kuushukuru uongozi wa Wizara kwa kukubali baadhi ya ushauri wa Kamati moja kwa moja wakati wa mchakato wa kuchambua na kujadili Muswada huu kwenye Kamati. Mfano, Kifungu cha 14, haja ya kuwepo muda maalum wa usajili kukamilika na Kifungu cha 27 (c), kuweka mipaka ya madaraka ya Wakaguzi ndani ya Kanuni

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru tena Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Basil Mramba, Naibu Waziri Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Katibu Mkuu wa Wizara, Dr. Stergomana Tax-Bamwenda, Naibu Katibu Mkuu, Dr. F. Turuka, pamoja na watendaji wote wa Wizara walioshiriki kuandaa na kuuboresha Muswada huu ikiwa ni pamoja na ushirikiano waliouonyesha kwa Kamati wakati wote wa kuujadili.

Mheshimiwa Spika, naomba vilevile nirudie kuwashukuru na kuwapongeza wadau waliofika mbele ya Kamati na kutoa maoni yao ambayo yametusaidia sana. Aidha, naomba kuwapongeza Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kwa michango yao mizuri na makini ambayo kwa kiwango kikubwa imesaidia sana kuboresha Muswada huu. Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Damian S.L. Foka, kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo na Makatibu wa Kamati Ndugu Abdallah Hancha na Ndugu Lina Kitosi kwa kuihudumia Kamati vizuri kwa wakati wote.Waheshimiwa Wabunge nawashukuru sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA - MSEMAJI WA UPINZANI WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa miongoni mwa wale wote waliovuka mwaka 2006 na kuingia mwaka 2007 wakiwa wazima na afya. *(Makofi)*

Aidha, natoa rambirambi zangu kwa ndugu na jamaa kwa kuondokewa na ndugu yao, Marehemu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti na wale wengine waliofariki pamoja nae. Naomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa ustahimilivu familia za marehemu na azilaze pema peponi roho za Marehemu. *Amin.*

Napenda pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Aidha, nawapongeza Waheshimwa wote waliopata Uwaziri na Unaibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba nitoe shukrani kwa kupata fursa hii kutoa maoni yetu kuhusu Muswada wa Sheria tajwa hapo juu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5) (c) na 70(2) Toleo la mwaka 2004.

Napenda kumpongeza Mheshimwa Basil Mramba, Waziri, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa kuandaa Muswada huu bila kumsahau msaidizi wangu Mheshimiwa Savelina Mwijage kwa ushirikiano wake katika maandalizi ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unakusudiwa kupendekeza kutungwa kwa Sheria mpya itakayoweka utaratibu wa uandikishaji wa biashara badala ya utoaji wa leseni za biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kifungu hiki kinatamka wazi kwamba *Chief Executive Officer* wa *BRELA* ndiye msimamizi Mkuu, sioni sababu ya kumuhusisha Waziri wa Tawala za Mikoa au Biashara kwenye usimamizi wa masjala ya kumbukumbu za biashara *(Main Registry)* Kifungu Na. 6 (2) badala yake kifungu hiki kitamke wazi kwamba shughuli hii iwe jukumu mojawapo la shughuli za Mtendaji Mkuu wa *BRELA,* ili kupunguza usumbufu na gharama za kuendesha biashara.

Mheshimiwa Spika, kama Sheria haitatamka wazi kwamba shughuli hii ni sehemu au idara ya *BRELA* gharama za uendeshaji zinaweza kuwa kubwa kuliko sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya Muswada huu, Kifungu cha 7(2) kinaeleza uanzishaji wa Ofisi za Usajili wa Biashara katika Halmashauri za Manispaa, Miji na Wilaya.

Ninashauri kifungu hiki kirekebishwe ili kitamke wazi kwamba shughuli zitakazofanywa na Idara za Biasahra za Halmashauri, Manispaa au Miji ndiyo hizo hizo zitaendelea na shughuli za usajili wa biashara na kifungu hiki kitamke wazi kwamba wanawajibika kwa Msajili Mkuu *(Chief Registrar)* na siyo kwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo zuri la kuondoa ukiritimba wa leseni za kufanyia biashara, lakini inatubidi tuangalie pande zote, Kambi ya Upinzani, inaweka angalizo kama ambavyo tulifanya wakati Serikali inafuta kodi zilizokuwa zikileta kero kwa wananchi. Serikali ilizifuta kodi hizo bila ya kuwa na utaratibu makini wa kuweza kuziba pengo ambalo lingesababishwa na ufutwaji huo na matokeo yake miradi mingi na shughuli za kiutendaji zikakwama kwa kukosa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo ni bora Serikali ikaweka wazi kwani makusanyo yaliyokuwa yanatokana na leseni yalikuwa ni makubwa, je, pengo hilo linazibwa vipi? Kwani katika Muswada haionyesha kama uandikishaji wa shughuli za biashara utakuwa na gharama zozote kama zipo ni bora ikawekwa bayana katika sheria kuondoa mwanya wa kero zilizokuwepo katika kipindi cha leseni.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 9(1) kinatamka kwamba uteuzi wa Wasajili wa Biashara utafanywa na Waziri wa Tawala za Mikoa, ili kuondoa muingiliano wa uwajibikaji, napendekeza Sheria itamke wazi kwamba Msimamizi ni Mkuu wa Usajili wa Biashara ambaye ni Mtendaji Mkuu awe na madaraka ya kuwateua Wasajili na Msimamizi Mkuu wa majukumu yao, hivyo, hii itaendana na kifungu cha 9(3) kinachohusu uwajibikaji wa wasajili hao.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 10 kinatoa madaraka kwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko kwa kushirikiana na Waziri wa Tawala za Mikoa kusimamia masjala na kuhakikisha yanaendeshwa kwa mujibu wa taratibu za kiteknolojia kwa kuzingatia ufanisi wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia pendekezo la mwanzo kwamba kusajili biashara iwe Idara ya *BRELA,* kwa ajili ya kupunguza gharama za uendeshaji, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itamke wazi katika kifungu hiki kwamba usimamizi unafanywa na Mtendaji Mkuu wa *BRELA* badala ya Mawaziri waliotajwa kwenye Kifungu hiki cha 10.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 14(2) kinatoa madaraka kwa Msajili Mkuu kumnyima mwombaji usajili wa biashara yake kibali cha kuandikishwa kwa kutozingatia masharti ya kifungu cha 13.

Mheshimiwa Spika, badala ya kumnyima mtu usajili wa biashara yake, napendekeza kuwepo na Kifungu cha Usajili wa muda mpaka mwombaji atakapotimiza masharti yote yaliyomo kwenye Kifungu cha 13 ndipo apewe kibali kamili.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 19(1)(b) kinaeleza kuhusu taratibu za kufuta biashara mtu akihukumiwa kwa kosa alilotenda kwa mujibu wa Sheria hii. Kama mtu alifutiwa usajili wa biashara kwa kosa na baadaye akajirekebisha itakuwaje?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kiongezwe Kifungu kitakachotamka wazi kwamba mtu akijirekebisha anaweza kurejeshewa usajili wa biashara yake baada ya kutimiza masharti ya usajili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 22(1) kinaruhusu mtu ambaye hakutendewa haki katika kufutiwa usajili wa biashara kukata rufaa kwa Waziri. Kambi ya Upinzani inapendekeza kifungu hiki kiwekwe wazi kuwa kama mtu hakuridhika na uamuzi wa Waziri aweze kwenda Mahakamani badala ya kwenda kwa *District Commissioner* kwa sababu ofisi hii haina watalaam isipokuwa kama sheria hii itatafakari kuwa watawaongezea watalaam wanaweza kwenda kuripoti kwa *District Commissioner.*

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 26(1) kinatoa mamlaka kwa Waziri wa Tawala za Mikoa, kuteua wakaguzi wa biashara. Kambi ya Upinzani inapendekeza uteuzi wa Wakaguzi ufanywe na Mtendaji Mkuu wa Halmashauri kwa niaba ya Msajili Mkuu *(Chief Registrar)* na siyo Waziri. Suala la ukaguzi wa afya katika maeneo ya biashara halikupewa umuhimu kwenye kifungu cha 26. Aidha, tunapendekeza ukaguzi wa afya uwepo kwenye kifungu hiki na ieleze wahusika katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, Kambi ya Upinzani haina pingamizi na uanzishwaji wa sheria hii, ila inamtaka Mheshimiwa Waziri kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya vipengele vilivyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Msemaji wa hoja hii ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko. Sasa kwa mujibu wa orodha yangu ya wachangiaji ninayo sasa majina matatu nitawatamka wote ili wajiendae wanaofuata. Tutaanza na Mheshimiwa Herbert Mntangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce Kimaro na hatimaye Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kuwa mchangiaji wa kwanza katika Muswada huu. Lakini naomba pia kuchukua nafasi hii kutoa rambirambi kwa wale wote waliopatwa na msiba hasa Marehemu Mheshimiwa Juma Akukweti. Vile vile na wengine walioumia na kufariki katika ile ajali ya ndege.

Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, waliopata wadhifa huo hivi karibuni, naamini kabisa wote waliochaguliwa ni wachapakazi wazuri na wataonyesha hivyo katika utendaji wao wa sasa.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba Muswada huu wa Uandikishaji wa Biashara ni Muswada, mzuri sana na unatekeleza mambo makubwa ambayo Tanzania

tulianza kuyafanya ambayo yalituletea sifa na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache katika nchi zinazoendelea ambazo zinafanya marekebisho makubwa katika mfumo wake wa biashara. Kwa maana hiyo, kutuelekeza vizuri katika kuwezesha kuhamasisha wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, mambo ambayo tuliyafanya na kuwezesha Tanzania kufikia hatua hiyo katika miaka iliyopita ya hivi karibuni, moja lilikuwa hili la kurekebisha sheria za biashara. Tulifuta ada za leseni za biashara kwa biashara ndogo ndogo. Vile vile tulijitahidi kuweka vizuri sheria yetu ya kodi ya mapato na tukarekebisha sheria hizo kwa kuweka viwango ambavyo viliwezesha vile vile wafanyabiashara wadogo wadogo kuweza kufanyakazi bila kubugudhiwa kulipa kodi ya mapato kwa mapato ambayo yalikuwa kwa kweli kwa kiasi kikubwa hayakuwa yanakidhi mahitaji yao wao binafsi.

Vile vile tulifanya marekebisho ya sheria ya biashara wakati ule na kuwezesha katika kodi hii ya mapato kwamba wafanyabiashara wasitakiwe kulipa kodi ya mapato kabla hawajaanza hata kufanya biashara yenyewe. Sasa tunaamini kabisa huo ni mvuto mmoja mkubwa unaotusaidia katika kuweka hali nzuri ya mfumo wa biashara hapa nchini. Lengo kuu la Muswada wetu ni kutekeleza azma kubwa ya mpango ambao tulijiwekea unaoitwa Mpango wa Taifa wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara (MKURABITA). Kwa kuwa na sheria hii kwa uhakika tunatekeleza hilo la kufanya MKURABITA kuwa kweli mpango unaorasimisha biashara hapa Tanzania kwa urahisi na kuweza kuwavutia wananchi wengi.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada wetu huu yapo mambo machache ambayo ni vema tukayaangalia. Katika Muswada huu katika sehemu ya 13 kifungu cha (q) ambapo kinasema miongoni mwa mambo ambayo mfanyabiashara ili aweze kuandikisha atatakiwa ayafanye ni awe na *TIN Number*. Wakati tukichangia katika Kamati tuliona ugumu wa utekelezaji wa jambo hili. Nilidhani kwamba katika *amendments* hizi ningeona kwamba kifungu hicho kimeondolewa, lakini naona bado kipo na kama bado kipo kama sehemu ya sheria nataka niwahakikishie kwamba kitaleta matatizo makubwa sana. Kwa sababu huyu mfanyabiashara anakuja kutaka kuandikisha biashara yake, biashara ndogo ambayo kwa kweli hastahili hata kulipa kodi ya mapato unamwambia awe na *TIN Number.* Haya ndiyo matatizo ambayo mara nyingi yamekuwa yakitokea katika Halmashauri zetu. Anapofika mfanyabiashara kwenda kutaka tu apate leseni ya biashara, ofisi zetu ndani ya Halmashauri zilikuwa zikimtaka aende kwanza *TRA* akalete *TIN Number*. Kwa hiyo, ulikuwa huwezi ukapata leseni ya biashara kwanza mpaka ukapate *TIN Number*.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi matokeo yake ni kwamba wafanyabiashara wengi walioambiwa waende wakatafute *TIN Number* hawakurudi tena maana yake wameendelea kufanya biashara bila kuwa na leseni za biashara. Sasa tusiweke vikwazo ambavyo bado vinaweza vikaleta matatizo. Limejitokeza hili na ndani ya taarifa aliyotoa Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu amelieleza vizuri. Nilitaka tu hapa nigusie tu kwamba sikuona hii *amendment* ya kukifuta kifungu kile cha (q).

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo lingine, sisi tunajitahidi kutunga sheria ambazo zina shabaha nzuri kwa watendaji wetu, kwa wananchi wetu na kwa wafanyabiashara wetu. Lakini kumekuwa na matatizo mengi ya watendaji, mara nyingi na mara kadhaa, watendaji huko vijijini wamekuwa kwa makusudi au kwa kutoelewa au kutokuwa na elimu wamekuwa wakipotosha sheria zetu. Tumeshasema tumefuta ada za leseni za biashara kwa biashara ambazo hazina mapato zaidi ya shilingi milioni 20 bado ukienda vijijini watendaji wanawalazimisha watu wawape fedha za ada za leseni za biashara. Ukifika Halmashauri ukimueleza Afisa Biashara, anasema hatuna maagizo hayo. Kwa hiyo, wako watendaji wachache kwa makusudi nasema hapa kwa lengo la kutafuta rushwa wanawalazimisha watu bado wawape fedha za ada za leseni za biashara jambo ambalo kwa hakika halipo kwa kiwango cha biashara zao wanazofanya kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, ni vema basi tukawaelimisha wananchi lakini tukawaelimisha watendaji wetu na tukawasimamia watendaji wetu ili wasipoteza mwelekeo huu wa sheria hizi tunazotunga kwa lengo la kurahisisha utendaji wa shughuli za biashara zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kufuta utaratibu huu wa ada za leseni za biashara tunaathiri kwa kiasi fulani mapato ya Halmashauri. Nini Halmashauri zilikuwa zikifanya? Katika kutafuta leseni za biashara Halmashauri nyingi zilikuwa zinatoza ushuru katika zile fomu za maombi za kupata leseni *whether* una-*qualify* kupata leseni au hu-*qualify* lakini lazima upate fomu ya maombi. Ile fomu peke yake Halmashauri ilikuwa inatoza ada shilingi 3,000 Halmashauri nyingine zaidi ya shilingi 3,000. Halmashauri yangu ya Wilaya ya Muheza ni shilingi 3,000. Kwa kiasi fulani tutakuwa tumezipunguzia Halmashauri zetu mapato kwa wale waliokuwa wakichaji shilingi 3,000 kwa jumla ya biashara zipatazo 3,000 katika Wilaya nzima ni mapato ya zaidi ya shilingi milioni 15 tumeziondoa ndani ya Halmashauri zetu. Tunasema nini kuhusu hili?

Mheshimiwa Spika, mpango wa awali Serikali iliamua kwamba itafidia Halmashauri zote kwa fedha ambazo walikuwa wanakusanya katika kodi tulizokuwa tumeona ni kero. Sasa na hapa lazima tuhakikishe tunatafuta njia ya kuzifidia Halmashauri zetu ili tusizipunguzie uwezo wa kiutendaji baada ya kuwaondolea pato hili ambalo walikuwa wakilipata kutokana na kuuza fomu hizi za maombi za leseni za biashara kwa viwango tofauti katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, sasa tulisema nini kifanyike, lakini nina imani kabisa hili tutaliona, Wizara ya Fedha itaangalia nini tutakachofanya. Hatutaki tena wananchi wetu waanze kubugudhiwa kwa kwenda kufanya *registration*. Naona katika Muswada mzima huku hakuna ada wala viwango vya ada kwa ajili ya kufanya *registration*. Tusije tukatengeneza kanuni tukasema wananchi walipe ada kwa ajili ya kupata fomu za kufanyia *registration*. Tuangalie uwezekano wa kuzifidia Halmashauri zetu kutokana na kipato hiki walichokuwa wanakipata sasa watakikosa.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa sheria hii wapo wataalam, wapo watendaji ambao wamepewa majukumu ya kufanya. Kwa mfano wapo ma-*inspectors*. Lakini vile vile katika ngazi fulani sasa za Wilaya, kuna rufaa pale ambapo mwananchi

haridhiki kwa yale ambayo aliyotendewa anakata rufaa na atasikilizwa na Mkuu wa Wilaya.

Pendekezo langu ni kwamba hawa watendaji wote pamoja na Wakuu wa Wilaya, viongozi wa Halmashauri, *Inspectors* ambao ni wakaguzi, Madiwani basi wapate elimu ya awali kuhusu Muswada wa Sheria hii namna ya kuusimamia, namna ya kuutekeleza. Kama Mkuu wa Wilaya ndiye atakayekuwa msikilizaji wa rufaa lakini haelewi sheria yenyewe inasema nini basi tutakuwa tunampa majukumu bila kumpa elimu ya namna ya kutekeleza na kusimamia majukumu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba basi kuwepo na utaratibu wa kuhakikisha hawa wanapata elimu hiyo ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nakusudia kusema hayo machache. Nataka kukiri kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, sehemu kubwa ya mchango wangu niliupitisha kule. Lakini niliona nisema haya machache ya ziada ili kutekeleza utekelezaji wa Muswada wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia mawazo yangu katika hii hoja ya *Business Regulatory Act*. Kabla sijaanza kutoa maoni yangu niungane na wenzangu kwa kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Juma Akukweti, kwa kumpoteza mmoja wa wachapakazi ambaye tulikuwa tunamtegemea sana hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hakika ndugu alikuwa ni mchapakazi sisi tulipopata na mafuriko mwaka jana Moshi Vijijini, alikuwa ni mtu wa kwanza kunipigia simu na alikuja mwenyewe tukashughulika na ushauri wake ulitufariji sana na tukaweza kupata misaada mingi ya kutosha. Vile vile kifo chake kimemfika alipokwenda Mbeya kuangalia na kutathimini athari zilizopatikana baada ya soko la Mwanjelwa kuungua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mwenzetu alifariki na nina hakika alikuwa mchapakazi, naomba Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Ndugu zangu pia niendelee kuwapongeza wale wenzetu waliopata nyadhifa mbalimbali, nikianzia na Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Hii ni sifa kwetu Watanzania, naomba wote tuungane, tumshukuru Mungu na tuendelee kujitahidi ili na wenzetu waendelee kuchaguliwa kuwakilisha Taifa hili nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza vile vile wale wenzetu walioteuliwa Mawaziri, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Dr. Matilda Burian na Naibu Mawaziri Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Gaudance Kayombo. Tutashirikiana wote kuhakikisha kwamba hili gurudumu la maendeleo ndani ya hii ari mpya, nguvu mpya na

kasi mpya tunafikisha hili Taifa nalo lijulikane kwamba ni Taifa lenye uwezo wa kupambana mpaka tuwe Taifa la kuweza kutambulika sasa kuwa ni Taifa lililoendelea.

Nawapongeza pia Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Naibu wake na watendaji wote kwa kuweza kuwakilisha huu Muswada ambao ndio tunaujadili sasa na ukweli umefika wakati muafaka wa kuweza kutambua wafanya biashara. Hii nchi yetu tunasema kwamba ni nchi ya wakulima, wafanyakazi na wafanyabiashara. Wafanyabiashara wamekuwa mara nyingi hawatambuliki. Tumekuwa tunasema kwamba ni nchi ya wakulima. Wakulima tunawatambua, wafanyakazi wanatambulika kabisa na idadi yao inajulikana. Wafanyabiashara na wakulima idadi yao si rahisi kuitambua. Sasa tumeanza na wafanyabiashara kuwatambua ili uweze kusaidiwa, kama nchi inataka kusaidia watu wake lazima iwatambuwe. Tunaanza sasa na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, huu Muswada ni Muswada mzuri kabisa, nawaomba Watanzania wenzangu wale ambao wanataka kufanya biashara, wakajisajili ili Serikali iwatambue na sisi Watanzania tutambue kwamba tuna wafanyabiashara kadhaa. Mfanya biashara mdogo ndio anayekuwa na kuwa mfanyabiashara mkubwa, anakuwa tajiri. Kwa hiyo, tunaomba kwa kuwatambua hawa wadogo na vile vile tuwatambue wale matajiri ili kama tunataka kuomba msaada tujue kwamba hawa watu ndio wanaweza kutusaidia. Tuwatambue vile vile wafanyabiashara wakubwa na tuwapange kwa aina ya biashara wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, mfano, wafanyabiashara wakubwa wa vyakula kama mazao, tukiwatambua wanaweza kutupa *data* ambazo zitatuwezesha kuelewa kwamba hii nchi tuna *reserve* kiasi gani ya mazao. Tunaweza tukashauriana nao tukawaambia sasa ili tuweze kusaidiana na wakulima hebu tusaidieni ninyi wafanyabiashara wakubwa kwamba mnunue matrekta, muya-*station* mahali fulani kama Kusini ili wakulima wale wadogo wadogo waweze kuja kukodisha matrekta kwao walime na wao wawe wanunuzi wa hayo mazao watakayolima. Kilimo cha namna hiyo kinaitwa *contract farming,* kwamba nakupa *facility* lakini nitakuja kununua kwako. Tukifuata utaratibu huu pia tutakuwa tumewatambua vile vile na wakulima. *(Makofi)*

Ndugu zangu hii Sheria ya kuwatambua wafanyabiashara ni vizuri tukahakikisha kwamba wale watendaji watakaofanya shughuli hiyo wanaifanya kikamilifu ili baada ya mwaka huu tuweze kujua kwamba tunao wafanyabiashara kadhaa na mfanyabiashara kujiandikisha lazima vile vile uwe na *TIN*. *TIN* maana yake hata ukipata kitambulisho cha Kitaifa lazima uwe na *TIN* tukutambue kwamba wewe unafanya kazi gani. Kutakuwa na kundi la wakulima, wafanyabiashara na wafanyakazi. Lile kundi ambalo litakuwa limebaki halijajiandikisha labda tutaliita ni kundi la wazururaji.

Mheshimiwa Spika, je, kuna mtu anataka kuitwa au kuwekwa katika kundi la wazururaji. Hayupo mtu wa namna hiyo, ili tuweze kutekeleza vizuri sera ya MKURABITA lazima tuhamasishe wafanyabiashara wajiandikishe. Zile *Registration Forms* nao walipie kidogo. Mfanyabiashara ajisikie kwamba na yeye ana uwezo aweze kulipa kidogo. Ndiyo maana unaitwa mfanyabiashara. Huwezi ukaitwa mfanyabiashara

halafu ukasema wewe ni maskini. Wewe ni mfanyabiashara unaweza ukabuni biashara. Sasa kama unaweza kubuni biashara na ulipe kidogo, unakwenda hospitali unalipa ada hospitali. Watanzania wote wanakwenda hospitali wanalipa kidogo.

Mheshimiwa Spika, wewe unaitwa mfanyabiashara hata ile ada ya kujisajili unasema hapana, nipewe bure na wakulima wapewe bure nini na wafanyakazi wapewe bure nini. Kwa hiyo, lazima tukubaliane kwamba ile ada ya *Registration* tukubaliane ilipwe na pia wafanyabiashara hao hao wawe na *TIN* ndiyo mwanzo wa kuwa mfanyabiashara mdogo, baadaye utakuwa mfanyabiashara mkubwa. Ukubali uanzie hapo ili uweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakubaliana na hii *Bill* kwamba waandikishwe lakini nasema walipe kidogo. Hawa wafanyabiashara wa kawaida tunasema leseni zao hawatalipa. Kuna hizi Leseni za Udhibiti *(Regulatory Licenses)* nitazungumzia eneo moja ambalo nalifahamu kwa kina. Eneo la leseni za utalii. Leseni za utalii kupata leseni ya utalii bei yake ni dola 2,000. Dola 2,000 kwa pesa za Kitanzania ni karibu na shilingi milioni mbili na nusu. Huyu Mtanzania ambaye anatoka kwenye ufanya biashara ndogo ndogo ambao ndio tunawa-*regester* sasa hivi. Sasa tunataka akuwe, aende kwenye biashara inayoeleweka kama hii ya utalii, unamwambia ili uweze kuingia kwenye shughuli za utalii unalipa dola 2,000. Udhibiti huu naona ni mkali mno.

Mheshimiwa Spika, wafanyabiashara wa utalii wako aina mbalimbali. Wako wenye mahoteli, hoteli inakuwa na vitanda zaidi ya 100, wako wenye mahoteli yenye vitanda 20, wako wenye mahoteli yenye vitanda 10 na wako wenye *tented camps* (mahema). Lakini wote wanawekwa kwenye *group* moja, aliye na mahema 10 wanalala watu 20 analipa dola 2,000. Aliye na hoteli yenye vitanda 100 analipa dola 2,000 na aliye na hoteli yenye vitanda 10 analipa dola 2,000. Aliye na magari manne analipa dola 2,000, aliye na magari 100 analipa dola 2,000. Sasa uwiano hapo naomba Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko angalau isimamie pia hizi leseni za udhibiti ili Watanzania hawa wadogo na wao waweze kukua taratibu waingie kwenye biashara hizi ambazo ni kubwa kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeshauri kwa mfano, kuwe na *flat rates,* leseni ya hoteli dola 100 lakini kila chumba unachokuwa nacho ulipie dola 20. Kwa hiyo, mwenye vyumba 10 atalipa dola 100, jumlisha na dola 20 kwa kila chumba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ataongezewa dola 200. Aliye na vitanda 100 atalipa *flat rate* 100 *plus* 20 mara 100. Kwa hiyo, atalipa 2,100. Vile vile hata wale walio na magari kwa namna hiyo kutakuwa na uwiano wale samaki wakubwa hawawezi kumeza wale wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ilichukulie hili suala kama ni suala muhimu kabisa ili hawa Watanzania wadogo ambao wanaingia kwenye biashara za utalii na wako wengi lakini kinachokwamisha ni hiyo leseni ya dola 2,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo, naomba niseme naunga mkono hoja na niiombe Serikali iipe kipaumbele hizi leseni za uthibiti na si kwa utalii tu na kwa maeneo mengine. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce Kimaro, nilitaka nikukumbushe Kanuni ya 48(7) na ikusaidie na pengine iwasaidie Wabungeni wengine. Kanuni nainukuu inasema: "Mbunge hatazungumzia jambo lolote ambalo yeye mwenyewe ana maslahi ya kifedha nalo isipokuwa baada ya kutaja jinsi anavyohusika na kiwango cha maslahi hayo."

Kwa hiyo, ninafahamu wewe una hoteli na umezungumzia nafuu fulani katika uandikishaji wa leseni za hoteli. Pengine ungetamka tu kwamba hivyo ni kweli. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Hivyo ni kweli Mheshimiwa Spika, mimi nina hoteli na nina maslahi kwenye masuala ya utalii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita msemaji wa mwisho maana sina jina lingine Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Muswada huu wa Usajili wa Biashara katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kuwapongeza Waziri Mheshimiwa Basil Mramba, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje na timu yake kwa ujumla kwa kutuletea Muswada huu ambao kweli utamaliza baadhi ya matatizo ya wafanyabiashara hasa wale wadogo wadogo.

Naomba pia nitumie nafasi hii kwanza kuungana na wananchi wenzangu wa Mkoa wa Ruvuma kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, na pia naomba nitoe pole kwa msiba mwingine ambao umetupata kuhusiana na kifo cha Mheshimiwa Diwani Adam Mwaibabile katika Kata ya Majengo kule Songea.

Mheshimiwa Spika, nichukue pia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa wote ambao walioteuliwa katika nyadhifa mbalimbali, lakini kwa upendeleo zaidi nitaanzia na akinamama, Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro pamoja na Mheshimiwa Dr. Batilda Burian na vile vile kwa nafasi hiyo hiyo iende sambamba na kupongeza sera za Chama cha Mapinduzi pamoja na Serikali yake kwa kutenga nafasi za upendeleo ambazo zimewawezesha akinamama hawa kufikia nafasi hizi ambazo wamezipata.

Naomba pia kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na Mbinga tushukuru pia uteuzi wa Mheshimiwa Gaudence Kayombo, kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Ni faraja kwetu sana.

Mheshimiwa Spika, nirudi sasa kwenye Sheria hii ambayo tunaijadili. Nikienda moja kwa moja kwenye kifungu cha 8. Kimsingi Sheria yote naona ina maslahi na imezingatiwa kwa kina hali halisi ya utendaji wa wafanyabiashara hasa wale wadogo wadogo ambao sifa yao kuu ilikuwa ni kutokusajiliwa. Sasa ina maana wameondokana na ile hali ya kuitwa *informal* sasa watakuwa *formalized.*

Mheshimiwa Spika, katika kifungu hiki kinazungumzia hali ya uwezeshaji wa wafanyabiashara hao. Mara ya mwisho wakati tunajadili Muswada huu kwa kuwashirikisha wadau, kuna mdau mmoja tunamshukuru Bwana Bitala, alizungumzia sana kuhusu hospitali za biashara. Hatujawa na hospitali maalum za kuziwezesha hizi biashara zetu kukua. Kwa hali ya sasa tutasajili lakini lengo siyo kusajili pekee. Ni usajili ambao una mafanikio. Ni usajili ambao tunategemea biashara ikishasajiliwa basi iwe na ule uwezekano wa kuendelea kuishi.

Sehemu kubwa ya wafanyabiashara wetu, tuseme wanafanyabiashara, lakini hawazifanyii kiujasiriamali. Tunahitaji wafanyabiashara wawe pia na uwezekano wa kuwa na utendaji wa kiujasiriamali ambao utawaongezea mapato. Vile vile hata katika maeneo ya uwezeshaji kwa mfano sehemu za huduma za Serikali ambazo zinawasaidia hao wafanyabiashara au wajasiliamali pia na wenyewe watahitaji kuwezeshwa zaidi. Kwa hiyo, katika kifungu hiki nilikuwa naomba kwamba kuwe na dira maalum ya Taifa ambayo itakuwa inaweka sehemu ambazo mfanyabiashara mdogo au mjasiliamali anapokuwa amekwama anaweza kwenda pale na kupata ushauri nasaha kama ilivyo katika maeneo mengine.

Kwa mfano, anasema kwamba nimelima mahindi mengi safari hii sina pa kuuzia, nitafanyaje? Basi akifika pale aweze kuambiwa kwamba hayo mahindi sasa hivi Mbeya kuna njaa, peleka Mbeya au akisema kwamba biashara yangu naona kila nikiuza nakaa toka asubuhi mpaka jioni sipati chochote, bora nifunge. Aulizwe unafanya vipi, je, unaosha angalau yale maembe yako mteja akikuita anahitaji embe unampelekea au unamwambia siwezi kukuletea, njoo uchukue. Kwa hiyo, hizi taarifa ndogo ndogo au ufahamu mdogo mdogo ambao unaboresha mazingira ya biashara ni vema sasa hawa wafanya biashara tukawaandalia mazingira ya kuweza kupata huduma kama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine nataka niuelekeze jinsi ambavyo huduma itatolewa. Tunafahamu kutakuwa na vituo maalum vya kusajili. Lakini tulikuwa tunaona kwamba sasa hivi wananchi wengi kwenye maeneo haya ya vijiji wanafanya hizi shughuli ndogo ndogo za biashara au za ujasiliamali kwa ujumla. Sehemu ambazo zitawekwa zinaweza kuwa zisiwafikie rahisi wananchi wengine ambao wako mbali zaidi hasa tukizingatia kwamba kuna maeneo hayana miundombinu za kutosha. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba kwa kutumia mikono yaani vyombo vingine ambavyo viko tayari kwenye yale maeneo kwa mfano Maafisa Watendaji, wanaweza wakasaidia kukusanya taarifa za watu katika maeneo yale ili kuongeza uwigo wa usajili wa wafanyabiashara hawa wadogo wadogo. Wala tusipuuzie kwamba kwenye maeneo ya vijiji hakuna shughuli kama hizo, zipo. Kuna miji midogo midogo ambayo inafanya

shughuli nyingi tu na hivyo itaweza kuongeza idadi ya wananchi au wafanyabiashara ambao watakuwa wamesajiliwa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba pia kuangalia katika maeneo ya wafanyabiashara ambao biashara zao hazitasajiliwa mpaka kwanza ziwe zimepata zile leseni ambazo zinahusiana na biashara zao. Biashara maalum kwa mfano, biashara hizi za utalii au zinazohusiana na mambo ya chakula au zinazohusiana na mambo usalama kwa mfano shughuli za umeme. Kwa sasa hivi leseni zinatolewa katika baadhi ya maeneo tu. Inaleta mzigo mkubwa kwa wafanyabiashara kama hao ambao pia wao ni kiungo kikubwa cha kuzalisha biashara kwa hawa wafanya biashara wadogo wadogo. Kwa hiyo, nilikuwa naomba pia katika maeneo hayo, nao waangalie uwezekano wa kusogeza huduma kama ambavyo leo Wizara yetu ya Viwanda, Biashara na Masoko imeona umuhimu wa kuzisogeza huduma hizo mpaka katika maeneo ya Mikoa na Wilaya zake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi nimehusika sana katika kuchangia Muswada huu na vile vile kwa kuwa unasisitiza maswala ya *standard and speed* nadhani nisichukue muda mrefu sana badala yake tumalizie shughuli yetu ili tuweze kuhakikisha kwamba sheria hii inapitishwa na inaanza kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SALOME J. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kutoa salaam za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Spika, na familia nzima ya Mheshimiwa Juma Akukweti (Marehemu) kwa kuondokewa na mpendwa wao. Pia ninatoa salaam hizo hizo kwa wana familia na maaofisa wengine waliofariki katika ajali iliyotokea.

Mheshimiwa Spika, pia ninatoa pongezi kwa Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Gaudence Kayombo, kwa kuteuliwa katika nyadhifa zao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, tukirudi katika hoja, ninaomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kuleta Muswada huu ambao kwa kweli umechelewa kuja. Muswada huu ni muhimu sana kwani biashara ni nyanja moja kubwa inayochangia katika kukuza uchumi katika nchi yoyote hasa zinazoendesha uchumi wa ushindani wa soko. Kwa namna hiyo ni lazima biashara iwe huru isiyokuwa na kero/masharti yasiyo ya lazima ili iweze kutoa mchango wa maendeleo ya uchumi kikamilifu. Ndiyo maana tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha *Best Programme,* MKURABITA na MKUMBITA na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini wengi tunafikiri kuwa kuendesha biashara katika mazingira ya soko huru la ushindani tunaweza tu kufanya tunayotaka. Mfano hai ni biashara ya zao la korosho katika mikoa ya Kusini, ambapo wafanyabiashara

wametengenezea ukiritimba *cartel* na *collussion* ili kuwakandamiza wakulima kwa kutoa bei ndogo. Suala hili ni ku-*abuse* kanuni za biashara katika soko huru. Soko huru lina kanuni zake na taratibu za udhibiti *(ethics)* za biashara.

Mheshimiwa Spika, ifike mahali sasa Wizara iunde chombo maalum *(equivalent* ya *Antigust body* ya Marekani). Kazi yao kubwa ni kufanya *intervention* wakati wafanyabiashara wanapo-*abuse* taratibu za soko huru. Chombo hicho kitakuwa kama refa wa mchezo huu wa biashara katika soko huru. Bila ya chombo hicho wafanyabiashara wataendelea ku-*abuse* biashara na kuleta adha, umaskini kwa wananchi na kilikosesha Taifa mapato. Bila ya chombo hicho wafanyiashara ndiyo watageuka Serikali. Tuunde chombo hicho ili kiweze kusimamia na kuratibu na kutoa mwelekeo wa mchezo wa *market economy.* Huu ndiyo ushauri wangu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga hoja mkono.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kuleta huu Muswada muhimu.

Ninapenda kupendekeza badala ya *TIN Number* tuwe na kitu kinachoitwa *PIN number* yaani *Personal Identification Number* ili kuwaondolea wasiwasi wafanyabiashara wakati wa kusajili ili kuwaondoa hofu ya kudaiwa kodi kwani kwa wafanyabiashara mengi wasikiapo neno *TIN* kwao ni kikwazo.

Mheshimiwa Spika, mengi tulichangia vizuri wakati wa Kamati. Nazidi kuwapongezeni tena kwa mara nyingine.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa natoa mkono wa rambirambi kwako Mheshimiwa Spika na kwa ndugu na familia ya marehemu Mheshimiwa Juma Akukweti, kwa msiba huu Mungu ailaze pema roho na mwili wa marehemu. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa kusimamia vyema na Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na watendaji wote kwa kazi zao kwenye Wizara hii. Kwa heshima kubwa naiomba Serikali kutoa uwezo zaidi ili Wizara iwe imara na kutekeleza kazi za Wizara na Idara na mashirika. Biashara ziende na wakati na Serikali ya Awamu ya Nne ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Muswada huu wa Sheria wa *Business Activities Registration,* naomba usimamiwe mchango wa huu Muswada. Uwe na wafanyabiashara na wale wanaokuza biashara watambuliwe na Serikali itowe elimu na maadili mazuri ya kisasa, pia kuwezesha kikamilifu kufanya biashara ndani na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Muswada usicheleweshwe. Upitishwe na kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Magogoni naunga mkono hoja hii kwa asilimia zote.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuungana na wenzangu kuwapa pole wale wote waliopoteza wapendwa wao katika ajali ya ndege iliyotokea Mbeya, pia nawapa hongera wale wote waliopata nafasi mbalimbali za uongozi hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, mimi ninayo hofu kubwa sana na Muswada huu, unalenga kuwaondoa Watanzania wenye mitaji midogo na wasio na elimu katika kujiajiri katika sekta ya biashara kwa kuwepo na taratibu ambazo aidha, juhudi za makusudi zifanyike za kutoa elimu stahiki.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika lipo kundi kubwa la wafanyabiashara ndogo ndogo ambao pia ni walipa kodi lakini hawajasajiliwa na kupewa namba ya walipa kodi *(TIN Number)* na moja ya masharti ya usajili huu wa biashara. Naomba kupata ufafanuzi kwamba kundi hili linajiondoa katika biashara?

Mheshimiwa Spika, kutokutajwa ada na gharama za usajili katika sheria bado inatia mashaka tunapoteza mapato kutoka kwa wafanya biashara ni lazima walipie, hawa wanao uwezo inasikitisha tunachangia elimu, maji na afya tunawasamehe matajiri ada yote itakayopatikana iwekezwe kwenye mifuko ya elimu ya Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, usajili huu urahisishwe na kuwa na usimamizi unaokuwa wazi zaidi kuondoa migongano inayoweza kujitokeza, Halmashauri, Msajili, *BRELA* na Wizara.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana na sasa kwa kufunga mjadala, ni nafasi ya mtoa hoja lakini atatanguliwa kwa muda ule ule uliopangwa watagawana. Namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, baadaye mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hoja hii ya Muswada ulioko mbele yetu asubuhi hii. Lakini pengine kabla ya hapo na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kusimama hapa Bungeni na kusema kwa kutoa rambirambi nyingi sana kwa kifo ndugu yetu mpendwa Mheshimiwa Juma Akukweti, aliyetutoka.

Lakini vile vile niwapongeze wale wote waliopata nyadhifa mbalimbali kwa uteuzi uliofanyika hivi karibuni. Kwa kipekee nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na vile vile nawapongeza Mheshimiwa Dr. Batilda Burian kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Bunge. Nampongeza sana na kwa jinsi tunavyomfahamu kwa umahiri wake najua kabisa kwamba tutashirikiana naye katika kutekeleza shughuli ambazo zilikuwa zinafanya na Mheshimiwa Juma Akukweti. *(Makofi)*

Pia nampongeza Mheshimiwa Bernard Membe kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Nawapongeza pia Manaibu Waziri, Mheshimiwa William Ngeleja, Mbunge wa Sengerema kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Mheshimiwa gaudence Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo kwanza napende nitamke wazi kwamba naunga mkono hoja iliyoko mbele yetu na niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika Muswada huu. Kwa ujumla tunataka kuwashukuru na kuwapongeza kwamba wametusaidia sana kwa kutupa nguvu kwa kuona kwamba Muswada huu una maana yake. Makusudio makubwa kama ambavyo ilielezwa katika maelezo ya mtoa hoja ni kuondoa kero ambazo zilikuwepo huko nyuma. Lakini vile vile kuwatambua wafanyabiashara kama ni sehemu ya jamii kama walivyosema baadhi ya wachangiaji, kwa hiyo, nitoe wito na mimi kwa wafanyabiashara wote kwa kuwahakikishia kwamba hakuna haja ya kusitasita kwenda kujiandikisha kwa sababu nia na madhumuni ni mazuri ya kutaka kuwajua wanafanyabiashara gani na kusema kweli ukishafahamika unafanya nini hata kama kutakuwa na msaada wa namna yoyote ile ambao utakuwa unahitajika, itakuwa ni rahisi kukufikia.

Kwa hiyo, nia ya Serikali ni nzuri na tunashukuru kwamba Waheshimiwa Wabunge wameutambua hivyo na tunaongezea kutoa wito katika hilo wa kushirikiana katika utekelezaji. Pengine nijielekeze katika maeneo mawili tu ambayo nataka niyatolee maelezo.

Mheshimiwa Spika, katika michango mbalimbali iliyotolewa hapa na Waheshimiwa Wabunge limejitokeza suala moja la jumla ambalo ni la msingi kwamba ni vizuri kwa sababu sheria hii ni mpya na ina makusudio mazuri kwa wananchi itolewe elimu kwa wadau, pamoja na wananchi wote kwa ujumla waelewe kwamba nia ya Muswada ni mzuri. Nataka niseme kwamba katika hilo Serikali imejiandaa vya kutosha kwamba itaendelea kutoa elimu katika ngazi mbalimbali kwa sababu hivi sasa ninavyozungumza kazi ya utoaji elimu inaendelea kwa kutumia vyombo vyetu mbalimbali ikiwemo kama *SIDO* ambao wanatoa semina pamoja na maelekezo mbalimbali ya wajasiriamali.

Mheshimiwa Spika, nadhani kwamba kwa kutumia fursa hiyo tutaendelea pia kutoa elimu kwa wananchi kwa ujumla juu ya utekelezaji wa Muswada huu ambao utakuwa ni wa manufaa kwao vile vile. Sasa katika vipengele mbalimbali ambavyo vimepitiwa na Waheshimiwa Wabunge hapa nataka nikumbushe kwamba kwa bahati mzuri kama ambavyo walisema, tulikuwa tumeshapitia katika kikao kile cha wadau pamoja na Kamati yetu ya Uwekezaji na Biashara na kukubaliana katika maeneo mengi. Ndiyo maana kama mtakavyokuwa mmeona katika ile *Schedule of Amendment* kuna baadhi ya mambo ambayo tulikuwa tumekubaliana na Waheshimiwa Wabunge lakini pamoja na yale ambayo yalizungumzwa na Waheshimiwa Wadau waliokuja kwenye kikao kile yamezingatiwa kwa kiwango kikubwa sana. Muswada huu kwa kweli unakusudia uweze kuwa ni wa kuboresha shughuli za biashara na kwa hiyo kwa sababu tutakuwa tunatekeleza kwa pamoja baadhi ya vipengele vingine ambavyo vitahitaji

marekebisho pengine yatakuwa yanajitokeza kadri tutakavyokuwa tunakwenda mbele ya safari.

Lakini kubwa zaidi kama tulivyokuwa tumekubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwenye Kamati kwamba baadhi ya mambo yataingizwa katika Kanuni ambazo zitakuwa zinasimamia utekelezaji wa Sheria, tunadhani kuwa ufafanuzi utakaokuwa umetolewa ni huo huo tutakaokuwa tunautumia katika kuelimisha wananchi kwa ujumla katika kutekeleza sheria hii na sisi tunataka tu kuahidi kwamba tutakuwa pamoja na nyinyi na ninyi muwe pamoja nasi katika kuhakikisha kwamba tunapeana ushauri wa hapa na pale tunapokuwa tunatekeleza sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada huu kwa sababu wametuunga mkono na wanatutia moyo kwamba tuendelee katika kuitekeleza na kwa hiyo, nimalizie kwa kusema kwamba tuunge mkono na hatimaye twende katika utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo namalizia kwa kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniita tena niweze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Labda niseme kwamba Waheshimiwa waliochangia hoja hii kwa majadiliano ni saba ambao ni Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Aloyce Kimaro na Mheshimiwa Stella Manyanya. Hao ndiyo waliochangia kwa majadiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna waliochangia kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa ambaye nitamtaja baadaye. *(Makofi)*

Samahani ni Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis. Hawa wote kwa ujumla wao ningependa niwashukuru kwa sababu wote wameunga mkono lakini wana mapendekezo na mimi ningesema kwamba baadhi ya mapendekezo hayo hasa yale yaliyotokana na Wajumbe wa Kamati tumeyazingatia na kama nilivyoeleza kwenye Kamati baadhi ya hayo tutayaweka vizuri zaidi kwenye *Regulations* kwa sababu Sheria hii inamruhusu Waziri kuweka *Regulations.* Baadhi ya mambo tutayaweka vizuri kwenye *Regulations.*

Mheshimiwa Spika, itachukua muda gani, ilikuwa inaulizwa kwenye Kamati. Natoa hapa kama mfano, kwamba je, itachukua muda gani mtu kupeleka fomu na kupata majibu na mimi nimesema nitafanya hivyo kwenye *Regulations* kwamba ukipeleka fomu ya maombi ni lazima ndani ya siku tano za kazi au wiki moja uwe umeshapata cheti chako cha uandikishaji. Kwa hiyo, ziko hoja huku ambazo zimetajwa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, zimetajwa na Mheshimiwa Lucy Owenya, ambazo tutaziweka vizuri zaidi kwenye *Regulations* siyo kwamba tumezisahau.

Hili la uandikishaji la Mheshimiwa Said Amour Arfi, ni muhimu hata wafanyabiashara wadogo wawe na *TIN number* ili watambuliwe. Kuna Waheshimiwa wengine wanaosema *TIN number* zitawaogopesha wanaojiandikisha kwa hiyo, wanaweza wasijiandikishe. Kama nilivyosema wakati wa Kamati nitashauriana vizuri zaidi na Waziri wa Fedha kuona namna bora ya kuifanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Fuya Kimbita anasema labda uweke tu kitu cha kujiandikisha, kuwa na namba ya kujiandikisha lakini isiwe ni namba ya kodi ili kutoogopesha watu. Inawezekana kwa sababu hata kile cheti cha kujiandikisha chenyewe kina namba, kitakuwa na namba. Labda mtu anaweza akajitambua kwa namba hiyo. Lakini kama nilivyosema nitawasiliana vizuri zaidi na Waziri wa Fedha tuone njia nzuri zaidi ya kufanya jambo hili, kwa sababu ni kweli kuna watu wanaotaka hizo *TIN number* na kuna watu wanaziogopa. *(Makofi)*

Labda jambo la maana la kufanya ni elimu zaidi kama inavyopendekezwa hapa lakini vilevile ni kushirikisha zaidi, Waziri wa Fedha. Hili la elimu kwa umma, ni muhimu mno na nafikiri ndio kazi ya kwanza na hatuwezi kufanikiwa kufanya hizi kazi nyingine bila hii elimu ya umma, kwa mfano tutakapoanza tu kuandikisha, kusema watu wajiandikishe upya ili muweze kutambuliwa itabidi kampeni ifanywe kwenye vyombo vya habari, magazeti, kwenye redio, kwenye televisheni na kwenye mabango.

Mheshimiwa Spika, ni kazi kubwa na lazima ienee nchi nzima, kila mahali hata vijijini, la sivyo ikieleweka vibaya hii kazi ya kuandisha biashara itakuwa ngumu sana, kwa hiyo, ni kweli tutatoa elimu ya kila jambo linalohusika na uandikishaji wa biashara hizi.

Hizi *regulatory licences* zile leseni za wadhibiti hizi leseni za wadhibiti ni kazi moja kubwa sana ambayo imebaki. Ugumu wake ni nini? Kwa mfano, Mheshimiwa Spika wewe mwenyewe unafahamu kwamba pale Dar es Salaam ile *Supermarket* inayoitwa *Shoprite,* mle ndani kuna leseni nadhani kumi na tatu au kumi na tano mle ndani. Maana yake akiuza mkate kuna leseni yake na taratibu zake za kuoka mkate, akiuza nyama vivyo hivyo, akiuza bidhaa za kawaida kuna namna yake, mle ndani yule mwenye ile *Supermarket*, anatakiwa atimize masharti ya leseni zisizopungua kumi tatu, kumi na nne, kumi na tano. Siku nzima ni kujaza fomu, kukutana na watu kujieleza hapa na wakaguzi wanapoingia kule ndani wanaweza wakaingia wakaguzi watano kwa siku, huyu anakagua nyama, huyu anakagua hili, huyu anakagua lile, ni kazi ngumu sana, haya ndiyo mambo tunayotaka kuyaangalia. Je, atahitaji leseni zote hizo?

Kwenye hoteli tumefanikiwa kupitia sheria ya fedha kusema kwamba mtu akiwa na hoteli hahitaji tena leseni nyingine yoyote mle ndani kwani inatakiwa ukiwa na hoteli kama una baa leseni tofauti, vile vitanda leseni tofauti, kama kuna duka humo leseni tofauti, kama kuna *bookshop* leseni tofauti, kama kuna *bureau de change* huko ndani leseni tofauti, kama kuna benki huko ndani leseni tofauti. Kwa hiyo, kuna usumbufu sana, lakini kwenye hoteli tayari tumeshaanza kufanikiwa kupunguza leseni, inakuwa moja isipokuwa zile leseni ambazo ni *regulatory* kama kuna benki kule ndani, ile benki

kule ndani tawi la ile benki litahitaji kibali cha Benki Kuu yaani leseni ya Benki Kuu *regulatory*.

Kwa hiyo, kazi hii sasa hivi naelezwa na wataalamu kwamba utafiti unaendelea na huo unafanywa chini ya Wizara ya Mipango, utafiti unaoendelea tayari umeshaona eneo moja ambalo tunaweza tukalirahisisha. Leseni ya vyombo vya fedha. Kwa hiyo, maagizo yangu sasa ni kwamba kila tunapomaliza aina moja ya *regulatory licence* tunaileta hapa Bungeni hata kama ni chini ya sheria *Miscellaneous Amendment*, ili tuendelee kupunguza badala ya kusubiri labda miaka mingine mitano ndio tuje na sheria nyingine hapa ya *regulatory licences* tunaendelea kuzingupunguza kadri muda utakavyokwenda kama utafiti utakavyoonyesha kwamba kunahitajika mabadiliko na ya namna gani ili turahisishe sana hii kazi.

Mheshimiwa Spika, juzi, mapema wiki hii Mheshimiwa Rais alipokuwa kule Davos, mimi nilibahatika kuwepo. Alikutana na Rais wa Benki ya Dunia na kati ya mambo Benki ya Dunia wanataka kujua ni je Tanzania mmepiga hatua gani katika kupunguza gharama za kuendesha biashara na sisi tulimweleza kwamba wiki hii tunaleta Muswada hapa katika kupunguza gharama za kuendesha biashara Tanzania. Hii mizunguko ina gharama sana na wingi wa leseni zisizo za lazima ni gharama sana, watu wa nje wanashangaa kabisa kwamba kuna leseni nyingi namna hiyo na vibali vingi namna hiyo na uandikishaji mkubwa namna hiyo kuhusiana na biashara.

Kwa hiyo, ni jambo kubwa na sisi wenyewe tunataka kulimaliza ili litupe sifa kwamba Tanzania gharama za kufanya biashara, *the cost of doing business* ni chini, inalingana na viwango vya Kimataifa yaani *International best practise.*

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na madukuduku miongoni mwa wale waliotuletea kwa maandishi na hata walizungumza juu ya Mawaziri na msajili. Wako Mawaziri wanaotajwa kwenye sheria hii, Waziri mhusika anayehusika na biashara ambaye ndiye atakaye tawala sheria hii kwa maana ya sera na katika taratibu za rufaa.

Lakini kuna Waziri wa pili anayeteua wale wasajili katika ngazi ya Wilaya ambaye ni Waziri wa Serikali za Mitaa na ametajwa hapa. Kwa nini, kwa sababu nadhani hili lilikuwa ni wasiwasi pia wa Mheshimiwa Lucy Owenya, ni kwa sababu tunataka tusibomoe ile dhana ya madaraka Wilayani na maboresho ya Serikali za Mitaa. Hatutaki kuibomoa, kwa sababu Serikali za Mitaa ndio katika hali halisi zinazosimamia biashara, hata leo ndio wanaotoa leseni za biashara.

Mheshimiwa Spika, tunachofanya sasa ni kusema Serikali ya mitaa sasa isiwe ndiyo chombo cha kuandikisha biashara, badala yake biashara zitaandikishwa kwa utaratibu wa sheria hii yaani huu wa kusajili, lakini msajili atakuwa pale pale kwenye Wilaya, Halmashauri ya Wilaya inawezekana ikawa yule Ofisa wa Biashara aliyekuwa pale kama atakuwa ametimiza masharti haya akawa ndiye huyo huyo atakayeitwa msajili wa biashara, lakini kwa kutegemea mazingira ya Halmashauri wanaweza wakateua aina nyingine ya mtu. La maana ni kwamba mtu huyu ni mtumishi wa Serikali za Mitaa, sio mtumishi wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, kwa hiyo *disciplinary authority*

(mamlaka ya kumdhibiti huyu mtu) yako kwa Waziri wa Serikali za Mitaa, ndio maana tumeiacha huko kutakapotokea madudu na malalamiko na mambo ya namna ile udhibiti wake utafanywa kwa taratibu za Serikali za Mitaa.

Lakini atakayesema, atakayetoa kauli juu ya sera ya biashara, mienendo ya biashara ni Waziri wa Biashara, ndio maana itakapofika kwenye mfanyabiashara analalamika kwamba msajili yule pale Wilayani anamdhulumu tunasema hapa kwamba kwenye taratibu, kwenye *regulations,* kanuni, tutasema kwamba mtu akimlalamikia yule msajili pale Wilayani, Mkuu wa Wilaya atasikiliza lalamiko hilo, Mkuu wa Wilaya ni kwa sababu Mkuu wa Wilaya sio sehemu ya Serikali za Mitaa, ile ni Serikali Kuu. Asiporidhika na maamuzi ya Mkuu wa Wilaya, kwa mujibu wa mabadiliko ambayo tumependekeza kwenye Muswada ya majadiliano katika Kamati, yule bwana au bibi anaweza sasa au Kampuni inaweza ikaleta rufaa kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Sheria inasema Waziri ataunda jopo la watu wa kumshauri, inasema sheria kwamba Waziri ataunda jopo la watu wa kumshauri na yeye atasikiliza rufaa hiyo ambayo itakuja kwa maandishi na kwa sababu hiyo ataamua kama mlalamikaji bado hakubaliani na *DC* na bado hakubaliani na Waziri aliyeshauriwa na jopo, anaweza kwenda Mahakama Kuu, yule mlalamikaji anaweza kwenda Mahakama Kuu kulalamika kwamba Mkuu wa Wilaya, Waziri na jopo lake hawakumtendea haki. Kwa hiyo, Mahakama Kuu inaweza ikaamua na ndio maana kwa sababu hiyo hiyo uamuzi wa faini pia tumeuachia Mahakama na iwe faini kiasi gani tumeachia mahakama kwa sababu Mahakama ikifanya inakuwa ni jambo bora zaidi kisheria kuliko kufanya tu kiutawala.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wako Mawaziri wawili na mantiki yake ndiyo hiyo lakini kuna Mahakama pia ambayo inaweza ikaamua kwa mara ya mwisho kama mtu hakubaliani na Waziri. Halafu sasa kuna *BRELA*. Inahusikaje hapa, *BRELA* inahusikaje hapa. Tunasema msajili yuko pale kwenye Halamshauri au kwenye Jiji au kwenye Manispaa yule msajili yuko pale, aliyeteuliwa na Waziri wa *Local Government* sio Mkurugenzi wala sio Bwana Mkubwa wa *BRELA*. Akishateuliwa tayari kazi zake anayezisimamia na kuzielekeza sio Halmashauri tena, ni *BRELA* ni Msajili Mkuu wa Taifa ambaye ni *BRELA*. Kwa nini, kwa sababu mtiririko wa maagizo ya kisera na kadhalika unaanzia Wizarani na Wizara ile ndiyo inayosimama *BRELA*. Utendaji wa kuandikisha unaanzia pale kwenye Wilaya kwa Msajili yule aliyeteuliwa pale.

Lakini msajili yule kiutaratibu na kiutaalamu na hii tunayoita hapa *best practice* anaripoti kwa Msajili Mkuu yule *Registrar of Businesses* ambaye ni *BRELA*. *BRELA* ndiye *registrar* wa makampuni, ndiye anayeandikisha majina ya makampuni na kadhalika anafanya kazi hizo. Kwa hiyo, hivi sasa yeye kiutaratibu ataunda *registry* ofisi ya uandikishaji, ambapo kutakuwako *registry* mbili, *registry* ile ya Wilayani ambayo anaisimamia yu ile *registrar* wa pale Wilayani na *registry* ya Kitaifa ambayo anaisimamia huyu bwana wa *BRELA*. Kwa hiyo, *registry* hizi mbili ndizo zinazosaidia na kuna utaratibu kila miezi mitatu, lazima taarifa zitoke kote, kila Wilaya, kila Halmashauri, kila Manispaa na huyu Msajili Mkuu wa Taifa na pia hata yule wa wilaya ni lazima kila miezi mitatu atoe taarifa za kazi zao tumeandikisha biashara 20 katika Wilaya ya Kongwa, 40 Mpwapwa, 100 Dodoma Mjini, zote zile kwa njia za mitandao ya

kisasa zinafika Dar es Salaam kwa msajili mkuu, yule naye anaweka orodha, ana *compile* matokeo kitaifa, Mkoa wa Dodoma biashara fulani za bucha, biashara fulani za maduka, biashara fulani za kitu fulani na kadhalika; naye anachapisha kitaifa.

Kwa hiyo, kuna toka *National Statistics* kama zinazotolewa na Benki Kuu kuonyesha hali ya uchumi imekuwaje mwezi uliopita au kipindi kilichopita. Kwa hiyo, wachumi na watu wanaofuatilia masuala ya mienendo ya biashara na wafanyabiashara wenyewe wanaweza kabisa wakajua kabisa kilichotokea miezi mitatu iliyopita, kuna watu wangapi wanaochinja ng'ombe wenye maduka ya ng'ombe, kuna watu wangapi wenye maduka ya rejareja  na maduka ya *size* gani, kuna mitaji kiasi gani imewekezwa kwenye maduka, kuna biashara ngapi zimefilisika na zimekufa na kwa nini, kuna biashara ngapi zina suasua, kuna biashara ngapi zimekua kubwa, kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Kimaro zimekuwa kubwa jana zilikuwa ndogo, kuna biashara zipi zilizokuwa hata hazikuandikishwa zilikuwa huko kwenye MKURABITA lakini sasa zimekua na zinatambulika ni ngapi.

Kwa hiyo, hizi takwimu ndiyo kazi kubwa itakayotumika katika kufuatilia mwenendo wa biashara na uchumi katika nchi yetu.  Kitu hiki hakikuwepo, hivi leo ukiniuliza kuna biashara ngapi katika nchi hii sijui, hatuna utaratibu wa kujua ni biashara ngapi katika Wilaya hii, katika mkoa huu, katika nchi hii. Kuanzia sheria hii itakapokuwa sheria tutaanza kuweka takwimu hizo na zitakuwa wazi na zitaapishwa wazi, mtu yoyote akizitafuta kwenye website na sheria hapa inasema ukizitafuta tu kwenye website unaweza ukajua biashara hizi ni za kina nani ziko wapi zinafanya nini zinaenda vizuri ama haziendi vizuri, zinakwama, zimekufa, zimefilisika ama hazijafilisika, yote hayo unaweza ukayapata. Kwa hiyo, huo ndio uhusiano kati ya Mawaziri, wasajili na *BRELA* Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache ningependa nimalizie tu kwa kusisitiza kwamba kwa kweli kazi haijaanza, kazi itaanza mara Waheshimiwa Wabunge mtakapoidhinisha ili kusudi Rais akiweka sahihi ndio tufanye kazi ya kitaalamu sasa inayotakiwa katika biashara ya kitaalamu na ya uhakika kwa sababu sheria inatulazimisha kufanya kazi hii kwa kutumia vyombo vya kisasa na taaluma za kisasa.

Ningependa kuwashukuru hasa Kamati, narudia na Kambi ya Upinzani kwa kuunga mkono kimsingi.  Nataka kuwahakikishieni kwamba kwa sababu jambo hili nilianza nalo, nilianza nalo toka mwaka 2001 kwenye hotuba ya bajeti,  hii ni kama tamati ya kazi ambayo ilianza huko nyuma, ni kazi ambayo tumenuia siku nyingi kuifanya tunajua kwamba ni lazima tuifanye, tunajua namna ya kuifanya ni suala tu sasa la kujipanga vizuri na kulifanya kwa utaalamu na uandilifu wa kazi inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tena kutoa hoja kwamba Bunge sasa liidhinishe hoja hii ili tuweze kusonga mbele. Naomba kutoa hoja.  *(Makofi)*

*(Hoja iliamliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Kusomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Usajili wa Biashara wa 2006**
***(The Business Activities Registration Bill, 2006)***

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 7

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 8

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 12

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 13

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 26

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Usajili wa Biashara wa Mwaka 2006**
***(The Business Activities Registration Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati yako ilikaa, imepitia Muswada uitwao *The Business Activities Registration Bill, 2006* pamoja na marekebisho yake na kukubali bila marekebisho yoyote. Naomba kutoa hoja sasa kwamba Muswada huu pamoja na marekebisho yake ukubaliwe.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada wa *Business Activities Registration* umekwisha pitishwa na Bunge na kwa kuwa hakuna tena muda unaotosheleza kuingia kwenye shughuli za kujadili Muswada mwingine sasa nasitisha Bunge hili hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06.22 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kuchukua nafasi hii kuwatakia heri ya mwaka mpya 2007.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria mbalimbali (Na.2) wa mwaka 2006 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendment (No.2) Bill, 2006*)

*(Kusomwa mara ya Pili)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa *the Written Laws (Miscellaneous amendments) No.* (2) *Act*, 2006 pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukutakia wewe mwenyewe, Waheshimiwa Wabunge pamoja na wapiga kura wenu heri na fanaka ya Mwaka Mpya. Tunamshukuru maulana kwa kutupa uhai na afya kwa mwaka 2006. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, aendelee kutupa afya njema na nguvu kwa mwaka huu wa 2007 na miaka ijayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu, mwaka huu tumeuanza kwa majonzi makubwa baada ya kumpoteza ndugu yetu mpendwa Juma Jamaldin Akukweti, ambaye Muumba aliamua kumchukua mapema mwaka huu. Kifo kimetunyang'anya ukarimu, ucheshi na msaada mkubwa wa rafiki yetu mpendwa, mwenzetu na ndugu yetu tuliyefanya naye kazi kwa karibu ndani na nje ya Bunge letu hili Tukufu. Napenda kutoa rambi rambi kwa familia yake, ndugu na Wananchi wa Jimbo la Tunduru. Mungu ametoa na Mungu ametwaa. Tunamwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake Mahali pema Peponi Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue vile vile fursa hii kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Dr. Asha-Rose Migiro, alikuwa Mbunge, hivyo Bunge lako Tukufu lina kila sababu ya kujivunia uteuzi wake. Lakini kubwa zaidi sasa jina la Tanzania litaendelea kung'aa duniani. Mheshimiwa Migiro ni Balozi wa Bunge letu, nchi yetu na Afrika kwa ujumla. Tunamwombea afya, baraka na fanaka katika majukumu yake mapya. *(Makofi)*

Hali kadhalika, naomba pia kuwapongeza wenzetu, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Gaudence Kayombo na Mheshimiwa William Ngeleja, kwa uteuzi wao hivi karibuni kuwa Mawaziri na Manaibu Waziri. Nao pia tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu awape afya njema, baraka na fanaka nyingi ili waendelee kumudu majukumu yao hayo mapya kwa umakini unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muswada ulioko mbele yetu, naomba nianze kwa kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Malima Lubeleje**,** Mbunge wa Mpwapwa, kwa kupitia na kuchambua Muswada huu na kwa ushauri mzuri walioutoa, umetuwezesha kuuwasilisha mbele yako Muswada huu. Tunawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kazi nzuri waliyofanya na kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu uitwao *the Written Laws Miscellaneous Amendments Act* wa mwaka 2006 unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali zifuatazo:-

- Sheria ya Udhibiti wa Mali inayotokana na Uhalifu, Sura ya 256;
- Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20;
- Sheria ya Urejeshaji wa Wahalifu, Sura ya 368;
- Sheria ya Ushirikiano na Nchi Nyingine katika Kudhibiti Vitendo vya Jinai, Sura ya 254;
- Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006;
- Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya mwaka, 2004;
- Sheria ya Makosa ya Uhujumu wa Uchumi, Sura ya 200;
- Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6;
- Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ya mwaka 2005; na
- Sheria ya Tume ya Utumishi wa Mahakama ya mwaka 2005.

**MAUDHUI YA MUSWADA**

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Kumi na Moja.

Sehemu ya Kwanza ya Muswada huu inahusu masuala ya utangulizi yanayojumuisha jina la Sheria inayokusudiwa kutungwa na Sheria mbalimbali zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho.

Sehemu ya Pili ya Muswada inatoa mapendekezo ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Mali inayotokana na Uhalifu, *(Proceeds of Crime Act Cap. 256).*

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho haya yana uhusiano mkubwa na makosa yaliyoainishwa katika Sheria ya Kudhibiti Fedha Haramu ambayo ilitungwa na Bunge letu Tukufu hivi karibuni katika kikao kilichopita. Mathalan Fungu 28 la Sheria ya Kudhibiti Fedha Haramu (*Anti Money Laundering Act, 2006*) linaweka masharti kwamba:

> "*The procedure in relation to arrest, information gathering, powers, trial, determination, confiscation, forfeiture, pecuniary penalty and restraining orders and control of property liable to confiscation shall be in accordance with the provisions of the Proceeds of Crime Act".*

Hivyo basi, imeonekana ipo haja ya kufanya marekebisho katika sheria hiyo ili iendane na wakati. Sheria hiyo ilianza kutumika tangu mwaka 2001 na mambo mengi yamefanyika tangu wakati huo.

(a) Mabadiliko ya kwanza katika Sheria hii ni ya tafsiri. Inapendekezwa kwamba ile tafsiri ya maneno "benki," "Taasisi za fedha" "makosa ya fedha haramu", "madawa ya kulevya", sasa iwiane na Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, Sheria ya Kudhibiti Fedha Haramu ya mwaka 2006 na Sheria ya Kudhibiti Biashara Haramu ya Madawa ya Kulevya, Sura ya 95.

Kama inavyofahamika tafsiri ya maneno hayo iliwekwa tangu mwaka 2001, wakati Sheria hiyo ilipotungwa. Hivyo, tafsiri katika Sheria hii haikidhi dhana ya mazingira mapya yaliyojitokeza siku za karibuni hapa nchini na sehemu nyingine duniani. Tafsiri inayopendekezwa tayari imekubaliwa na Bunge kupitia Sheria mbalimbali zilizokwishatungwa. Aidha, tafsiri hizo ndizo zinazotumika katika nchi nyingi za Jumuiya ya Madola na *SADC* ambazo tunashirikiana nazo katika kudhibiti uhalifu.

(b) Inapendekezwa pia kufanya marekebisho ya kichwa cha habari katika sehemu hiyo na kuongeza masharti ya kuboresha utaratibu wa utaifishaji wa mali zinazopatikana kwa njia ya uhalifu kama ifuatavyo:-

(i) Mwanasheria Mkuu wa Serikali anapoomba Mahakama kutoa amri kutaifisha mali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu, basi atoe taarifa kwa mtu anayemtuhumu na kwamba muda wa kutoa taarifa hiyo usipungue siku kumi na nne. Hivi sasa hakuna muda maalum wa kutoa taarifa hiyo.

(ii) Ikiwa wakati maombi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yanaendelea kusikilizwa na Mahakama, mali nyingine haramu zitapatikana, basi atapaswa kutoa ilani ya kufanya mabadiliko katika maombi ya awali ili mali hiyo iliyopatikana iongezwe kwenye orodha ya mali zitakazotaifishwa. Ilani hiyo itatakiwa kutolewa ndani ya muda

usiozidi siku kumi na nne. Mapendekezo haya hayatahusu utaifishaji wa mali haramu zinazomilikiwa na makampuni.

Aidha, inapendekezwa chini ya Muswada huu kwamba hata mali haramu zilizofichwa kwa wadhamini pia ziweze kukamatwa na kutaifishwa. Ili kutekeleza malengo hayo, fungu la 23(2) inapendekezwa kufanyiwa marekebisho.

(iii) Inapendekezwa vilevile kuwaongezea nguvu za kisheria wapelelezi wa makosa yanayohusu mali haramu inayopatikana kwa njia ya uhalifu kupata nyaraka za fedha, amana za benki, mawasiliano ya elektroniki na simu, kumbukumbu za kompyuta, picha za video na kumbukumbu nyinginezo za aina hiyo.

(iv) Inapendekezwa kuwa Wapelelezi wanaolazimika kutenda vitendo vya kihalifu kwa madhumuni pekee ya kukusanya ushahidi wapatiwe kinga ya kisheria.

(v) Kwa kutambua ukweli kwamba wahalifu wanaohusika na makosa haya ya jinai ni watu wenye fedha nyingi na uwezo mkubwa na wanamiliki silaha za hatari, inapendekezwa kwamba iwe ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kuwatishia mashahidi, kuunda au kutunga uongo au kuwatishia watoaji wa haki, kama vile Majaji, Mahakimu na Waendesha Mashtaka. Inapendekezwa kwamba adhabu ya kosa hilo isipungue kifungo cha miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20. Marekebisho yanakusudia kuongeza makosa yanayohusu fedha haramu kwenye orodha ya makosa yasiyoruhusiwa kupewa dhamana. Inapendekezwa kuongeza aya katika kifungu cha tano (5) cha fungu la 148 kwa ajili hiyo. Kosa hili ni kubwa na zito kama makosa mengine yaliyoainishwa kwenye fungu hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Urejeshaji wa Wahalifu, Sura ya 368 *(The Extradition Act Cap. 368)*. Maudhui ya marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza makosa ya "ugaidi" na "usafirishaji wa fedha haramu" kwenye Jedwali lililopo kwenye Sheria hiyo.

(b) Kuzuia masharti ya fungu la 17 linalohusu utaratibu wa kurejesheana watuhumiwa wa makosa ya kisiasa kutumika katika makosa ya ugaidi na usafirishaji wa fedha haramu. Inapendekezwa kwamba watuhumiwa wa makosa hayo warejeshwe nchini kwao wakaadhibiwe hata kama watajitetea kwamba walifanya makosa ya ugaidi au usafirishaji wa fedha haramu kwa sababu za kisiasa;

(c) Inapendekezwa kuongeza katika Ibara ya 20(b) makosa yanayohusu ugaidi au usafirishaji wa fedha haramu kwenye orodha ya makosa ambayo nchi yetu inaweza kukubali, endapo itaombwa kuwarejesha nchini kwao watuhumiwa wa makosa hayo ili wakaadhibiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushirikiano na Nchi Nyingine katika Kudhibiti Vitendo vya Jinai, Sura ya 254 (*Mutual Assistance in Criminal Matters Act Cap. 254*). Marekebisho haya yanalenga kuweka kwenye Sheria hiyo fungu jipya la 32A litakaloainisha utaratibu wa kugawana mali zinazokamatwa nchini mwetu kutokana na harakati za udhibiti wa uhalifu. Inapendekezwa kwamba kuwepo na kanuni mbili:-

(a) Kanuni ya kwanza mali yoyote itakayokamatwa hapa nchini itabakia hapa nchini.

(b) Kanuni ya pili ni kwamba, pale ambapo mali hiyo inahusu nchi ambayo tumekubaliana nayo kugawana mali za uhalifu zinazotoka katika nchi hizo, basi Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatakiwa kuelekeza kiasi cha mali au thamani yake ambayo itarejeshwa kwenye nchi husika.

Kanuni hizi zinazingatia ukweli kwamba nchi huingia gharama katika kudhibiti uhalifu. Gharama hizo zinaweza kufidiwa kwa mali inayokamatwa kutaifishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Sita ya Muswada inahusu marekebisho ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha, ya mwaka 2006 kwa ajili ya kuifanya iwiane na Sheria ya *Anti-Money Laundering Act, 2006***.** Inapendekezwa kuongeza katika fungu hilo linalohusu kosa la kujihusisha na fedha haramu kuwa moja ya makosa ya jinai kwa mujibu wa Sheria za Benki na Taasisi za Fedha. Aidha, inapendekezwa katika Ibara ya 23 hadi ya 25 kwamba mtu atakayetiwa hatiani kwa makosa yanayohusu fedha haramu aondolewe sifa ya kushika madaraka katika Benki au Taasisi yoyote ya fedha.

Sehemu ya Saba ya Muswada inahusu Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya mwaka 2003. Marekebisho yanayopendekezwa yanalenga katika kuainisha mamlaka ya Kitengo cha Uchunguzi wa Fedha (*Financial Intelligence Unit, (FIU*). Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, 2006 *Anti Money Laundering Act, 2006* inaweka sharti kwa waendeshaji wa michezo ya kubahatisha kutoa taarifa zinazohusu shughuli za michezo ya kubahatisha kwa *FIU* kwa kuwa michezo hiyo inaweza kutumika kama eneo mojawapo kwa ajili ya kuendeleza makosa yaliyoanishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu (Ibara ya 26 hadi 28 za mabadiliko haya zinahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nane ya Muswada inahusu Sheria ya Makosa ya Uhujumu wa Uchumi, Sura ya 200. Inapendekezwa kufanya marekebisho katika maeneo mawili ili kuondoa katika Sheria hiyo makosa yanayohusu fedha ambayo tayari yameainishwa vizuri katika Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya mwaka 2006 ili kuondoa uwezekano wa kuwepo mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa Sheria hizo.

Mhshimiwa Naibu Spika, pia inapendekezwa kwamba tafsiri ya neno "benki" na aya ya tano ya Jedwali la Kwanza vifutwe kutoka katika Sheria hiyo kwa kuwa maudhui ya makosa hayo yameainishwa kwa uangalifu katika Sheria ya Udhibiti wa Biashara Haramu ya Fedha (Ibara ya 29 hadi 31 zinahusika).

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tisa ya Muswada huu inahusu marekebisho ya Sheria ya Ushahidi (Sura ya 6) kwa nia ya kuutambua rasmi ushahidi wa elektroniki katika Sheria ya Ushahidi. Yapo maeneo makuu matatu yanayopendekezwa kufanyiwa marekebisho katika Sheria hii. Maeneo hayo ni haya yafuatayo:-

(a) Kuhusu ushahidi unaopatikana kutokana na upelelezi wa siri, inapendekezwa kuwa Mahakama ziruhusiwe kuupokea ushahidi huu unaotokana na uchunguzi wa siri (*Survaillance*) au rekodi za mazungumzo ya simu za mikononi na njia nyingine za mawasiliano pamoja na mawasiliano baina ya wahalifu au watuhumiwa.

(b) Kuhusu kuutambua ushahidi wa kumbukumbu za kibenki zinazotunzwa kwa njia ya Elektroniki ikiwa ni pamoja na vitabu vya Benki na kumbukumbu nyingine kuwa ni ushahidi wenye hadhi sawa na ushahidi mwingine wa kumbukumbu za nyaraka, yaani *documentary evidence*.

(c) Kuruhusiwa kwa ushahidi wa kumbukumbu za elektroniki za kibenki kutolewa Mahakamani kama ushahidi mwingine wowote, ili mradi ushahidi huo uwe umepatikana katika kumbukumbu za kibenki ambazo zimetunzwa katika utaratibu wa kawaida wa kutunza kumbukumbu za Benki. Sasa hivi Benki nyingi zinatunza kumbukumbu zake kwa kompyuta na huzichapa pale zinapohitajika. Hali hii imeleta mkanganyiko wa kisheria kuhusu kumbukumbu ya awali *(Best Evidence Rule)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi ya Muswada inahusu marekebisho kwenye Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ya Mwaka 2005. Inapendekezwa kuwaondoa katika Bodi ya Utawala, Mkurugenzi wa Elimu na Mkuu wa Chuo na badala yake Mkurugenzi wa Elimu ya Ufundi ndiye awe Mjumbe wa Bodi ya Utawala. Kwa msingi huo, inapendekezwa kuwa Mkuu wa Chuo awe Katibu wa Bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kumi na Moja, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Utumishi wa Mahakama ya Mwaka 2005 kwa madhumuni ya kuiongezea Tume madaraka ya kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu. Ili kuwezesha hali hiyo, Ibara za 38 na 39 zinapendekeza kumpatia Katibu wa Tume madaraka ya kusimamia watumishi katika Tume hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Naibu Spika**,** nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala baada ya kuchambua na Kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (*the Written Laws (Miscellaneous Amendements)(No. 2*), 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Serikali, familia, ndugu na wananchi wa Jimbo la Tunduru kutokana na kifo cha Marehemu Juma Jamaldin Akukweti, aliyefariki nchini Afrika Kusini Januari, 2007. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amina!

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Mtengeti Migiro, Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Pia nawapongeza Mheshimiwa Dr. Batilda Buriani, Mbunge, Mheshimiwa Bernard Membe, Mbunge, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mbunge, na Mheshimiwa William Ngeleja, Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa Waziri na Naibu Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria zifuatazo:-

1. Sheria ya Udhibiti wa Mali inayotokana na Uhalifu, Sura ya 256;

2. Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20;

3. Sheria ya Urejeshaji wa Wahalifu, Sura ya 368;

4. Sheria ya Ushirikiano na Nchi Nyingine katika Kudhibiti Vitendo vya Jinai, Sura ya 254;

5. Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006;

6. Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya mwaka, 2004;

7. Sheria ya Makosa ya Uhujumu wa Uchumi, Sura ya 200;
8. Sheria ya Ushahidi, Sura ya Sita;

9. Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ya mwaka 2005; na

10. Sheria ya Tume ya Utumishi wa Mahakama ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilitekeleza kazi ya kuujadili Muswada huu katika kikao chake kilichofanyika katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam

tarehe 15-16 Januari, 2007 kwa kupokea maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mbunge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali akisaidiana na wataalamu wake. Aidha, Kamati ilipokea maoni ya wadau kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu yaliyowasilishwa na Bwana Harlod Sungusia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe waliotekeleza kazi hii ni hawa wafuatao:- Kwanza, Mheshimiwa Geroge Malima Lubeleje - Mwenyekiti, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Athuman S. M. Janguo, Mheshimiwa Rajab H. Juma, Mheshimiwa Shoka K. Juma, Mheshimiwa Charles N. Keenja, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Salim Y. Mohammed, Mheshimiwa Abbas Z. Mtemvu na Mheshimiwa Dr. Wilbroad P. Slaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2), Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, sasa naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu sheria nilizozitaja hapo awali kama ifuatavyo:-

Kwanza, Sheria ya Udhibiti wa Mali inayotokana na Uhalifu, Sura ya 256 *(The Proceeds of Crime Act, Cap 256).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Mali inayotokana na Uhalifu, Sura ya 256. Mapendekezo haya yanalenga kumpa mamlaka Ofisa wa Polisi wa cheo cha Mratibu Msaidizi wa Polisi kwa amri ya Inspekta Jenerali wa Polisi kufanya uchunguzi kwenye kompyuta, simu, *fax*, mawasiliano ya elektroniki, kurekodi kwa redio au video pamoja na kuangalia nyaraka zote muhimu za kisheria, Benki na biashara zinazomhusu mtuhumiwa wa makosa ya fedha haramu.

Mapendekezo haya yamewapa Polisi kuzuia akaunti ya Benki ya mtuhumiwa wa uhalifu wa fedha haramu kwa muda wa siku saba saba na kufanya uchunguzi wa akaunti hiyo.

Mapendekezo haya pia yanatoa kinga kwa mchunguzi yeyote akiwa katika uchunguzi wa makosa ya fedha haramu au yale yanayohusiana na sheria hii. Aidha, Muswada huu pia unapendekeza kufuta na kupendekeza baadhi ya tafsiri mpya zitakazokwenda na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii kwa kuwa yanalenga kupambana na vitendo vya kihalifu vinavyofanyika duniani. Uhalifu umeongezeka kwa kiwango cha kutisha na wahalifu wanatumia mbinu za kisasa. Hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kubuni mikakati hii.

Hata hivyo, pamoja na mapendekezo mazuri ya Serikali ya kuboresha sheria hii, Kamati inaona kuwa mtoa taarifa (*infomer*) hajalindwa na sheria hii. Kamati inaona kwamba watu wataogopa kutoa taarifa za kihalifu kwa kuwa hakuna kinga ya kisheria,

hasa ukizingatia kuwa wahalifu wana nguvu kubwa ya kifedha ambayo wanaweza kuitumia kuwadhuru watoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kamati inaona kuwa mamlaka waliyopewa Polisi kuzuia akaunti ya mtuhumiwa kwa muda wa siku saba kwa ajili ya kufanya uchunguzi yanaweza kutumika vibaya na kusababisha madhara ya kiuchumi na kijamii kwa mtuhumiwa. Hivyo, Kamati inashauri na kupendekeza ifuatavyo:-

(a) Watoa taarifa walindwe na sheria hii;

(b) Muda wa kuzuia akaunti ya mtuhumiwa wa uhalifu wa fedha haramu ufupishwe kuwa siku tatu badala ya saba;

(c) Kuwachukulia hatua kali za kinidhamu na kisheria kwa mtu yeyote anayetoa taarifa kwa wahalifu kuhusu vyanzo vya taarifa ili kujenga imani kwa raia wema wanaotaka kutoa taarifa za uhalifu;

(d) Kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kushirikiana na vyombo vya dola kupambana na uhalifu.

Pili, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 *(The Criminal Procedure Act, Cap 20);*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20.

Lengo la mapendekezo haya ni kuongeza makosa yanayohusu fedha haramu kwenye orodha ya makosa yasiyoruhusiwa kupewa dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo haya.

Tatu, Sheria ya Urejeshaji wa Wahalifu, Sura ya 368 *(The Extradiction Act, Cap. 368);*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Urejeshaji wa Wahalifu, Sura ya 368, kwa kuongeza makosa ya ugaidi na usafirishaji wa fedha haramu kwenye orodha ya makosa kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Muswada huu unapendekeza kuwa watuhumiwa wa ugaidi na usafirishaji wa fedha haramu warejeshwe na kuadhibiwa hata kama walifanya makosa haya kwa sababu za kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kutokana na vitendo vya kigaidi vinavyofanyika duniani ambavyo watuhumiwa hutegemea sana fedha haramu kufanikisha uhalifu wao. Mara nyingi wahalifu hushiriki

kwenye vitendo hivi kwa sababu zao binafsi na wakikamatwa hudai wanafanya hivyo eti kwa sababu za kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa adhabu kali itolewe kwa watakaopatikana na hatia kwa kuwa vitendo vyao vinahatarisha maisha ya raia, kuharibu mali na kuvunja amani.

Nne, Sheria ya Ushirikiano na Nchi Nyingine katika Kudhibiti Vitendo vya Jinai, Sura ya 254 (*The Mutual Assistance in Criminal Matters Act, Cap 254);*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoeleza mtoa hoja, Muswada huu unapendekeza kutunga kanuni zitakazoainisha utaratibu wa kugawana mali zinazokamatwa nchini mwetu kutokana na harakati za udhibiti wa uhalifu kwa kushirikana na nchi rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaunga mkono juhudi za Serikali za kupambana na uhalifu na inashauri kwamba kuwepo na utaratibu wa mtandao wa *kiintelijensia* utakaosaidia kupeana taarifa za kihalifu baina ya Tanzania na nchi nyingine.

Tano, Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 *(The Banking and Financial Institutions Act, 2006);*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza kumwondolea sifa mtu kushika madaraka katika Benki au Taasisi yoyote ya fedha kwa mtu atakayepatikana na hatia kwa makosa yanahusu fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na pendekezo hili kwa kuwa linalenga kuwadhibiti watu ambao sio waaminifu wanaofanya kazi katika Mabenki na Taasisi za fedha. Hata hivyo, inashauriwa kuwa hata Benki au Taasisi za fedha zitakazobainika na kuwa zinajihusisha au kusaidia biashara ya fedha haramu nazo zifutiwe leseni ya kuendesha shughuli za kibenki. Vilevile, mtu akipatikana na hatia hiyo azuiliwe kufanya kazi kwenye Benki au Taasisi ya fedha kwa kuwa sio mwaminifu.

Sita, Sheria ya Michezo ya Kubahatisha ya mwaka, 2004 (*The Gaming Act, 2004).* Muswada huu unapendekeza sharti la kuwataka waendeshaji wa michezo ya kubahatisha kutoa taarifa zinazohusu shughuli za michezo ya kubahatisha kwa Kitengo cha Uchunguzi wa Fedha *[Financial Intelligence Unit, (FIU)].*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Kamati inaunga mkono mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii, kwa kuwa yanalenga kudhibiti michezo ya kubahatisha ambayo wahalifu wengi wakiwemo wa fedha haramu duniani hupendelea kucheza michezo hii. Kamati inashauri kuwa *FIU* isisubiri kupelekewa taarifa na waendeshaji wa michezo hii, bali uwekwe utaratibu wa kuwakagua mara kwa mara waendeshaji wa michezo ya kubahatisha.

Saba, Sheria ya Makosa ya Uhujumu wa Uchumi, Sura ya 200 *(The Economic and Organized Crime Control Act, Cap 200).* Muswada huu unapendekeza tafsiri ya neno

"*bank*" kama linavyotafsiriwa katika Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha, 2006 na kuondoa makosa ya fedha kwenye sheria hii. Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanalenga kuondoa utata unaojitokeza kwenye sheria mbalimbali.

Nane, Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 *(The Evidence Act, Cap 6).* Sheria hii inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushahidi, Sura ya Sita. Lengo la mapendekezo haya ni kuutambua rasmi ushahidi wa elektroniki katika Sheria ya Ushahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati yangu inaunga mkono mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii. Hata hivyo, pamoja na hayo, Kamati ina wasiwasi kuwa ushahidi wa aina hii utawatia watu wengi hatiani hata kama hawatashiriki kwenye vitendo vya uhalifu.

Mathalani, ujumbe unaoingia kwenye akaunti ya mtumiaji kwa njia ya "*junk mails*," ukweli ni kwamba aliyetumiwa hakuomba atumiwe ujumbe huu. Kwa hiyo, Kamati inashauri kuwa Serikali itafute njia za kudhibiti mitandao ya *internet* kuzuia uhalifu wa aina hiyo.

Tisa, Sheria ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ya mwaka 2005 *(The Mwalimu Nyerere Memorial Academy Act, 2005);*

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unapendekeza kumwondoa Mkurugenzi wa Elimu na Mkuu wa Chuo kuwa Wajumbe wa Bodi ya Utawala. Pia, inapendekezwa kuwa Mkuu wa Chuo hiki awe Katibu wa Bodi ya Utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaunga mkono mapendekezo ya Serikali. *(Makofi)*

Kumi, Sheria ya Tume ya Utumishi wa Mahakama ya mwaka 2005 *(The Judicial Service Act, 2005).* Muswada huu unapendekeza kuipa Tume ya Utumishi wa Mahakama kuwa na uhuru wa kuajiri watumishi wengine kwa kadri inavyoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwa kuwa yanalenga kudumisha na kuboresha uhuru wa Mahakama na mgawanyo wa madaraka miongoni mwa mihimili ya dola. Kamati inashauri pia Mahakama iwezeshwe vitendea kazi kama vile Ofisi, usafiri, nyumba za watumishi, vifaa vya ofisini, na kadhalika ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi. Aidha, inashauriwa kuwa Bajeti ya Mahakama iongezwe ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii muhimu. Aidha, napenda kumshukuru na kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mbunge na wataalamu wake kwa kusaidia Kamati katika kuujadili Muswada huu. Vilevile, nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa michango yao ya kina iliyouboresha Muswada huu kufikia hatua inayoonekana.

Mwisho, nawashukuru sana makatibu wa Kamati, Ndugu Emmanuel Mpanda, Ernest Zulu na Charles Mloka, kwa kuhudumia Kamati hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. FATMA MAGHIMBI – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA :** Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia naomba niungane na wenzangu kwa kutoa pole kwa familia ya Marehemu Jamaldin Akukweti kwa kifo cha Mzee wao, ndugu yao na Kiongozi wa familia yao na jamaa wa Marehemu waliokuwamo katika ndege iliyopata ajali.

Pia, natoa pole kwa Baraza la Mawaziri kwa kumpoteza mwenzao mpenzi na mchapakazi hodari katika Baraza lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nakipa pole Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kumpoteza mwenzao. Wakristo wanasema: "Bwana ametoa na Bwana ametwaa" na Waislam tunasema "*Inna Lillah Wa-inna lillayhi Rajiun.*" Pia, napenda kuwapongeza wale wote waliopata nyadhifa mbalimbali kutoka katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa narudi kwenye Muswada ulioko mbele yetu. Kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(c) na kifungu cha 70(2) Toleo la mwaka 2004, napenda kutoa mtazamo wa Kambi ya Upinzani kuhusu marekebisho ya sheria ambazo zimo katika Muswada huu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha Tano cha Muswada kinachofanyia marekebisho ya sheria kuu kwa kufuta na kuongeza sehemu ndogo ya sehemu ya pili (*sub-title*) kukamata na kutaifisha, yaani *to forfeiture and confiscation.* Kama vifungu vinavyofuatia vinavyosema, Kambi ya Upinzani inaona hii nayo itakuwa ni ukombozi na kitu kitakacholeta heshima na uaminifu miongoni mwa Watendaji walioaminiwa na wananchi kufanya maamuzi mazito kwa niaba yao kuwa waaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa njia moja ama nyingine, ile dhana ya rushwa kubwa inaweza kuanza kupungua kama sheria itaanza kwa wale ambao tayari wanajulikana na viongozi wa juu wa nchi hii kama Mheshimiwa Rais alivyosema na kuwataka wajirekebishe. Badala ya kujirekebisha, Sheria ianzie kwao na uwe mfano wa wale wote wenye nia ya kudhalilisha nafasi zao za maamuzi. Yaani sheria ianzie iwe *retrospective.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa nane *Section 11* au *Section 31*(a) iliyoko katika *Prospect Act* ambapo inasema, naomba kunukuu: *"Where the Inspector General of Police or the Director of Criminal Investigation suspects on a reasonable grounds that any person has been involved in the commission of a serious offence, a predicate offence or money laundering he may authorise and direct a Police Officewr of the rank of Assistant Superintendent of Police or above to freeze a bank account and seize any document from that bank or financial institution for seven days during which leave of the court for continued seizure shall be obtained."*

Mheshimiwa Naibu Spika, *the word any* ni *vague* ina maana *documen*t yoyote hata ile ambayo haihusiki ili mradi tu ni ya kwake yule mtuhumiwa. Sisi Kambi ya Upinzani tunapendekeza neno "*relevant"* liongezwe mara baada ya neno "*any"* yaani isomeke '*any relevant document*".

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *section* hiyo hiyo ya 11 au *section 31*(a) katika *principle act* kuna maneno yanayosema, *The IGP,* yaani *Inspector General of Police* au *the Director of Criminal Investigation* wanaweza kumwagiza askari mwenye cheo cha *Assistant Superintendent* au cheo cha juu zaidi kwenda ku-*freeze account* ya mtuhumiwa bila kupata amri ya Mahakama, inaonesha kwamba ni *arbitrary powers to the police.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo askari anaweza kutumia mabavu. Sisi upande wa Upinzani tunapendekeza kwamba, *the law should put into mandatory,* kwamba Polisi lazima wapate *order* ya Mahakama *under certificate of urgency*. Au kifungu hicho kisomeke kama kilivyo endapo kutakuwa na *exceptional urgent cases or incidences* ambapo Afisa huyo wa Polisi ale kiapo, yaani a-*swear affidavit* kueleza uharaka wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote tunaelewa jinsi askari wanavyoweza kutumia mabavu na kuweza kumdhalilisha yule ambaye anatiliwa mashaka kwa makosa hayo na mwisho wake mara nyingi mtuhumiwa yule kuonekana hana kosa.

*Section 13* au *63(a)* kwenye *principal act* inasema, naomba tena kunukuu. *Sub section one* inasema: *"Notwithstanding the provision of any other written law, the Inspector General of Police may, where he considers that any evidence of the commission of a serious offence, predicate offence or money laundering by a person is likely to be found in a bank account kept by that person, spouse or child or any person..."*

Mheshimiwa Naibu Spika, neno "*child"* halikuwa "*defined"* popote katika sheria hii. Kama tunavyojua, katika sheria hakuna makubaliano juu ya tafsiri ya neno "*child"*. Tanzania kila kwenye neno "*child"* katika kifungu cha sheria, basi wanakuwa na tafsiri yao tofauti, yaani *every law defines a child in its own perspective*.

Kwa maana hiyo basi, sheria hii ni bora itoe maelezo ni nani "child*"*. Sheria hii ni bora iangaliwe sana. Swali la Doll Incapax, yaani *in ability to commit criminal offence by the child who is under ten years of age,* kama ilivyoelezwa ndani ya sheria ya adhabu, yaani *penal code.* Kwa ujumla, mabadiliko yanayotaka kufanywa ni muhimu sana na sisi upande wa Upinzani tunakubaliana nayo hasa kwa kuzuia *Money Laundry.*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, naomba kuwasilisha na naomba kabla sijaondoka katika kilele hiki, naomba maji yanayowekwa kule kwenye Baraza la Mawaziri, yawekwe katika Baraza la Mawaziri Vivuli pia maana sote tunaweza kupaliwa. Ahsante sana kwa kunisikilliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Maji mmeshapata. *(Kicheko)*

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza na mimi niungane na wenzangu katika kutoa rambirambi kwa familia ya Marehemu Akukweti na familia ya Marehemu wengine waliofariki kwenye ajali ya Mbeya. Vile vile, natoa pongezi kwa viongozi, Wabunge waliopata nyadhifa mbalimbali za Uwaziri na Unaibu Waziri. Lakini zaidi kwa Mheshimiwa Dr. Buriani kwa kuwa mwanamke wa pili kuwa *Chief Whip* katika Bunge la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kuchangia sehemu chache sana za Muswada huu. Lakini kabla sijaanza kuchangia naomba niseme yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunachangia Muswada wa *Money Laundering* hapa ilitahadharisha na kuomba sana Serikali kwamba Muswada huu hautakuwa na meno kwa sababu watu wataogopa, haitaletwa sheria ya kumlinda *witness*, sheria ya kumlinda mtu ambaye atatoa taarifa. Hata kama mtaleta masahihisho ya aina gani kwenye sheria hii kama *witness* hana sheria ya kumlinda, basi Muswada huu utakuwa Muswada ambao watu wataogopa kutoa taarifa kwa sababu hawana uhakika wa maisha yao.

Kwa hiyo, naomba Serikali ilete Muswada na ipitishe hapa sheria ya kumlinda mtu anayetoa taarifa juu ya *Money Laundering.* Nilisema, hawa ni watu wenye nguvu sana za kipesa na uwezo mkubwa sana wa kumnunua mtu yeyote. Sasa kama mnyonge kama mimi nikitoa taarifa na kwa sababu hakuna sheria ya kunilinda, basi maisha yangu yapo hatarini. Naiomba sana Serikali na Serikali, inajua hilo kwa sababu popote duniani unapopitisha Muswada wa *Money Laundering,* basi lazima pawepo na Muswada ambao utamlinda *witness,* sisi hatuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie kitabu cha sheria chenyewe cha *Miscellaneous Written Laws, Miscellaneous Amendment Act No.2*, ukurasa wa nane Ibara ya 11 kifungu cha 31(a). Mimi nakubaliana nacho kabisa isipokuwa niulize tu hivyo, baada ya kushika makaratasi na kufunga *bank account* kwa siku saba na halafu kuomba kibali cha Mahakama kwa muda wa siku saba; Je, kibali kisipopatikana katika muda wa siku saba, sheria mbona imenyamaza kimya, haisemi kitu?! Kwamba kama kibali cha Mahakama hakikupatikana katika muda wa siku saba, *Bank Account* zile zitafunguliwa, makaratasi yaliyokuwa *seized* na *documents* zitarudishwa ama kutatokea nini? Naomba Mheshimiwa *AG* atueleze hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo linapingana na lile la Ibara ya 13 kifungu 63(a) kinamruhusu mtu huyo huyo kushika *documents* bila ya kusema kwa muda gani. Hapa Afisa huyo anaweza kufanya hivyo *forever* kwa sababu hakuna muda. Sasa tunaomba tuelewe nini kinachomsibu hapo. Kingine ni kifungu cha 63(a)(2) na hiki kina-*apply* kila mahali. Ukisema Mahakama, una maana Mahakama gani hapa? Huyu Afisa aende akapate kibali cha Mahakama ipi? Kuna Mahakama yoyote tu aende ama kuna ngazi ya Mahakama ambayo Afisa huyu mkubwa wa Polisi anatakiwa apate kibali? Kwa hiyo, naomba maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine linahusu kifungu 63(b). Hapa Afisa vile vile anatakiwa apate kibali katika siku saba. Lakini lazima tuelewe wanaofanya kazi ya kupanga uhalifu hawazuki tu wakafanya, wanachukua muda mrefu kupanga ili waweze kutenda kitu fulani. Wana mikakati yao! Sasa kwa sababu sheria inasema ni siku saba katika kifungu hicho hicho, anaweza kukaa nacho siku saba, lakini katika siku saba hawa wahalifu ni watu wenye akili sana na wanaweza wakafanya *weekend*. *Polisi Officer* ambaye hana nafasi ya kufanya vitendo, hatapata kibali kwa sababu *weekend* Mahakama haifanyi kazi. *Holidays* Mahakama haifanyi kazi! Sio vizuri mkakifungulia kifungu hiki cha 63(b) sasa kiwe wazi ili Polisi wapate uwezo wa kuwa na meno?

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii ni nzuri, lakini marekebisho haya yanamfunga *Police officer* kuchukua hatua za dhati kabisa katika kutekeleza sheria hii. Kwa jinsi sheria hii ilivyo sasa na masahihisho haya ni kwamba *Police officer* hawezi kufanya kitu mpaka Mahakama imemwambia ndio. Lakini msisahau Mahakama zetu. Twende na hali halisi, watu wenye fedha hawa wanaweza kutawala hiyo Mahakama na Polisi asiweze kutekeleza sheria hii. Sasa tunafanya nini? Lazima tumpe nguvu Polisi. Hii habari ya siku saba lazima awe ameomba kibali, lazima awe ameapa huko Mahakamani, basi Polisi hawezi kufanya kazi kwa sheria hii na watu wenyewe wanaohusika kwenye sheria hii hawawezi kusumbuliwa na sheria hii tena, itakuwa imetengenezwa sheria nzuri imepitishwa na Bunge lakini inakuja kuzuiwa na vipengele hivi vya siku saba saba ili Polisi iweze kupata kibali kutoka Mahakamani. Mimi nadhani wenzetu mjitahidi kusahihisha hizi sheria mtuambie Polisi watafanyaje kazi *weekend* na *holidays* katika kuzuiwa kwa siku saba zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ndio ulikuwa woga wangu sana ukurasa wa nane na tisa, kwa kusema kweli Polisi wamefungwa mikono kuchukua hatua kutekeleza sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Muswada huu mzuri katika historia ya Bunge.

Awali ya yote, ningependa niungane na wenzangu walionitangulia kutoa rambirambi zangu za dhati kwa kifo cha ndugu yetu Mheshimiwa Akukweti na pia kutoa pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuwa Mawaziri pamoja na dada yetu aliyechaguliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Muswada wenyewe unachukua sheria nyingi, nisingependa kupoteza muda, nitakwenda moja kwa moja kujadili ninayoyaona mapungufu kwenye Muswada huu. Mengi nimeyatanguliza kwa maandishi ya Mwanasheria Mkuu kuhusu marekebisho haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miswada yote iliyoletwa kurekebisha Sheria ya *Money Laundering,* Sheria ya *Mutual Assistance,* Sheria ya *evidence act* na mengineyo yote yanatokana na juhudi za Umoja wa Kimataifa kupitisha azimio la mwaka 2001 baada ya

matokeo mabaya yaliyotokea kule *New York,* wale ma-*terrorist* waliobomu *towers* kule *New York.* Haya yote ni matokeo ya ujambazi wa *New York,* yamekuja kwetu wakishinikizwa kuona Mataifa makubwa kama Marekani, hakuna kigeni hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekani wamelazimisha nchi nyingi zipitishe sheria zinazofanana na kwao. Lakini mazingira ya Marekani na ya kwetu ni tofauti. Marekani wamesoma, wana vyombo vizuri vya kufanyia kazi, hapa kwetu haiwezikani kufanya hayo. Tumesukumizwa tu, lakini kwa nini tusiwe angalau *bold enough* kuchukua muda na kujadili kuona jinsi gani tunaweza ku- *localize* hizi sheria mbalimbali? Natoa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1991 Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria ambayo tunaizungumzia leo ambayo ni Sheria ya *Crime* ya mwaka 1991. Ilikuwa mwaka 1991, ikafanya marekebisho mwaka 1995 na 2001. Hiyo sheria tuliyokuwanayo haina *implement rules,* bali kwenye sheria ilikuwa haitumiki. Imekuja baada ya mwaka 2001 ndio nguvu zimetoka mpya kutoka Marekani kusema kila nchi inayofaidi kupata fedha kutoka kwa nchi tajiri zipitie sheria, zipitishe sheria zinazofanana za kwao.

Lakini ukiangalia nafasi hii, hiyo sheria ya mwaka 1999 ambayo tunaita *cap. 5 to 6* inafanana na *Antimoney Laundering Act* tuliyoirekebisha mwaka 2006. Makusudi yake yanafanana kabisa. Sheria zote mbili, ile *cap* 2, 5 to 6 inazungumza juu ya *serious crimes*. *Serious crime* maana yake ni nini? *Money laundering* maana yake ni nini? Ni wale wanaochukua fedha za haramu wanakwenda kufanya ujangili ama ujambazi ama u-*terrorism* kama ulivyofanyika kule *New York.* Sasa tunajiuliza, Je, Tanzania pamoja na mipaka yake, Tanzania na watu wake, kweli wanaweza kuielewa sheria hiyo bila ya kuwepo angalau *training* fulani?

Ukitazama hizi sheria mbili, unajiuliza, kwa nini tumeweka mbili tusichanganye ile *cap* 5 to 6 na *Antimoney Laundering* iwe sheria hii. Lakini tufanye Semina kwa Wabunge kwanza tujue maana yake ni nini, madhara yake ni nini kabla hatujaipitisha. Kama tunasema ndiyo kwa kuwa tumeambiwa na wakubwa tufanye hivyo, mimi nashangaa kabisa. Nadhani tutachukuliwa tunafanya mambo bila ya kufikiri zaidi. Ningeishauri Serikali ipitie upya tena hizi sheria mbili.

**NAIBU SPIKA:** Naomba usogee kwenye *microphone.*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Kwanza kuona maana ya *serious crime* ama *serious offence*. Kama Mmasai anachukua ng'ombe wake anawaleta pengine Dar es Salaam anauza anapata Shilingi milioni mia moja anazo mfukoni: Je, huyo Mmasai lazima aende akaripoti kwa hicho chombo kilichoundwa *under the money laundering* ajieleze amezipata wapi? Marekani hicho kitu hakipo, maana wao fedha zao ziko Benki. Sisi hapana. Fedha zetu ziko mifukoni na kwenye magodoro. Siamini kama kweli tuko *serious* na kulinda wananchi wetu kama tukianza kuwanyanyasa na mambo madogo madogo mmepata wapi fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, sheria ya ushahidi ambayo naona Muswada huu unalenga kurekebisha *Evidence Act* ya mwaka 1967. Ukiangalia Muswada ulivyokuja

wanarekebisha vifungu viwili ama vitatu tu. Lakini lengo lake ni kufanya *electronic data* ziwe *part* ya ushahidi. Sasa sisi hapa Tanzania hatuna *Information Technology Act*. Sheria ya *electronic* hatujatunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ingekuwa ni busara kwanza Serikali ilete Bungeni Muswada wa *Information Technology* halafu kuona kama kuna uwezekano wa kunyofoa vifungu vingine na kuviingiza kwenye sheria ya ushahidi. Vinginevyo, itakuwa vigumu sana sisi Wabunge hapa tunapiga kelele kila wakati mkataba uliotengenezwa ni mbaya, umetengenezwa vibaya, lakini ukienda Mahakamani, Mahakama inamwachia mhalifu kwa kuwa *Information Technology* yake hatuna hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kuingia kwenye mkataba ukipitia mtandao. Sasa hii sheria inasema kama umeandikwa kwenye *E-mail* tu na umetia *signature* yako, basi unaweza kukubaliwa Mahakamani kama ushahidi.

Lakini kuna sheria nyingine zinapinga ushahidi unaokubalika Mahakamani. Ni ule tu ambao ni *primary*. Sasa *Information Technology* ingetuambia bayana ni ushahidi gani tutaukubali na ushahidi gani hatutaukubali. Ni mapema mno kuja na marekebisho ya *Evidence Act* kwa *Section two* na kudhani unaweza kukidhi mahitaji ya *Information Technology*.

Nchi nyingine jirani zimefanya hivyo, India imefanya hivyo, Uingereza imefanya hivyo na *United Nations* imetoa *model* ya Sheria ya *Information Technology* itekelezwe na Mataifa mbalimbali ikiwemo Tanzania. Hatujafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri Muswada huu urudi nyumbani ukasubiri kwanza, tuletewe Bungeni humu Muswada wa *Information Technology,* mtaona *Antimoney Laundering* na *Process of Crime Act* zinaoana, wafanye kitu kizuri kabisa.

Tukija kwa swali la *extradition*, mimi naunga mkono kauli ya Serikali kwamba hii sheria ifanyiwe marekebisho. Nikija kwa swali la *transactions* za Kibenki, Sheria ya *Banking and Finance* inaweka bayana, ina mapungufu hapa na hapa. Lakini pia nasema tunge-*follow* ile *model* ya *United Nations* waliyotoa na tukaingiza kwenye sheria zetu ingelikuwa maana zaidi kuliko kupitisha sheria hii. Kwa sababu gani? Sisi hapa Tanzania pamoja na kuwa na *Bank Institution Act,* hatuwezi kudhibiti watu walio nje kwamba wanafanya vitendo vya kigaidi. Ingelikuwa jambo la busara zaidi kama tungeunganisha yale tuliyoambiwa na *United Nations* kwenye *resolution* iliyosema tutunge sheria ya namna hii, bila shaka tungekwenda hatua kubwa kuliko tulikofikia leo.

Kwa machache haya, nasema naunga mkono hoja hii, lakini kwanza wafanye marekebisho, walete Bungeni. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo Muswada uliopo mbele yetu. Lakini kabla sijachangia, niungane na wenzangu kutoa rambirambi zangu za dhati na za wananchi wa

Karatu kwa msiba mkubwa wa mpendwa wetu Mheshimiwa Akukweti ambaye wote tulifanya kazi naye na wengine tumefanya naye miaka kumi, kwa kweli msiba ni mkubwa. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amin.

Napenda niungane na wenzangu pia katika kutoa pongezi kwa wote walioteuliwa na kwa ajili ya muda, naomba niishie tu kwamba wote naomba niwape pongezi kuanzia Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro pamoja na Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri pamoja na Makatibu Wakuu walioteuliwa katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kwa ajili ya kipengele kimoja tu katika muswada huu. Kwa kiwango fulani Mheshimiwa Nimrod Mkono amenisaidia. Nilitaka kuzungumzia kinachohusu Marekebisho ya Sheria ya Ushahidi *(Amendment of the Evidence Act).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati iliyochambua Muswada huu, niliyasema haya katika Kamati na utadhani niliyoyasema yalisikilizwa na nikaletewa na ninaomba nichukue nafasi hii kukuomba pia kwamba wakati ukifika ninaomba ninukuu *document* kwa sababu ni ushahidi wa wazi kwa sheria hii, tusipokuwa waangalifu kama alivyotuambia Mheshimiwa Nimrod, tutafunga Watanzania wengi sana. Wabunge tusipokuwa waangalifu na mara nyingi usipopata *experience,* hutajua madhara ya sheria. Lakini ukipata *experience* ya tukio baya la sheria, utaelewa maana yake nini. Nami naommba nitangaze tena kama nilivyofanya safari nyingine, mimi nina *experience* jinsi Sheria inavyoweza kukuathiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilieleza kwamba gari langu lilikamatwa mwaka 1992 kwa dawa za kulevya bila mimi kuhusika. Limekodishwa. Mimi sikupelekwa Mahakamani wala Kampuni iliyokodisha haikupelekwa Mahakamani na Polisi walijua dawa hizo zilitoka wapi toka mwanzo tangu zinapakiwa, lakini mimi ndiye niliyeathirika na Sheria inazungumzia *for feature* ya gari hilo. Sasa Sheria tunayopokea sasa ni kupokea katika sheria zetu tukubali ushahidi wa *electronic data* Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 26 nimepokea *document* katika *E-mail Account* yangu na naomba niinukuu, sehemu yake ni ndefu, sitaweza kuinukuu kwa ajili ya muda, lakini ninukuu sehemu yake. Inasema hivi: *"From Hassan Abudul* (abudul_hassan7@hotmail.com. *Subject -From the Desk of Dr. Abudul tarehe Friday, 26 January,2007; 11:02:11 +000."* Wanaojua mtandao, huo ni utaratibu wa kawaida. Sasa inasemaje?

"*From the Desk of Dr*. Abudul Hassan, *Manager Bill and Exchange Unit, Bank of Africa,(BOA),* Ouagadougou Burkina Faso.

*Dear Friend,*

*I am Mohamed Hassan, the Bill and Exchange Manager at the Foreign Remittance Department of Bank of Africa. I got your contact from the internet while searching for an honest and trust worthy person, who will assist me to implement this*

*transfer.* (Nashukuru kwamba kwenye internet wananitambua kwamba ni *honest* na *trust worthy).*

*I discovered the some of the sum of twenty five million and five hundred thousand United States Dollars belonging to a deceased customer of this Bank. The fund has been lying without anybody coming to put claiming over the since money since the Account owner late Mr. Salla Khatif who was involved in the December 25th, 2003 Benin plane crash here is the air crash website."* (Akatoa na *Website* ambayo ilionyesha ndege). Sasa kwa kuwa ni ndefu sitaisoma lakini msingi ni nini? Msingi ni kwamba ananiomba mimi nijitokeze kwamba mimi ni *next of kin,* yaani ni ndugu wa karibu wa huyu Bwana Salla Khatif na bahati mbaya jina linakaribiana na langu. Akaendelea kusema kwamba iwapo utakubali kusaidiana wewe na mimi, wewe utapata asilimia 40 ya hizo fedha na mimi kutokana na fedha hizo nitastahili kupata asilimia 55 (yeye Afisa wa Benki ambayo inajiita *Bank of Africa).* Sasa mimi nitakayejitokeza ni asilimia 40 ya dola milioni 25. Akaendelea kwamba, atatoa asilimia tano ya fedha hizo kwa ajili ya *expenses*.

*"If the money is transferred to your account from Bank of Africa I and my family in this transaction will proceed immediately to your country for our own share of the money. I expected you to keep this business strictly confidential and secret as you may wish to know that I am Bank official. Be rest assured that this business is 100 percent risk free on both side and every arrangement to transfer this money to the account you are on going to provide have been concluded provided we maintain the confidentiality and secrecy involved. Your Faithfully* Abudul.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwanini nilishtushwa sana na hii? Nimeshitushwa sana na hii kwa sababu Kifungu cha 63 (b) cha Marekebisho ya Sheria yetu ya Jinai ukurasa wa 29 wa Muswada wenu kinamruhusu Afisa wa Polisi kuja kukagua *computer data system network and services* wakati wowote. Kwa hiyo, akaunti zenu wale wanaotumia *internet* wakati wowote Afisa wa Polisi anaweza akaingia akaja kukagua *internet service* yako kwa mujibu wa sheria hii na baada ya kukaguliwa kifungu cha *Evidence Act* kinaruhusu ushahidi utakaopatikana utumike Mahakamani. Ndugu yangu wewe huna habari vijana wetu wengi sasa hivi kwenye *internet cafe* wanafungua *website* wanaingia kwenye *E-mail* zao wanakuta kishawishi cha namna hiyo, wana-*transfer* fedha.

Nina taarifa Norway zimekuwa *transferred* mabilioni ya fedha kwa mtindo huu na ninamfahamu kijana Mtanzania aliyehusika katika kuchukua fedha kwa mtindo huu. Kwa hiyo, nakubali kwamba ni kweli hiki kitu kinaweza kikafanyika kwa sababu ni *syndicate* ya Maofisa ndani ya Benki. Inawezekana hili jina lake wala sio sahihi. Lakini ni Afisa mwenye *access* kwenye Benki, lakini Mtanzania akaingia bila ya yeye kujua, lakini na *network* ya *Interpol* au nani wakagundua wakaenda kumfuata kabla hata yeye hajakubaliana na utaratibu huu. Ikikutwa pale, yeye ataingizwa kwenye ushahidi kwamba ni mshiriki wa *money laundering*.

Anachosema Mheshimiwa Mkono, katika kuweka sheria kabla ya hatujaweka mfumo wa sheria wa kudhibi mambo ya namna hii katika nchi yetu, tuna Watanzania wengi sana ambao wamefurahia mtandao, wanapenda kuutumia, wanapata *information*

kama hizi, lakini hawajui namna ya kuzi-*control*, namna ya ku-*monitor* na kipi ni cha kweli na kipi ambacho sio cha kweli.

Nilitaka kushauri kama nilivyoshauri kwenye Kamati. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu na Mheshimiwa Waziri watuhakikishie sheria hii kama itapita na mimi nadhani sheria ipite kwa sababu ushahidi pia tunauhitaji. Wanaopitisha fedha haramu pia hatuwataki nchi hii. Kwa hiyo sheria itumike Mahakamani itusaidie kuwakamata wale wahalifu, lakini wakati huo huo tuna *safety valve* zipi zitakazosaidia watu wetu wasije wakaingizwa katika makosa ambayo sio ya kujitengenezea au yakutaka au kukubali wao wenyewe. Najua hatimaye mtaingia kwenye Sheria, mtaingia kwenye *Mainslair Actesuleous* na kadhalika lakini wakati mmeshakamatwa wewe unahangaishwa kule, umeshapelekwa ndani, haya mengine hayana nafasi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, gari langu limekamatwa kwa zaidi ya miaka nane, nimekuja kulitoa mwaka 1999 kwa sababu sheria ndivyo inavyosema. Mimi siko Mahakamani, sina mahali pa kujitetea, wala siwezi kusema, lakini gari halikufanya biashara wala halikwenda kuleta ile dawa kule ilikotoka. Nashukuru waliohusika baadaye sheria ilichukua mkondo wake.

Kwa hiyo, ninachopenda mimi kusisitiza katika hili ni kwamba tuwe waangarifu tunapotengeneza sheria. Tunaweza kuwa tunatafuta kitu ambacho kweli kina mantiki, lakini kikawaingiza wasiohusika, kama mtego wa paka na panya wakakamatwa wasiohusika wengi zaidi kuliko tunavyopanga.

Sisi leo tunataka mtandao tunaingia kwenye *Information Technology* inatuunganisha kwenye ulimwengu ambao ni wa utatandawazi. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tunali-*encourage* sana, tuna-*encourage* na vijana wetu. Lakini hatuna Sheria inayotusaidia kudhibiti vitu hivi. Kila anayetumia mtandao ameona kitu kinaitwa *Junk Mail,* ameona kitu kinaitwa *Spam,* unafanya kazi yako ghafla mezani kwako kinaingia kitu ambacho hukukitegemea na mengi ni aibu hata mtu mwenye heshima huwezi kutamani kukiangalia, lakini kiko kimedondoka pale kimetoka.

Tunafanya nini kudhibiti haya? Tuna-*system* gani ya kudhibiti na kuchuja kama nchi za wenzetu zinavyojaribu kuchuja? Hatujajiwekea mfumo, hatujajiwekea *system,* lakini tumeleta sheria ile moja tu ambayo tunataka iweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, mimi sina ugomvi sana na kupata ushahidi Mahakamani, lakini hiyo inapanuka pia kwenye kifungu cha (b) tunazungumzia suala la *Audio*, suala la *video recording*. Siku hizi kuna vitu ambavyo viko *scientifically mounted.*

Unapopata *scientifically mounted* hata *video* inaweza ikatengenezwa kwa kuunganishwa *scene* moja mbili na tatu, ukaenda kukamata watu. Una nini cha kudhibiti hapo? Uka *produce* Mahakamani *video* imetengenezwa ukasema hii *video* ndiyo ushahidi wa kilichofanyika au Mkutano mliofanya siku fulani? Tuna nini cha kudhibiti hiki? Kwa hapa sasa tuna-*prove* hii *video* kweli ni *scientifically mounted* au sio *scientifically*

*mounted,* sina Kiswahili kizuri cha *scientifically mounted,* nadhani ni *simulated* lakini *simulated* bado ni Kiingereza. Sasa sina hakika Kiswahili kizuri ni kipi.

Kwa hiyo, bado tuna matatizo makubwa na vipengele hivi. Tunaingia kwenye karne ya Sayansi na Teknolojia, tusiingie kichwa kichwa, tuingie pia na tupanue pia maeneo yote yanayohusika ili nchi yetu kweli tuingie kwenye *science* na *technology* lakini tuwe na mfumo utakaolinda Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana hasa hizi *E-mail* zinazoleta mamilioni na mamilioni kutoka Ouagadougou zinakuwa nyingi sana na zinawachanganya watu. Kwa hiyo, nadhani taarifa hiyo wengi muipokee. Naendelea Mheshimiwa Shellukindo.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mchango kidogo, lakini kabla sijafanya hivyo, naomba uniruhusu nitoe pole zangu za dhati kabisa kwa familia ya Marehemu Juma Jamadin Akukweti kwa msiba mkubwa huu. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Vilevile napenda nichukue nafasi hii niwapongeze wenzetu Waheshimiwa Wabunge walioupata uteuzi mbalimbali Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migoro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Mheshimiwa Bernard Membe kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Mheshimiwa Batilda Burian kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu.

Vilevile napenda kuwapongeza Mheshimiwa Gaudence Kayombo kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mipango Uchumi na Uwezeshaji na kijana wajina wangu William Ngeleja kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Napenda kumpongeza na kwa kawaida, hili jina la William lina miiko yake na yeye anaielewa na mara nyingi wale akina William tuko wanne humu ndani, huwa tunapiga picha. Kwa hiyo, tunakupongeza kabisa. Lakini napenda kupongeza zaidi kwa hatua uliyoichukua kwa haraka ya kukanusha kwamba wewe sio Daktari. Aliandikwa kwenye Gazeti akaitwa Dr. William Ngeleja, haraka sana akasema mimi sio Daktari. Wengine wangenyamaza tu, halafu wangetupa taabu ya kuanza kuuliza, umepata wapi, lakini ametusaidia sana. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni mdogo tu katika maeneo machache. Kwanza napenda sana kumpongeza Mwanasheria Mkuu kwa kuleta marekebisho ya sheria kumi kwa mara moja, mimi nadhani ameanza vizuri na mimi namshauri akae chini achunguze sheria zote, kuna sheria nyingine zinaleta matatizo kwenye utekelezaji ndio tunasema hii imepitwa na wakati. Kwa hiyo, atuletee ikiwekezekana hizo Sheria nyingine zirekebishwe ili utekelezaji uwe mzuri zaidi. Ziko Sheria nyingi sana hata za mashirika ya umma, ziko nyingi tu ambazo ni za siku nyingi sana. Kwa mfano nyingine ni za mwaka 1969, sasa hivi tuko kwenye utandawazi ,wakati zinatungwa hazikuzingatia mazingira ya namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa kwanza ni katika Muswada wa Sheria ya Mapato yanayotokana na vitendo vya uhalifu sura ya 256. Hapa napenda vilevile kupongeza kwa kuondoa maneno ambayo yana utata. Kuna Sheria mbalimbali zimeandikwa mambo ambayo kiutekelezaji ina matatizo. Kwa mfano hii aliyoondoa *as soon as practicable,* ni miaka mingapi? Kwa hiyo, nashukuru kwamba sasa anaweka muda halisi katika kifungu kile cha tisa ukurasa wa saba ya kuweka muda halisi kwa kuondoa maneno; kwa mfano ukisema haraka sana, mapema iwezekenavyo huleta utata katika utekelezaji na ndiyo mianya ya rushwa hiyo. Kwa hiyo, sheria zote zile ambazo zina vipengele vya mapema iwezekanavyo, haraka, mara moja, havitoi mwelekeo wowote kwamba hapa kuna utekelezaji halisi.

Kwa hiyo, mimi naunga mkono sana hatua hii. Nadhani ni mwanzo mzuri. Sheria zote zitizamwe. Vifungu ambavyo vinatoa mwanya ambao hauna mwelekeo, inabidi watu wadai na hapo kuingia kishawishi kwamba hapa nadhani natakiwa nitoe chochote, kumbe ni sheria yenyewe tu ilivyowekwa. Ukimwambia mapema iwezekanavyo inaweza kuwa mwaka mzima, inaweza kuwa baada ya siku ishirini, ni mara moja. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa hatua aliyoichukua Mheshimiwa Waziri.

Nimeangalia vilevile kifungu cha 17 cha Sheria hiyo ya Mapato yanayotokana na vitendo vya uhalifu. Kifungu cha 17(c) ukurasa wa 11 hapa pamewekwa kifungo kwa mtu ambaye ataingilia shughuli za Majaji, Mahakimu, Waendesha Mashtaka, atafungwa miaka mitano. Sasa Magereza haya yamejaa, mimi nadhani tuweke nafasi ya kuweka faini. Faini ziwe kubwa zaidi. Mtu anaingilia shughuli za Jaji, za Mahakimu, Waendesha Mashtaka, basi apigwe faini kubwa zaidi. Hivi vifungo tuviangalie kwenye mambo ambayo hawa majambazi wanaopiga watu nyundo na nini wacha waende jela, lakini hawa kwa sababu wana fedha wapigwe faini.

Kwa hiyo, mimi nadhani tusiweke kifungo tu, Magereza yamejaa, hakuna nafasi. Kwa hiyo, tusitunge sheria ambazo zinaweza zikaongeza watu kwenda Magerezani, tujaribu kutunga ambazo zinapunguza zinazoweka udhibiti wa uhalifu. Haya ndiyo maoni yangu mimi kwenye kifungu hicho cha 17 cha Sheria hii ya Mapato yanayotokana na uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 Kifungu cha 26 kifungu kidogo (b) Ukurasa wa 13 wa Muswada huu kuzuia mtu ambaye amehusika na makosa ya fedha haramu kushika nafasi ya uongozi katika Mabenki na Taasisi za Fedha.

Hapa nilikuwa na wasiwasi kidogo, nikasema unaanzia wapi? Ambaye anaomba kazi sasa au hata wale ambao walipata kazi mwaka juzi lakini walihusika siku zilizopita na makosa hayo. Nadhani tungeweka *cut off point,* ni lini inaanza. Tunapofanya marekebisho haya au hata hao ambao wana makosa ya siku zilizopita nao watahusika? Ili iwe wazi kabisa. Kuna uwezekano kwamba siku zilizopita kwa sababu watu hawafuati, hakuna kumbukumbu zinazowekwa za mitandao na nini kuweza kujua wasifu wa mtu kwa mara moja, wengine wanahusika na makosa pengine hawakuwa wanafanya kazi hapa nchini, pengine walikuwa wanafanya kazi nje, pengine kwa ajili wamefanya makosa

ya kuingia kwenye uhalifu wa namna hiyo, nadhani tungekuwa wazi zaidi. Zuio hilo linaanza lini? Kwa anayeanza kesho au aliyeanza jana na juzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena kumshukuru sana Mwanasheria Mkuu kwa kutuletea mabadiliko haya na nazidi kusisitiza kwamba tunahitaji kwa kweli kwa Serikali kuwa na programu ya kurekebisha sheria, *Legislative Programme* ili na sisi tujiandae tujue katika kipindi kijacho hiki katika labda cha mwaka mmoja tutahitajika kuangalia Sheria zifuatazo ili na sisi tuzifuatilie utekelezaji wake na tuweze kuzichangia vizuri katika kuzirekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON GEORGE MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa mchangiaji wa mwisho, naomba uniruhusu nigusie maeneo mawili tu katika Muswada huu wa marekebisho ya sheria mbalimbali. Nianze na Sheria ya Mapato yatokanayo na vitendo vya uhalifu ukurasa wa tisa wa Muswada huu.

Tumeambiwa kwamba katika kupambana na makosa makubwa ya jinai kama vile biashara ya fedha haramu, biashara ya madawa na kadhalika, basi Muswada huu unapendekeza kiongezwe kifungu kilicho ukurasa huu wa tisa 63(b) ambacho kinataka Afisa wa Polisi wa cheo cha *ASP (Assosiated of Police)* na juu yake aweze kuingilia mtandao na nyaraka za kompyuta za mtuhumiwa ukurasa wa kumi, kuna madaraka zaidi aweze kunasa kwa *video,* matendo ya mwenendo ya mtuhumiwa aweze vilevile kunasa mazungumzo ya mtuhumiwa kwa *tape recorder* au vinasa sauti vingine na vilevile aweze kupata nyaraka zozote za uwakili na za kibenki za mtuhumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraka haya katika kipengele hiki yatatekelezwa na huyo Afisa, lakini kwa kibali cha Mkuu wa Jeshi la Polisi *(IGP)* na Mkuu wa Upelelezi *(TSI)*. Lakini hatimaye lazima apate ridhaa ya Mahakama.

Sasa ziko tetesi kuwa kutokana na changamoto kubwa inayotukabili sasa hivi ya makosa haya ya jinai kuwa yanaongeza na ile nia yetu sisi kupambana nayo vizuri, Mahakama inaonekana kwamba inaweza kuwa kikwazo iwekwe pembeni Polisi tuwape *open check* ya kuweza kufanya wanalolitaka lakini bila kupitia Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani tuwe wa kweli. Haya ni madaraka makubwa kweli kweli tunayojaribu kuyaleta kwenye sheria. *Process of Claim Act* ni madaraka makubwa ambayo yanagusa haki za msingi za kikatiba zilizomo katika Katiba yetu. Kwa hiyo, umuhimu wa Mahakama kuwepo bado upo palepale, ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine twende mara moja kwenye Ibara ya 16 ya Katiba yetu, kwa ruhusa yako nitainukuu kidogo. Katiba yetu inasema: “Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi.” Sasa hii sheria, watu mjiandae. Tunaruhusu kwamba kakitu kadogo, sikuhizi hawatumii ma-*tape recorder* au *Camera* kubwa, kanakuwa tu kama kifungo,

kanawekwa chumbani kwako. Ndugu yangu Rished umelala pale unafikiri uko huonekani kumbe unaangaliwa *Central Police* unafikia kwenye faragha. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, hii nataka tu niwaeleze kwamba haya ni madaraka makubwa mno tunayoyatoa na yanagusa haki za binadamu za msingi, lakini kama tunavyosema, kila haki ina mipaka yake na mipaka imewekwa na Katiba yetu hii. Ibara ya 16(2) inaeleza hiyo, kwamba mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali na kiasi ambacho haki ya mtu ya faragha na usalama wake yanaweza kuingiliwa bila kuathiri Ibara hiyo ya 16. Sasa swali linalokuja hapa ni; Je, ni nani mwenye uwezo wa kupima huko kuingiliwa muafaka, yaani kupima kiasi muafaka cha kuingiliwa kwa hiyo haki?

Lakini Katiba yetu ndio inayotoa jibu hilo vilevile katika Ibara ya Nne. Uukisoma yote utapata ujumbe kwamba ni Mahakama. Hata ukiangalia Ibara ya 30 ambayo pia inaweka mipaka ya uhuru wetu huu wa faragha na unasema uhuru wowote na haki zote ndani ya Katiba hii havitatumiwa na mtu mmoja kuweza pengine kuathiri kukatiza maslahi ya umma na ya watu wengine. Kwa hiyo, hii ni mipaka.

Lakini swali linakuja vilevile kwamba, nani mwenye madaraka na uwezo wa kupima kwamba sasa utumiaji wa haki fulani katika Katiba sasa umeanza kugusa maslahi ya umma? Hakuna chombo kingine, ni Mahakama peke yake! Kwa hiyo, mimi naona umuhimu mkubwa wa kuweza ku-*retain* Mahakama katika hii *process*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuko kwenye utawala wa Sheria na utawala wa sheria unategemea kabisa kwamba mfumo wetu uwe na *cheques and balances*. Sasa kuweko Mahakama pale, ndizo *cheques and balances* hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka miaka kadhaa wakati mimi sioti hata kuja hapa Bungeni, Mbunge mmoja anaitwa Msigalo, aliwahi kutoa mfano mmoja haujawahi kunitoka kichwani, akisema, kwa ruhusa yako, naomba ninukuu; "Alikuwepo mtu mmoja alikuwa anajua kutengeneza pingu, lakini pingu zenyewe akawa anazi-*improve* mara kwa mara, akafikia mahali akasema pingu nzuri sana. Akasifiwa sana. Sasa kichwa kikawa kikubwa, akaendelea kutengeneza pingu ambazo hata uwe na lile koleo kubwa huwezi kuzikata. Akasifiwa sana. Siku moja yeye akakamatwa akafungiwa hizo pingu, lakini aliona kama ameonewa, akapata fursa ya kutoroka. Sasa wafungwa wenzake wanamwambia sasa wewe ndio uliyetengeneza, tusaidie kidogo tufungue hizi, akabakia kulia tu."

Waheshimiwa Wabunge, haki tulizonazo ndani ya Katiba hii ni haki za msingi kwelikweli, tusijaribu hata kuziweka pembeni kwa matakwa ya haraka haraka. Sawa, tuna changamoto, lakini changamoto isi-*undermine* misingi ya haki katika Katiba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kitu kimoja tu; Sheria ya Ushahidi. Ni kweli kuwa Sheria yetu ya Ushahidi imepitwa na wakati, ni ya siku nyingi, ya mwaka 1967 na vipengele tulivyovichukua hivyo vingi vilikuwa wala havioti kwamba dunia hii itaweza kuwa na Televisheni hata Kompyuta. Kwa hiyo, mabadiliko yanahitajika, lakini isiwe kwa kasi sana kama wenzangu walivyokwishaongea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina tatizo kubwa sana kuhusu mabadiliko yanayopendekezwa kuruhusu kumbukumbu za elektroniki za kibenki kutambuliwa rasmi kama kumbukumbu. Hilo halinipi taabu. Linalonipa taabu ni kifungu cha cha 40(a).

Mheshimiwa Naibu Spika, hiki kifungu kinataka ushahidi wa *video*, ushahidi wa kumbukumbu nyingine za elektroniki zikubalike kama ushahidi kwenye kesi za jinai. Hapo nasema, hapana, tusiende haraka sana. Napendekeza kwamba ushahidi wa aina hiyo ukubaliwe, lakini lazima uwe *collaborated,* sijui kwa Kiswahili. Yaani uandamane na ushahidi mwingine. Tuukubali kama *secondary evidence*, lakini lazima ushahidi mwingine uwepo kuweza mtu kuhukumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu mbili kubwa.- Kwanza, teknolojia ya elektroniki kama alivyoeleza Mheshimiwa Wilbrod Slaa, ni rahisi sana kuichezea. Kuna mbinu wanaita *superimposition, imaging*. Inaweza kutolewa hapa kichwa changu, kikapachikwa kichwa cha kaka yangu Dr. Sigonda pale, kesho ukasingiziwa ni wewe ulionekana sehemu ile. Kwa hiyo, bado hatujajenga sisi wenyewe teknolojia ya ndani ya kuweza kutambua aina hiyo ya udanganyifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili; hili ni eneo nyeti sana la sheria za jinai ambalo kiwango cha uthibitisho *(standard proof)* wa kwamba mtu amekosea, kiko juu mno na ndiyo sheria yetu ilivyojipanga pale, kiko juu sana! Kuweza kuthibitisha mtu kwamba ametenda kosa la jinai, lazima uthibitishe kukidhi wasiwasi wote, kuvuka wasiwasi wowote, wanasema *beyond reasonable doubt*. Sasa huu ushahidi wa elektroniki sidhani kama unaweza ukasema kweli unaweza kuthibitisha kitu *beyond reasonable doubt*. Hii yote ni kwa sababu ya athari au ya hatma ya mtuhumiwa katika kesi ya jinai, anafungwa. Kufungwa maana yake unapoteza uhuru wako. Jela sio mahali pazuri sana. Sasa hii ndiyo maana tunahakikisha kwamba kwa kweli kwenye sheria za jinai bado tuwe weaangalifu sana kuweza kukubali ushahidi ambao utawaingiza wengi hata wasiohusika, hata wasio na hatia katika hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, tuukubali ushahidi huo *as secondary evidence* ambao lazima uwe *collaborated*. Tunamwomba sana!

Kwanza nafikiri tuna umuhimu wa kujenga uwezo wa ndani kuweza kugundua hii michezo ambayo wenzetu sasa hivi wameanza kucheza, tukitolea mifano mingi sana hapa, ndipo tuweze kuingia kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo machache, naomba niunge mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante! Kama nilivyosema, huyu ndiye msemaji wa mwisho niliyekuwa naye katika orodha yangu. Kwa hiyo, sina namna isipokuwa kumwita Naibu Waziri wa Katiba na Sheria ili aanze kujibu hoja.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kidogo hoja ya Mwanasheria

Mkuu wa Serikali. Lakini, kabla sijafanya hivyo, nami kama wenzangu, nichukue nafasi hii kutoa rambirambi zangu na za wananchi wa Jimbo la Uchaguzi la Nachingwea kwa msiba wa jirani yetu, mtani wetu Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti na wengine wote ambao walifariki katika ajali ile.

Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza ndugu zetu ambao wameteuliwa katika nyadhifa mbalimbali pamoja na Mheshimiwa Dr. Asha-Rose M. Migiro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitangulie kwa kusema kwamba naunga mkono hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mia kwa mia na niseme pia kwamba hoja hii imechelewa kidogo, ilikuwa ije mapema zaidi. Mabadiliko haya ya sheria tulikuwa tunayasubiri kwa muda mrefu, sasa tunashukuru yamefika na nitaomba Waheshimiwa Wabunge waipitishe sheria hii ili tuanze kuzitumia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie hoja mbili zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Moja, ni hii ambayo inaonyesha wasiwasi kwamba pengine sheria hizi sio zetu, tumelazimishiwa tu, zimetoka Marekani na kadhalika. Ukweli ni kwamba, *nature* ya *crimes* hizi ni *International*. Kwa hiyo kufanana kwa sheria hii au kutokea kwamba zinatungwa kwa wakati mmoja baada ya vitendo fulani vilivyotokea kimataifa, ni kitu kinachoeleweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sio sahihi kusema kwamba eti tumeziiga au tumelazimishwa, hapana! Ugomvi wa Marekani tumeona na Waarabu, tumepigwa mabomu sisi Dar es salaam. Kwa hiyo huwezi ukasema kutunga kwetu sisi ni kwa sababu tunaiga tu. Hapana! Zinatu-*affect* kwa sababu nature ya *crimes* hizi zote; *money laundering, terrorism, nature* yake ni *International*. Kwa hiyo, naomba tujue kabisa sheria hizi tunazitunga kwa sababu tunazihitaji kutokana na hali yetu halisi ilivyo katika jamii ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze kuhusu wasiwasi walioonyesha Waheshimiwa Wabunge kwamba kweli hatuna sheria ya *ICT*. Labda niwataarifu tu kwamba Tume ya Kurekebisha Sheria mwaka 2006 iliwasilisha kwa Waziri wa Katiba na Sheria utafiti waliofanya kuhusu uanzishwaji wa sheria za *ICT* na *Cyber Crimes*. Hivi sasa ripoti hiyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaifanyia kazi na tunategemea muda sio mrefu italetwa humu ndani ili ipitishwe kama sheria.

Lakini hii tunayofanya sasa, *actually* tunafuata nyuma ya Mahakama. Katika Mahakama ya Rufaa, ushahidi wa hii teknolojia ya sasa ulikubaliwa katika kesi iliyoamuliwa na Jaji Nsekela Mahakama ya Rufaa, kwamba ushahidi huu wa kutumia *video*, kutumia *computer* uruhusiwe. Kwa hiyo, Mahakama iko mbele tayari. Tunachofanya sisi ni kuja nyuma ya Mahakama na kuleta sheria sasa ieleweke vizuri zaidi. Kwa upande huo, hicho ndicho tunachokifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, kuhusu *Cyber Crimes* 66 na *ICT* kwa ujumla, tunataka kuleta sheria na tutaileta katika Bunge lako Tukufu ili sasa tuweke misingi ya *crimes* nyingine. Lakini hizi za ushahidi, kukubali ushahidi ambao ni wa teknolojia hii

ya kisasa, hili lilishaamuliwa na Mahakama ya Rufaa. Kwa hiyo, ni kama moja ya sheria zetu hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko alilolizungumzia Mheshimiwa Dr. Slaa, kuhusu mbinu zinazotumiwa sasa hivi za kuletewa *message* katika kompyuta zetu katika akaunti zetu za *Internet*. Ni kweli inatokea na hizi zinafanywa na *International Criminals* hawa hasa wa *West Africa* huko ambao wana tabia ya kuleta, halafu wewe ukishapeleka sasa anuani yako na *Bank Account* yako, ukiamka kesho, hamna kitu katika Akaunti wameishakufuta, wamekufanya maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunachosema, unapokwenda Mahakamani, kwanza hizi *crimes* zitakuwa zimekuwa *investigated* na ile *Financial Intelligence Unit* yetu ambayo tumeiunda chini ya Sheria ya *Money Laundering*. Wale watakuwa wameshafanya kazi na utakapokwenda Mahakamani kama alivyoomba Mheshimiwa Mwakyembe na kusema kwamba ile *standard* ya *proof* ni *very high*, ni *beyond reasonable doubt* na ndiyo maana tunakwenda pale Mahakamani na *standard* hiyo.

Kwa hiyo, haiwezekani waka-*superimpose* tu mambo yakaenda pale, ukadhani yatapita tu! Yatakuwa *challenged* na *proof* yake kama alivyosema ni *very strict* na *standard* ni *very high*. Kwa hiyo, tunategemea kwamba Mahakama itakapoamua, itakuwa kwanza imetumia utaalam huu uliofanywa na hawa watu wa *FIU* na pia wale *Advocates* watakuwa wame-*argue case* vizuri na ushahidi utakuwa umekuwa *proven beyond reasonable doubt 100%.* Kwa hiyo, haiwezekani kwa sababu tu ni teknolojia mpya, basi watu wakaenda na ushahidi wakadanganya danganya wakadhani utapita tu kwa urahisi. Hapana, haitatokea hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwaondoe tu wasiwasi kwamba ushahidi utakapokwenda Mahakamani utapekuliwa vizuri, hata hizo teknolojia za ku-*superimpose* Mahakama nayo inazijua. Kwa hiyo, *proof* lazima iwe ya kikweli kweli, tusiwe na wasiwasi sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli sheria hii muipitishe mkiwa na uhakika kabisa kwamba watu ambao watakuwa wanaitumia pale Mahakamani wanazijua hizi *ICT* kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwondoe wasiwasi pia Mheshimiwa Dr. Mwakyembe kuhusu uvunjaji huu wa Katiba. Lakini akiangalia vizuri kifungu kile cha 63(b) kinasema wazi kabisa kwamba *with leave of the Court*. Hakuna Polisi atakayeruhusiwa kwenda kuweka mitego, kwenda kuweka *Camera* hivi hivi tu, kuna *with leave of the Court*. *Court* ikishatoa kibali hicho, basi hapo sasa ndiyo watakuja kuchungulia ile *private life* yetu. Lakini vinginevyo, sio Polisi tu peke yake aamke aseme anaweza kufanya kitu kama hicho. Hiyo haitawezekana. Kwa hiyo, baado tunafuata kabisa misingi ile ya Katiba kwamba ni Mahakama tu inaweza kuturuhusu kufanya vitu kama hivi, kuingilia uhuru wa mtu na faragha ya mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema sikukusudia kuyasema mengi. Lakini nilikuja kuunga mkono hoja hii na ninaiunga mkono kama ilivyoletwa hoja ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nianze kwa kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mbunge wa Mpwampwa na Mwenyekiti mahiri wa Kamati makini ya Katiba na Sheria kwa maoni aliyoyatoa kwa niaba ya Kamati yake kuhusu Muswada huu. Pia, naomba kupitia kwake kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yake kwa maoni waliyoyatoa. Kwa kweli maoni haya mazuri niliyatarajia kutokana na ushrikiano mzuri walionipa Wajumbe. Maoni na nasaha zao zimenisaidia sana katika kuboresha Muswada huu. Naamini Mwenyekiti na Wajumbe wake hawatakifunika kisima chao cha busara, bali wataendelea kuturuhusu tuendelee kukichota kwa manufaa ya Bunge hili Tukufu pamoja na wananchi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwatambua kwa majina Wabunge wote waliochangia Muswada wetu huu moja kwa moja hapa Bungeni kwa maandishi au hata kwa kunitonya sikio. Wabunge waliochangia moja kwa moja hapa Bungeni ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Fatma M. Maghimbi , Mheshimiwa Dr. Hamza A. Mwenegoha , Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Wiliam H. Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Mbunge na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Waheshimiwa waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa na Mheshimiwa Felix N. Kijiko. Ni hawa wawili tu walichangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye michango yenyewe. Nikianzia na maoni ya Kamati, nawashukuru Wajumbe wote kwa kuniunga mkono. Maoni yao ni ya kiutendaji na ninapenda kumthibitishia Mheshimiwa Mwenyekiti kwamba bila shaka tutayafanyia kazi hususan hili angalizo la matumizi ya ushahidi wa elektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeonyesha hofu kwamba sheria hii inaweza kuwatia hatiani watu wasiohusika, mathalani wale ambao watajikuta Akaunti zao zimejazwa fedha na maharamia wa elektroniki *(hackers)* au kama alivyozungumzia Mheshimiwa Dr. Slaa. Lakini, nashukuru kwamba Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria amelielezea kwa ufasaha jambo hilo.

Lakini napenda tu kueleza kwamba, lengo halisi ni lile la kukataza watu kutenda kosa, la *Money Laundering*. Sasa, *Money Laundering* mara nyingi watu hutumia akaunti zao za Benki. Kwa hiyo, tunapozungumzia juu ya ushahidi wa elektroniki unaohusiana

na kosa hilo la *Anti-Money Laundering* tu, napenda kusisitiza kwamba kama kwenye Sheria ya Ushahidi ni kwamba lazima kosa lithibitishwe *beyond reasonable doubt*, yaani pasiwepo na mashaka yoyote ya maana. Kama kuna mashaka yoyote kwenye kosa lolote lile la jinai, basi mashaka hayo hupewa mshitakiwa. Kwa hiyo, itakuwa ni wajibu wa Mwendesha Mashitaka yeyote yule ambaye anapeleka Mashitaka ya aina hii Mahakamani, kuhakikisha kwamba analeta ushahidi ambao utathibitisha kwamba kosa lile kweli lilitendwa.

Kwa hiyo, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba hii Ibara tuliyopendekeza kuboresha sheria ya ushahidi, yaani ile *Section* ya 40(a), madhumuni yake ni hayo. Lakini ukweli ni kwamba, kuna mipaka mingi ambayo inabidi ivukwe kama mtu anaweza kuonekana kwamba ana hatia kwa kosa lile ambalo atakuwa amepelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa mmoja mwingine alieleza juu ya yale mafungu yanayohusu madaraka waliyopewa mapolisi. Vifungu vyote vile vinahusika, vinataja kwamba lazima Inspekta Jenerali au *DCI*, ndio waridhike kwamba kuna haja ya kufanya upelelezi ule ulioelezewa kwenye vile vifungu. Sasa, wale ni watu ambao kwa kweli wana *integrity* ya hali ya juu. Hawawezi kufanya kitu chochote kile ambacho kitaathiri wale ambao wanakwenda kufanyiwa upelelezi ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tahadhari zimechukuliwa, ndiyo sababu tumesema kwamba ni pale tu ambapo Inspekta Jenerali au *DCI* atakaporidhika kwamba kuna haja ya kufanya ule upelelezi na Maafisa ambao watatakiwa kufanya ule upelelezi ni wale ambao wako *beyond the rank* ya *Assistant Superintendent of Police*. Hawa watu pia sio watu wa chini, ni watu ambao pia wana *integrity*. Kwa hiyo sidhani kwamba wanaweza kuingiwa hivi kirahisi na watu ambao wana nia mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, hayo yote ambayo wameyazungumzia, tumeyatafakari wakati wa kutunga hii sheria. Kwa hiyo, naomba watusaidie tu kupitisha Muswada ili tuangalie mambo yatakavyokuwa, kama kutakuwa na matatizo yoyote katika utekelezaji wa hii sheria, basi tutarudi tena hapa kufanya mabadiliko kwenye vifungu hivi ambavyo tumevizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na yale ambayo alizungumzia Mheshimiwa Mwenegoha, kwamba Mahakama inatakiwa itoe kibali cha kushikilia akaunti ya huyu anayefanyiwa upelelezi kwa muda unaozidi siku saba. Anasema kwamba, ule muda ni mfupi sana, kwa hiyo Polisi watashindwa kufanya kazi yao vizuri. Sisi tunasema kwamba, kwa kweli tuliona kuna haja ya ku-*protect* watu ili kama kweli Mahakama itaona kwamba hamna haja ya maaskari kuendelea kushikilia Akaunti za yule mteja au *Documents* zake, basi Mahakama inaweza kusema lolote lile, inaweza kusema ama waendelee, au wasiendelee. Kama watasema wasiendelee, basi itabidi akaunti zile ziwe *released*.

Kwa hiyo, mimi nadhani kwamba hilo halina tatizo. Siku saba siyo siku chache sana. Nadhani maaskari wetu watahakikisha kwamba katika hizo siku saba watakuwa wamefanya vile vitu ambavyo wanatakiwa kufanya ili waweze kupata ruhusa ya Mahakama kama itabidi wawe na hizi akaunti zaidi ya siku saba. Kwa hiyo, mimi nadhani sheria ilivyo sasa hivi, inakidhi mahitaji yale ambayo ameyaelezea Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye hoja aliyotoa Mheshimiwa Shellukindo, napenda kumhakikishia kwamba hivi sasa tuna kitu kinaitwa *Legal Sector Reform Programme*. Katika *Legal Sector Reform Programme*, kuna *component* moja ya kuangalia sheria zote za nchi ili tuweze kurekebisha zile ambazo zimepitwa na wakati. Kwa hiyo, jambo ambalo alilizungumzia Mheshimiwa Shellukindo, sasa hivi tunalifanyia kazi. Kwa hiyo, asiwe na hofu. Napenda kumhakikishia kwamba Ofisi yangu itahakikisha sheria zote ambazo zimepitwa na wakati, zinaletwa mbele yenu hapa ili muweze kuzifanyia marekebisho na kuzi-*update* ziendane na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ile adhabu ya miaka mitano ambayo amesema kwamba itafanya majangili wajae, yaani kuhusiana na wale ambao wataingilia au watafanya vitendo vya kuwadhuru ambao watapeleleza kesi au wale Mahakimu au Waendesha Mashitaka, nasema kwamba, kwa sababu *Anti-Money Laundering* tunashughulikia watu hatari sana - matajiri. Sasa, ukiwaambia kwamba walipe faini ya Sh. 500,000/= au 1,000,000/=, hiyo ni mchezo kwao.

Kwa sababu ni watu ambao wamechukua hela chungu nzima kutoka nje au wapi, wameleta hapa kwa ajili ya kusafisha. Kwa hiyo, tulifikiri kwamba adhabu tuliyoweka kwenye sheria hii ambayo tunaleta mbele yenu sasa hivi ni adhabu ambayo ndiyo itaweza kukidhi mahitaji na kuweza kuwafanya hawa watu wasiweze kufanya vitendo vile ambavyo vitawadhuru wale ambao watakuwa wanashughulika na kesi hizi Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu alichosema Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, naungana na yale aliyosema Mheshimiwa Mathias Chikawe, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwamba nia yetu hasa kuleta sheria hii siyo kwenda kinyume na katiba ya nchi. Nia yetu siyo hiyo. Katiba ya nchi inaweka mipaka, kuna haki na wajibu. Kutoka Ibara 12 hadi 29 inaweka haki na wajibu. Lakini pia Ibara ya 30(ii) inaweka wazi matumizi ya mipaka hiyo. Inasema kwamba sheria ya Bunge hili inaweza kuweka mipaka na ndiyo sababu tumeleta hii sheria hapa kwa sbababu mambo ambayo tunataka kuyadhibiti ni mambo ambayo ni hatari kwa nchi yetu na sisi wote kwa pamoja.

Kwa hiyo, tulifikiri kwamba hii sheria yetu sasa itaweka mipaka hiyo kwamba mtu yeyote ambaye atafanya yale ambayo yamezungumzwa kwenye Ibara hizi ambazo ametaja Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, basi itabidi adhibitiwe. Sheria ya Ushahdi 40(a), mipaka iliyowekwa ni kwa ajili ya kutufanya sisi wote tuishi kwenye nchi ambayo haitakuwa inawalinda hawa ambao watakuwa wanafanya makosa haya ya hatari ya *Anti-Money Laundering*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna haja ya kuwalinda hawa watu wanaoleta habari *(Whistle Blowers)*. Kuna haja ya

kuwalinda. Kuna sheria ambayo itasomwa kwa mara ya kwanza nadhani katika Kikao hiki cha Bunge hili ya *Prevention and Combating of Corruption*. Kwenye sheria ile utakuta kuna kifungu ambacho tutakipendekeza cha kuwa-*protect* hawa watu. Lakini hao ni kwa ajili ya ile sheria tu. Tuko mbioni, mnakumbuka kwenye Kikao kilichopita tulivyokuwa tunaleta sheria ile ya *Anti-Money Laundering*, tulileta pia na marekebisho ya sheria mbalimbali ambazo zilikuwa zinahusu pia sheria ya *Criminal Proceedure Acts* ambayo tulikuwa tumependekeza kuwa-*protect* hawa watu, *Whistle Blowers*, mashahidi pamoja na Waendesha Mashitaka.

Sasa labda wakati ule tuliweka na wale ambao watapelekwa Mahakamani kushitakiwa kwa makosa kama yale. Kwa hiyo, mkatushauri kwamba hicho kifungu tukiangalie tena upya. Nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tutakiangalia upya tena kifungu kile pamoja na kuleta Muswada mwingine ambao utakuwa una-*protect* hawa *Whistle Blowers*. Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ni jambo ambalo tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nadhani nitakuwa nimeshajibu karibu yote ambayo yameelezewa na Waheshimiwa Wabunge. Mimi nawashukuru sana kwa michango yao. Naomba kwa radhi, tafadhari mturuhusu huu Muswada upite ili tuweze kuanza kufanyia kazi. Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana. Naomba kutoa hoja! *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

### Muswada wa Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbali Mbali Na. 2 wa Mwaka 2006 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 2 Bill, 2006*

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 13

*(Kifungu kilichotajwa hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Kufanya Marekebisho katika Sheria Mbali Mbali Na. 2 wa Mwaka 2006 *(The Written Laws Miscellaneous Amendments No. 2 Bill, 2006***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeufikiria na imeukubali Muswada huu pamoja na marekebisho yaliyofanywa. Hivyo natoa hoja kwamba Muswada wa *The Written Laws Miscellaneous Amendment Act No. 2* wa mwaka 2006 kama ulivyorekebishwa sasa ukubaliwe. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa upande wetu tumemaliza kupitisha Muswada huu, tunangoja tu *accent* ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nina matangazo yafuatayo:-

Kwanza, Mwalimu Msaidizi wa Bunge *Sports Club* anawatangazia Wabunge wote kuwa kesho tarehe 01 Februari, 2007 mazoezi yataanza rasmi kwenye uwanja wa Jamhuri na magari yatapita kama kawaida. Kwa kuzingatia michezo ni afya, tunawaomba wote wahudhurie uwanjani saa 11.30 alfajiri na zoezi litamalizika saa 1.00 asubuhi. Kwa hiyo, michezo ni furaha, nendeni mkafurahi kule.

Waheshimiwa Wabunge, lakini nina hoja nyingine ya kikanuni; Mheshimiwa Shibuda anauliza *very seriously,* anasema hivi; tunapewa *bills supplement* ya *the written laws miscellaneous amendment* kwenye *bill supplement* tu. Lakini sheria zenyewe za kimsingi hazipo. Hivi atawezaje kuunga mkono au kupinga makofi wakati sheria zenyewe za msingi hajaziona? Anaona tu hiki kitabu

Mimi nakubaliana na yeye kwamba hata sisi tulipoanza Bunge tulikuwa na maswali haya. Sasa fikiria hii ni *bills* 10 na mengine ma-*volume* yake haiwezekani humu ingekuwa sijui mngeweka wapi. Ndiyo maana mabunge yote lazima yawe na *library* na

ndiyo maana miswada inapaswa *first reading* ifanywe kikao kingine na Muswada uingie katika *second reading* kipindi kingine kusudi watu waweze kupata nafasi ya kufanya *reference* huko. Lakini siyo sisi kuingia na Miswada na ma-*book* yale ni mengi, Miswada kumi hapa hata mwenyewe sijui ingebidi toroli la namna gani kuijaza halafu hata wewe mwenyewe ingekuchanganya. Kwa hiyo, ndiyo hiyo inatumika.

Katika Mabunge yaliyoendelea, kwa kweli kuna *research department* kubwa na ndiyo maana tunatumia pia hata hii *public hearing* kusudi watu wenye taaluma hizo wanaijua Miswada hiyo mingine. Lakini wewe ukiletewa hapa utachanganyikiwa kuliko kufanya kitu chochote. Inakuwepo kwenye *library* na ndiyo maana tunatakiwa kuwa na muda mrefu wa kuweza kupata nafasi ya kufanya *research* na kuweza kuwa na maandalizi yetu ya kupitisha sheria. Hatuwezi kuleta *the original bills* ndani ya Nyumba, itakuwa haiwezekani.

Nadhani nimetosheleza hoja hiyo na sisi tulipokuwa tunaingia Bungeni madai yalikuwa ya namna hiyo. Lakini siku moja wakatuletea yale ma-*book* haikuwezekana, hata chumba cha Kamati kilijaa vitabu, haikuwezekana. Pia gharama, kwa sababu ku-*produce* vitabu vinavyolingana kufuatana na idadi yetu itakuwa vigumu. Kwa hiyo, tuna *library,* tuna *research service*, halafu tuna *time* yenyewe, *bills* zenyewe hatupendi sisi kuwa *bill* inasomwa na kuingia katika *stage* zote wakati mmoja inakuwa ngumu.

Baada ya kusema hayo, sina lingine. Naahirisha kikao mpaka kesho saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 01.03 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 01 Februari, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*